

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tano – Tarehe 9 Septemba, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Sita, Kikao cha leo ni cha Tano. Katibu.

#### NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

#### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WALEMAVU (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII):**

Maelezo ya Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadijishaji Hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII):**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

**MHE. PETER S. MSIGWA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

**SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Swali la kwanza la Mheshimiwa Japhery Raphael Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, nimekuona. Uliza swali lako sasa.

Na. 55

**Kupandisha Hadhi Zahanati Kuwa Vituo  
vya Afya - Moshi**

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL aliuliza:-**

Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa muda mrefu imekuwa na maombi ya kupandishwa hadhi kwa Zahanati za Msarango, Longuo B na Shirimatunda kuwa Vituo vya Afya:-

Je, ni lini Zahanati hizo zitapandishwa hadhi kuwa Vituo vya Afya?

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI majibu tafadhali, Mheshimiwa Sinkamba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Raphael Japhary Michael, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Moshi ina jumla ya Zahanati 31, 12 za Serikali, tatu za Mashirika ya Dini na 16 binafsi. Vituo vya Afya viko 10. Viwili vya Serikali, kimoja cha Shirika la Dini na saba ni vya watu binafsi; na Hospitali nne zote za Mashirika ya Dini ambapo Serikali imeingia mkataba na Hospitali ya St. Joseph kuwa hospitali teule kwa maana ya CDH.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mwongozo wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (*MMAM*) Kituo cha Afya kinapaswa kuhudumia wakazi kati ya 10,000 hadi 60,000. Zahanati inapaswa kuhudumia wakazi wasiozidi 10,000 na hospitali ina wakazi kuanzia 50,000 na kuendelea. Zahanati ya Msarango inahudumia wakazi 7,699, Longuo B wakazi 6,632 na Shirimatunda wakazi 4,485, hivyo, zinakosa sifa ya kupandishwa hadhi kuwa vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inasisitiza kujenga Vituo vya Afya vipyaa badala ya kuhuisha Zanahati izopo ili kuendana na ubora wa miundombinu inayohitajika na pia kuongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya na siyo kupunguza zahanati zilizopo ili kuongeza Vituo vya Afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhary Michael nimekuona, swalii la nyongeza.

**MHE. RAPHAEL H. MICHAEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ya Kikanuni, lakini kutokana na jiografia ya Manispaa ya Moshi, Kata ya Msaranga, Ng'ambo na Kibororoni zipo karibu na wananchi hawa wanashirikiana pamoja katika kutafuta huduma za afya. Sasa je, Serikali kwa maelekezo hayo kwamba wanahamasisha kujenga vituo vya afya, ni lini itatupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika Kata hiyo ya Msaranga ili tuweze kusaidia hizo Kata tatu kwa pamoja ili wananchi wapate huduma za afya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Manispaa ya Moshi tuna ombi la muda mrefu kwa Serikali kuhusiana na Hospitali ya Wilaya na kuna uhitaji mkubwa sana ili kusaidia wagonjwa ambao wamezidi Hospitali ya *KCMC* na Hospitali ya Mawenzi. Je, ni lini sasa ombi letu litakubaliwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI tafadhalii, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza anaongelea Kata mbili ambazo ziko tayari kushirikiana ili waweze kupata Kituo cha Afya. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali tuko tayari pale ambapo wazo limeanzia kwa wananchi na eneo linakuwepo na utayari wa wananchi katika kujenga Kituo cha Afya, nasi kama Serikali tunapeleka nguvu yetu.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili anaongelea juu ya suala zima la ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa ajili ya Manispaa ya Moshi. Katika jibu langu la msingi nimemwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba huduma kwa ajili ya sehemu ambazo hakuna Hospitali ya Wilaya zinapatikana na ndiyo maana sisi kama Serikali kwa kushirikiana na St. Joseph tumewapa hadhi ya

kuwa kama Hospitali ya Wilaya kwa ajili ya kutoa huduma hiyo, lakini itekelezwe kwa muda wa mpito pale ambapo Hospitali ya Wilaya haipo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali tuko tayari kama ambavyo tumeanza maeneo mengine, tutahakikisha kwamba hata Manispaa ya Moshi nayo inapata Hospitali ya Wilaya.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na swalilinalofuata ambalo ni la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, linaulizwa na Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka. Kwa niaba yake, nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Tabora, Viti Maalum.

Na. 56

#### **Zoezi la Ukamataji Waendesha Bodaboda**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA (K.n.y. MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA)** aliuliza:-

Waendesha pikipiki (bodaboda) nchini wamekuwa wakikamatwa na Askari wa Usalama Barabarani mara kwa mara kwa tuhuma za makosa mbalimbali:-

Je, zoezi hili la ukamataji wa waendesha pikipiki limefanikiwa kwa kiasi gani?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya chanzo cha ajali za barabarani huchangiwa na waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda. Mathalan mwaka 2016 nchini kote kulitokea jumla ya ajali za pikipiki 2,544 zilizosababisha vifo vya watu 890 na majeruhi 2,128. Mwaka 2017 zilitokea ajali za pikipiki 1,459 zilizosababisha vifo vya watu 728 na majeruhi 1,090. Mwaka 2018 zilitokea ajali za pikipiki 876 ambazo zilisababisha vifo vya watu 366 na majeruhi 694.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2019 kumetokea ajali za pikipiki 334 zilizosababisha vifo 176 na majeruhi 289. Ukililinganisha na kipindi kama hicho cha Januari hadi Juni, 2018 ambapo ajali zilitokea 408 zikasababisha vifo 165 na majeruhi 344, utaona kuwa ajali za pikipiki zimepungua sawa na asilimia 18 ingawa vifo viliongezeka kwa idadi ya 11 ambayo ni sawa na asilimia 6.6 na majeruhi kupungua kwa idadi ya 55 ambayo ni sawa na asilimia 16. Kwa ujumla takwimu hizi zinathibitsha kupungua kwa ajali za bodaboda barabarani ambazo zinatokana na waendesha pikipiki kutozingatia sheria.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa ajilia hizi ni mafanikio yanayopatikana kutokana na usimamizi wa Sheria za Usalama Barabarani kwa kuwachukulia hatua waendesha bodaboda ambao wanakiuka sheria na kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha Mahakamani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne Mcemba, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya kuhakikisha kwamba usalama wa barabarani unasimamia mazingira yote. Kwa kuwa usalama barabarani wanafanya kazi kubwa na kwa kuwa waendesha bodaboda kwa sasa pamoja na kupunguza ajali, wapo wanaovunja sheria na baada ya kuvunja sheria wao pia wanakuwa vyanzo vya watu kupata ulemavu: Je, Serikali inatoa adhabu gani kali kwa hao ambao wanavunja sheria?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha inasajili bodaboda zote hapa nchini ili kupunguza uhalifu na kupunguza ajali pale inapotokea wale wenye bodaboda wanapokimbia?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri wa Mambi ya Ndani, Mheshimiwa Eng. Masauni tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, aina ya adhabu zipo kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani lakini inategemea pia aina ya kosa la mhusika. Hata hivyo nikiri kwamba inawezekana adhabu hizo sasa hivi zikawa zimepitwa na wakati, ndio maana tupo katika hatua za mwisho za mchakato wa marekebisho makubwa ya Sheria za Usalama Barabarani. Ni imani yetu kwamba sheria hiyo itakapokamilika, inaweza ikasaidia sasa kuweka adhabu ambazo zitawabana zaidi wavunjifu wa sheria za usalama barabarani hususan waendesha bodaboda.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la usajili, nimhakikishie kwamba tupo katika hatua za kuanza mchakato huo tukiamini kwamba utaratibu huo utasaidia sana katika kupunguza malalamiko ya baadhi ya waendesha bodaboda ya uonevu wanaofanyiwa dhidi ya baadhi ya Askari wetu, lakini pia itasaidia sana kuweza kuwadhibiti na kuwakamata pale ambapo wanafanya makosa hayo kwa urahisi na uvunjifu wa Sheria za Usalama Barabarani kwa wanaotumia bodaboda.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa, uliza swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, yaani majibu yake, anasema kwamba ajali zimepungua lakini vifo vimeongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa idadi ya vifo ambavyo wamevitaja kuanzia mwaka 2017, 2018, 2019 hadi Juni

inaelekeea kwamba jumla ya vifo vilivyotokea ni 1,270. Hawa ni Watanzania, idadi ni kubwa. Mheshimiwa Naibu Waziri tuambie hasa mkakati wa ziada wa mwarobaini ili kukomesha vifo hivi visiendelee tena. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, niliposoma takwimu tokea mwaka 2016 mpaka 2019 kwa ujumla ajali, vifo na majeruhi vyote vinaonekana kushuka, lakini takwimu ambazo nilisema kwamba vifo vinaongezeka ni za kipindi cha Januari mpaka Juni 2019. Kwa hiyo, ni kipengele kimoja na cha kipindi kimoja ambacho tumeona kwamba upande wa vifo umeongezeka, lakini kwa ujumla ajali zimepungua.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza, haya ni mafanikio ya usimamizi wa Sheria ya Usalama Barabarani ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kupunguza ajali za barabarani ambaao tumeuandaa kuititia Baraza la Usalama la Taifa kwa maana mkakati huu umegusa katika maeneo mengi. Moja, ndiyo hili eneo ambalo nimezungumza katika jibu langu la msingi kwamba ni kuhakikisha kwamba Askari wetu wanasimamia Sheria ya Usalama Barabarani kwa nguvu zote na kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Ahsante. Tunahamia Wizara ya Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini.

Na. 58

**Ombi la Kuongezewa Ardhi ya Kilimo Kutoka  
Hifadhi ya Kalambo**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Wananchi wa Kijiji cha Kasapa walikuwa na ombi la kuongezewa maeneo ya kilimo kutoka kwenye eneo la hifadhi ya Kalambo *TFS*:

Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa ombi hilo la wananchi wa Kijiji cha Kasapa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Msitu wa *Kalambo River* ulihifadhiwa rasmi kwa kupitia tangazo la Serikali Na. 105 la mwaka 1957. Msitu huo upo katika Wilaya ya Kalambo na Nkasi Mkoani Rukwa na una jumla ya hekta 41,958.

Mheshimiwa Spika, hifadhi hii imekuwa na umuhimu wa kipekee kwa uhifadhi wa viumbi haia na vyenye umuhimu wa kipekee wakiwemo tembo. Aidha, hifadhi ina umuhimu mkubwa katika kutoa huduma za Kiikolojia kama maji. Maji haya ni muhimu kwa matumizi ya wananchi wa eneo hilo, pia kwa ajili ya maporomoko ya Kalambo ambayo ni pili kwa urefu mita 240 Barani Afrika baada ya yale ya Victoria yaliyoko Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, aidha, maporomiko ya Kalambo yana upekee kwa kuwa ni moja ya vivutio muhimu ambavyo vinaendelezwa kuchangia ukuaji wa uchumi kupitia Sekta katika Mikoa ya Rukwa na Katavi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 5 Julai, 2017 Waziri wa Maliasili na Utalii alitembelea Hifadhi ya Kalambo na baadaye Vijiji vyta Kisapa ili kusikiliza maombi yao ya uhitaji wa ardhi. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Waziri aliagiza *TFS* kushirikiana na Halmashauri kufanya upimaji na tathmini ya maeneo yanayolimwa na kutoa taarifa ya mapendekezo ya hatua stahiki zitakazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo hayo, TFSkwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ilifanya soroveya na kubaini kuwa maeneo mengi ya vijiji hivyo yamo ndani ya hifadhi ya misitu. Katika kushughulikia changamoto ya migogoro hiyo Mheshimiwa Rais aliunda Kamati ya Wizara nane kisekta kushughulikia migogoro baina ya wananchi na hifadhi. Mojawapo ya maeneo yanayofanyiwa kazi na Kamati hiyo ni pamoja na ombi la kuongezewa ardhi kwa wananchi wa Vijiji vya Kisapa na King'ombe. Taarifa ya Kamati imewasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kupata maelekezo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati tunasubiri maelekezo ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa mwuliza swali, uliza swali la nyongeza, Mbunge wa Nkasi Kusini.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nishukuru sana majibu mazuri ya Serikali, naomba tu utekelezaji uwe wa haraka kwa sababu msimu wa mvua karibu unafika. Katika operasheni zao mbalimbali, watu wa Maliasili wa *Luafi Game Reserve* wamekuwa wakiwafukuza wananchi usiku kwenye Vijiji vya King'ombe, Lundwe, Mlalambo, Kizumbi na Lupata: Je, utaratibu huo hauwezi kubadilika ili operesheni zao wafanye mchana ili sheria zifuate taratibu zake?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Kigwangalla alipofanya ziara Wilayani kwetu, aliahidi kutoa bati katika Kijiji China katika ujenzi wao wa zahanati: Je, bati hizi zitatolewa lini? (*Makofi*)

**SPIKA:** kwa kuwa Mheshimiwa Kigwangalla yupo, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, wanasema uliahidi bati huko. Ngoja ajibu mwenyewe. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba nijibu hili la bati, la kwanza atajibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba niwasiliane na Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili kwisha ili tuweze kuona hatua stahiki za kuchukuliwa ili ahadi hiyo iweze kutekelezwa mara moja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimuhakikishie kwamba kama kuna Askari wetu wa Wanyamapori badala ya kufanya *operation* mchana anakwenda usiku kufungua nyumba za watu anafanya makosa, maelekezo ambayo ninayatoa hapa ni kwamba *operation* hizo zifanyike mchana na zisifanyike usiku kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mipata, majibu yako umeshayapata tumalizie na Maliasili halafu tutamalizia lile swali la Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa hiyo, nimuite Mheshimiwa Dalaly Kafumu tafadhali Mbunge wa Igunga.

Na. 59

#### **Kupima eneo la Hifadhi ya Wembere**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Asilimia 70 au zaidi ya maeneo ya Kata za Isakamaliwa, Mbutu, Igunga, Nguvumoja, Lugubu na Itumba katika Jimbo la Igunga na Kata za Igoweko katika Jimbo la Manonga yapo ndani ya Mbuga ya Wembere ambayo kwa sasa imekosa sifa ya kuwa hifadhi ya wanyama na wananchi katika Kata hizo wameongezeka na kufanya kukosekana kwa maeneo ya makazi, kilimo na ufugaji na kwa kutokuwepo mipango mizuri ya matumizi bora ya ardhi kwa sababu ya hifadhi hiyo na kusababisha migogoro mikubwa kati ya wakulima na wafugaji na kuleta mauaji:-

Je, ni lini Serikali italitenga na kulipima eneo la Hifadhi ya Wembere hususan katika maeneo ya Kata hizo kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi?

**SPIKA:** Majibu la swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Pori Tengefu Wembere, Serikali inakusudia kulibadilisha hadhi pori hili kuwa Pori la Akiba. Katika zoezi hili alama za mipaka ya hifadhi na maeneo yanayopakana zitapitiwa na kuhakikiwa upya.

Mheshimiwa Spika, aidha, mipango ya matumizi bora ya ardhi hufanyika katika maeneo ya vijiji na husimamiwa na Wizara za Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wizara yangu iko tayari kushirikiana na mamlaka hizi na wadau wengine pale itakapohitajika.

Mheshimiwa Spika, mbuga ya Wembere ina ukumbwa wa kilimeta za mraba 8,784 na ilitambuliwa kisheria kuwa Pori Tengefu kwa Tangazo la Serikali Na. 269 la mwaka 1974, pori linapatikana katika Mikoa ya Singida (Wilaya ya Manyoni) na Mkoa wa Tabora (Wilaya za Igunga, Sikonge na Uyui).

Mheshimiwa Spika, Pori Tengefu Wembere ni ardhi oevu (Chepechepe) ambayo ni muhimu Kitaifa na Kimataifa kwa kuwa ni chanzo cha maji dakio na chujuo la maji ya Ziwa Kitangiri na Eyasi. Pori hili ni mazalia na ushoroba wa wanyamapori ambaao ni kiunganishi pekee cha mfumo wa ikolojia wa Hifadhi za Taifa ya Ruaha na Serengeti, mapori ya akiba ya Rungwe, Kizigo, Muhezi na Ugalla. Aidha, pori ni makazi na mazalia ya ndege wahamao ambapo mwaka

2001 utafiti wa Kimataifa ulibaini uwepo wa zaidi ya spishi 12 za ndege walio hatarini kutoweka.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, pori hili linatumika kwa uwindaji wa kitalii na utalii wa picha ambapo fedha inayopatikana hutumika kwa ajili ya uboreshaji wa huduma za jamii kupitia Halmashauri za Wilaya husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafumu nimekuona.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake nina maswali mawili ya nyongeza;

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye swalii msingi Kata za Isakamaliwa Mbutu, Igunga, Nguvumoja, Luguba, Itumba na Igoweko kwenye Wilaya ya Igunga zimo ndani ya Mbuga ya Wembere na mimi nilizaliwa na kukulia humo na kuna migogoro mikubwa sana ya wafungaji wakulima pamoja na mbuga hiyo.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza ni kwa nini ile Kamati ya Mawaziri iliyokuwa imeagizwa na Mheshimiwa Rais kupitia maeneo ya namna hii ili kutafuta suluhisho haikufika Igunga?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili ni lini Serikali itapima eneo hili kupunguza maeneo ambayo yamekosa sifa kuwapa wananchi, lakini maeneo ambayo yanahitaji kuhifadhi kama alivyoeleza umuhimu wake yaendeleee kutumika?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Constanine Kanyasu Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akifuatilia kwa umakini sana utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais kuhusu maeneo yote yenye migogoro na ambayo wananchi tayari

wamekwishaanza kuyatumia lakini yamepoteza hadhi ya kuifadhi. Kwa ujumla wake pamoja na Wabunge wengine taarifa hii kama nilivyojibu kwenye Swali la Mheshimiwa Mipata iko mezani kwa Mheshimiwa Rais na tunasubiri maelekezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kujibu swalı lake la kwanza Kamati ilipewa mwezi mmoja kuwa imekamilisha taarifa ya nchi nzima na kwa kweli haikuweza kuzunguka nchi nzima kufikia maeneo yote, lakini kwa kutumia mfumo wa Serikali ambayo ipo kila sehemu kupitia Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, Kamati ilipokea maeneo yote yenye malalamiko ya nchi nzima. Kwa hiyo, ninachowezza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba eneo hili pamoja na Kamati kutokufika katika eneo hilo, limo ndani ya mjadala ambao tuliuendesha katika Kamati ya Mawaziri Nane na majibu yatakapotoka itakuwa pamoja na eneo hili.

Mheshimiwa Spika, swalı lake la pili ni lini Serikali itaondoa maeneo ambayo yamepoteza hadhi ya uhifadhi. Yapo maeneo mengi nchi nzima yenye hali kama hii na ndiyo ambayo sasa hivi yamevamiwa na wananchi na tumeelekezwa na Serikali kuangalia kama yamepoteza hadhi tupendekeze kuyaachia ili wananchi waweze kuyatumia, pamoja na swalı lake la kwanza tunasubii maelekezo ya Kamati ambayo Mheshimiwa Rais aliunda.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana sasa tunarudi swalı ooh! Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri Tafadhali, sikuwa nimekuona.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Kafumu ambaye katika nyakati tofauti tofauti amewaleta wazee kutoka katika Kata zilizoathirika nami binafsi nimeonana nao na kuwapa ahadi

kwamba maombi yao yamefika mahala muafaka na tutayashughulikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kuongezea kwenye majibu mazuri aliyyoatoa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba katika mchakato wa kuchora ramani upya ya Pori Tengefu la Wembere ili kulipandisha hadhi sehemu yake kuwa Pori la Akiba tutazingatia maombi ya wananchi wa Kata ambazo zimetajwa, eneo la pori la akiba litakalobaki litakuwa dogo zaidi kuliko hili la *square kilometre* zaidi 8,000 liliopo sasa. Lengo hasa ni kubakisha walau eneo dogo ambalo litakuwa *intact* na ambalo tutalilinda ipasavyo kwa ajili ya faida za kiuhifadhi na hiyo *connectivity* kati ya hifadhi zilizopo kusini na hifadhi ambazo ziko upande wa Kaskazini, maombi ya wananchi yatazingatiwa na kwa hivyo eneo ambalo wanaweza kulitumia kwa kufuga kwa kilimo na kwa makazi litabaki kwa wananchi na watalishi kwa uhalali kuliko ilivyo sasa wananyanyasika.

**SPIKA:** Ahsante sana tunarudi swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis swali Na. 57 uliza swali lako samahani.

Na. 57

### **Uchakavu wa Nyumba za Askari Zanzibar**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Askari wa Jeshi la Polisi Zanzibar (Ziwani) wanakabiliwa na matatizo makubwa ya makazi kama vile miundombinu ya maji, nyumba chakavu, uhaba wa vyoo na kuharibika kwa uzio uliokuwepo katika eneo hilo unaohatarisha usalama wao:-

(a) Je, kuna mpango gani wa kufanyia matengenezo nyumba na vyoo kwa wakati huu?

(b) Je, Uzio wa boma hilo la Ziwani utafanyiwa ukarabati?

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Fakharia, majibu ya swali hilo la Kamishna wa Tume wa Bunge, Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linakabiliwa na tatizo la uchakavu wa miundombinu kama majengo ya ofisi na nyumba za kuishi Askari kutokana na kuwa ya muda mrefu. Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikifanya ukarabati wa miundombinu hiyo kwa awamu ili kuboresha huduma kwa wananchi Mheshimiwa Spika Mipango ya ukarabati ya miundombinu hiyo kwa awamu ili kuboresha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mipango ya ukarabati wa miundombinu katika Kambi hiyo imeanza kwa kuanda makadirio ya ukarabati kwa kuzingatia vipaumbele hasa kwa nyumba ambazo zimechakaa na ambazo zinaweza kukarabatika, mahitaji na gharama za majengo husika.

Mheshimiwa Spika, uzio wa Kambi ya Polisi - Ziwani ni wa fensi ya waya ambayo imezunguka eneo kubwa na waya huu katika baadhi ya maeneo ambao umechoka na kuchakaa kabisa. Aidha, upo mpango wa kujenga fensi ya matofali mara tu pale fedha zitakapokuwa zimepatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Sina budi kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jawabu alilonipa ambalo ni zuri na linaridhisha na kaamua kusema ukweli wake hali halisi ya Kambi hiyo, lakini ni nana maswali mawili ya nyongeza:

Kwa kuwa, uzio ambao ninaupigia kelele kila siku, sasa hivi wanataka waukarabati kufanya wa matofali na sasa bado upo wa waya, lakini hata hivyo wamejitalidi upande wa *School* ya Jang'ombe tayari wameufanya ukarabati, ningombaa na upande wa Matarumbeta, upande wa kwa Alinatu, upande wa Kwahani kwa sababu hizo njia za panya zimekaa sehemu mbaya na watu bado wanazitumia kama vichaka au njia za kupitia wangelifanya kila mbinu na sehemu hizo wakafanya ukarabati kabla hata kufanya ukarabati huo utakaozungushwa kwa matofali.

Swali la pili, kwa kuwa tayari amekubali kwamba nyumba za kambi hizo zote zimechakaa na kweli zimechakaa, maana zimejengwa kabla ya Mapinduzi ya 1964 na kwa kuwa nyumba hizo hasa zili wanazokaa Askari wa wa kawaida siyo Maofisa ambao ni kama mabanda nyumba hizo zimechakaa na haziridhishi kukaa binadamu ningombaa angalau wangeanza kuzifanya ukarabati hizo ili Askari wetu wakaishi maisha bora.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Injinia Masauni, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Fakharia kwa jitihada zake kubwa anazochukua katika kukabiliana na changamoto mbalimbali katika Majimbo ya Mkoa mzima wa Mjini. Mimi ni shahidi ni Mbunge ambaye anashirikiana nami vizuri katika Jimbo langu ambalo lipo katika Mkoa wake katika kukabiliana na changamoto hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo za dhati kwa Mheshimiwa Fakharia naomba sasa nijibu maswali yake kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa amekiri ameridhishwa na jitihada ambazo tumeshaanza kuchukuwa katika

kukarabati uzio kwa upande uliopo karibu na school ya Jang'ombe nimhakikishie kwamba jitihada hizo ambazo zimeanza ndizo ambazo tutaendelea nazo katika kukamilisha uzio wote lakini pamoja na kukarabati nyumba za Askari Polisi pale ambapo fedha zitakapokuwa zimepatikana kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa swali linaulizwa na Mheshimiwa Kanali Mstaafu Mosoud Ali Khamis Mbunge wa Mfenesini.

Na. 60

**Raia Kupewa Nyumba za Askari**

**MHE. KANALI (MST.) MASOUD ALI KHAMIS** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikijitahidi kujenga nyumba kwa ajili ya wapiganaji wake ili waishi kambini kama taratibu za Jeshi zinavyoelekeza:-

(a) Je, kwa nini sasa nyumba nyingi katika Kambi za Jeshi wanapewa wafanyakazi 'Raia Jeshini' kwa ajili ya kuishi?

(b) Je, wafanyakazi raia wana haki ya kupewa nyumba za kuishi za Askari?

(c) Je, kwa nini Askari wanaruhusiwa kuzihama nyumba zilizojengwa kwa ajili yao na kuhamia katika nyumba binafsi?

**SPIKA:** Majibu ya maswa hayo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dkt. Hussein Mwinyi tafadhalii.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kanal (Mstaafu) Masoud Ali Khamis Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, raia wanaofanya kazi Jeshini hupewa nyumba za kuishi kwa mujibu wa Kanuni za Majeshi ya Ulinzi ya Wananchi wa Tanzania. Aidha, ugawaji wa nyumba hizo unategemea na uwezo uliopo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Majeshi ya Ulinzi ya Wananchi wa Tanzania Juzu ya kwanza (Utawala), Ibara ya 21.30 Makazi ya waliooa kutumia Raia, Kifungu Kidogo cha Kwanza (1) kinasema, bila kuathiri maagizo yoyote yaliyotolewa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, wakati makazi yanayofaa ya kiraia hayapatikani, Kamanda wa Kituo, Kikosi au sehemu nyingine anaweza kumgawia makazi ya waliooa raia ambaye ni Mtumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye anajaza nafasi katika Muundo wa Jeshi na ambaye si kibarua.

Hali kadhalika, Juzu ya Kwanza (Utawala) Ibara Ndogo ya Pili inaeleza kuwa, kwa idhini ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Kamanda Kituo Kikosi au sehemu nyingine anaweza kumgawia makazi ya waliooa raia, mbali na yule aliyetajwa katika sehemu ya kwanza ya aya hii, wakati kazi zake ni zile ambazo zinachangia ufanisi au maslahi ya kituo, kikosi au sehemu nyingine, endapo makazi yanayofaa ya kiraia hayapatikani anaweza kupewa nyumba kuwa makazi.

(c) Mheshimiwa Spika, Maafisa au Askari wanaruhusiwa kutoka kambini au vikosini na kuhamia katika nyumba zao binafsi. Aidha, hulazimika kubaki kambini au vikosini kutokana na sababu maalum za kimajukumu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kanali Mstaafu swali la nyongeza.

**MHE. KANALI (MSTAAFU) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo yamefafanua na itawasaidia wale ambaao walikuwa na utata kuhusu jambo hili, lakini pia nina swali moja la nyongeza;

Mheshimiwa Spika, nyumba nyingi za Jeshi wanazoishi Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania kupata athari

na kuharibika wakati mwingine hufika wakati hawa wakashindwa hata kuishi Askari. Je, Serikali haioni sasa umefika muda wa kuwapa uwezo wanaoishi katika nyumba hizi kuzifanyia matengenezo kwa kupitia kitengo cha ujenzi ndani ya Jeshi, kuzifanyia tadhimini na baadaye kumruhusu anayeishi kufanya matengenezo na kumrudishia hela zake. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa Dkt. Hussein Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, wazo hilo ni nzuri, kwamba kitengo cha ujenzi cha Jeshi kifanye tathmini na kuwaruhusu wanaoishi wazitengeneze na kisha kulipwa lakini utekelezaji wake una shida kidogo kwa sababu ya uwezo wa kulipa fedha hizo, ndiyo maana sasa hivi kupitia bajeti ya *maintenance* ya Ngome tunafanya ukarabati mdogo mdogo kwa maofisi na makazi ya Wanajeshi katika kambi mbalimbli lakini kasi yake ni ndogo kutokana na uwezo uliopo. Kwa hiyo, wazo hili linapokelewa na pale uwezo utakapo ruhusu basi litafanyiwa kazi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Tunaamia Wizara ya Fedha na Mipango ambayo ina maswali matatu kwa siku ya leo, tunaanza na swali la Mheshimiwa Joyce Sokombi, uliza swali lako.

Na. 61

#### **Malipo ya Wastaifu wa Kiwanda cha *MUTEX***

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Wafanyakazi wa Kiwanda cha *MUTEX* ambacho kilifungwa tangu mwaka 1984, wamekuja kulipwa stahiki zao Disemba, 2018 na badala ya kulipwa shilingi 400,000/= kwa gharama ya kila mwezi wakalipwa shilingi 100,000 tu:-

Je, Serikali haioni kuwa inawakandamiza wastaifu hao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisimamisha uzalishaji katika kiwanda cha Nguo cha Musoma (*Musoma Textile Mills Limited – MUTEX*) mwaka 1994 baada ya kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mtaji na ongezeko kubwa la madeni kutoka iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*). Kiwanda cha *MUTEX* kilifilisiwa na hatimaye kuuzwa mwezi Machi, 1998 kwa Kampuni ya *LALAGO Cotton Ginnery and Oil Mills Company Limited*.

Mheshimiwa Spika, kikao kati ya wadai, Serikali na Mfilisi kilifanyika Septemba 23, 2005 na kuridhia mapendekezo ya kulipa kiasi cha shilingi 161,347,359 kwa wafanyakazi 935 walilokuwepo kiwandani wakati Serikali ilipofanya uamuvi wa kusitisha uzalishaji. Maamuzi ya kulipa kiasi hicho cha fedha yalizingatia sheria, kanuni na taratibu za ufilisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi la ufilisi kukamilika, wafanyakazi 512 pekee ndiyo waliojitokeza kuchukua mafao yao na wafanyakazi 423 waligoma kupokea mafao yao kwa madai kwamba, nauji ya familia na gharama za kusafirisha mizigo ni ndogo. Wafanyakazi hao 423 walifungua kesi katika Mahakama ya Kazi ya Tanzania, shauri la Uchunguzi wa Mgogoro Na. 49 wa mwaka 2007. Mahakama ilitoa tuze mnamo tarehe 10 Juni, 2008 na kutupilia mbali shauri hilo na kuamuliwa wadai waende kwa Mfilisi kuchukua stahili zao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wafanyakazi hao hawakuridhika na uamuvi wa Mahakama na kufungua shauri lingine la kuomba marejeo katika Mahakama ya Kazi Tanzania shauri la Maombi ya Marejeo Na. 77 la Mwaka 2008. Mahakama hiyo ilitoa tuze tarehe 15 Februari, 2010 na kutupilia

mbali shauri la marejeo. Uamuzi ukabaki kuwa wafanyakazi hao 423 waliogoma kuchukua mafao yao waende kwa Mfilisi kuchukua stahili zao kama ilivyokubalika katika kikao cha wadau.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kupokea maombi ya malipo kutoka kwa wafanyakazi hao mwaka 2018, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifanya uhakiki wa wafanyakazi hao ili kujiridhisha na hatimaye kufanya malipo. Awali jumla ya wafanyakazi 219 walijitokeza na wasimamizi wa mirathi 14 na hivyo kulipwa jumla ya shilingi 44,591,559. Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifanya tena zoezi la uhakiki mwezi Juni, 2019 kwa wafanyakazi ambao hawakujitokeza kwa uhakiki wa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika zoezi hilo, jumla ya wafanyakazi 115 walijitokeza tena pamoja na wasimamizi wa mirathi 27 ambao kwa ujumla wanastahili kulipwa shillingi 20,738,863. Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea na taratibu za kulipa fedha hizo kwa wahusika katika mwaka huu wa Fedha 2019/2020. Aidha, Serikali inafuatilia kwa karibu malalamiko yote yanayohusu tofauti ya kiwango cha malipo yaliyofanyika hivi karibuni ikilinganishwa na kiwango kilichoidhinishwa kwenye kikao cha pamoja kati ya Mfilisi, wadau pamoja na Serikali kuona kama yana msingi na ukweli wowote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sokombi.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, niseme tu, sawa majibu ni marefu lakini hayajaniridhisha. Kwa mujibu wa sheria Mfilisi anapofilisi kiwanda au anaponunua kiwanda ni lazima kuwalipa wafanyakazi wote malimbikizo ya madai yao yote. Je, ni sahihi madeni ya msingi ya wale wananchi yapotee bure?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; hivi Serikali ilichukua hatua gani ili kwa aliyenunua kile kiwanda kuhakikisha wanawalipa wafanyakazi wale stahili zao zote toka shilingi 400,000, hatimaye wakawalipa laki moja, zile laki tatu zitalipwa lini? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha tafadhali, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali haiko tayari kuona Mtanzania yeyote wa aina yeyote akipoteza stahiki zake mahali popote ndiyo maana kwenye jibu langu la msingi nimeeleza kwa urefu jitihada zote ambazo Serikali imechukua kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ufilisi. Kwa hiyo, hakuna Mtanzania yeyote au mtumishi yeyote wa kiwanda hiki ambaye stahiki zake zitapotea.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza wazi; watumishi 512 walilipwa tangu mwaka 1994 kulingana na sheria, kanuni na taratibu zinavyoelekeza, hawa waliokataa wamekwenda mahakamani zaidi ya mara mbili na wote mahakamani walikokwenda malalamiko yao yametupiliwa mbali, wameelekezwa kurudi kwa mfilisi. Ni mfilisi ndio anayetoa fedha hizi za kulipa baada ya kuwa ameshalipa madeni mbalimbali ambayo kiwanda hiki kilikuwa kinadaiwa, kinachobaki ndicho wanacholipwa watumishi hawa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameuliza aliyenunua kiwanda hiki anatakiwa kulipa. Kulinaganga na sheria na kanuni na taratibu za ufilisi anayetakiwa kulipa siyo aliyenunua kiwanda, aliyetakiwa kulipa ni Serikali kwa sababu Serikali ndiyo iliyokuwa inamiliki kiwanda hiki na ndiyo maana mpaka leo Ofisi ya Msajili wa Hazina inashughulikia watumishi 312 waliobaki ili wakiwa tayari waweze kulipwa shilingi milioni 20 kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi. Kwa hiyo aliyenunua kiwanda hiki hana *liability* yoyote ya kuwalipa watumishi hawa na Serikali tuko tayari kuwalipa kwa wakati wowote.

**SPIKA:** Swali linaliofuata katika Wizara hii hii la Mheshimiwa Issa Mangungu; Mheshimiwa Mangungu uliza swali lako.

Na. 62

### **Kodi ya Majengo**

**MHE. ISSA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Tangu *TRA* ianze kukusanya kodi ya majengo imekusanya kiasi gani katika Mkoa wa Kodi Temeke kwa mwaka 2017/2018 na ni asilimia ngapi ya lengo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilianza kukusanya kodi ya majengo (*property rate*) katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 baada ya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura 290 kufanyika kuititia Sheria ya Fedha ya mwaka 2016. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Mkoa wa Kikodi wa Temeke ulikusanya jumla ya shilingi 3,707,731,450 ikiwa ni sawa na asilimia 60 ya lengo la kukusanya jumla ya shilingi 6,197,367,187.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, umepata hizo takwimu?

**MHE. ISSA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, lakini ningemuomba Mheshimiwa Waziri kama atakubali ombi langu la kuongozana na mimi ili akaangalie jinsi gani wananchi wanavyokadiriwa makadirio ya juu yasiyokuwa na haki na kuropa usumbufu mkubwa hasa wale ambao wanaishi katika maeneo ambayo hayajapimwa.

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili; je, ni lini Serikali itaifanya sasa Wilaya ya Mbagala kuwa mkoa wa kikodi ili waweze kukusanya vizuri kodi katika maeneo yasiyopimwa, yameachwa kwa asilimia nyingi sana na wanashindwa

kufikia huko kwa sababu *TRA* hawana *man power* ya kutosha? Kama hawawezi basi warudishe kwenye halmashauri zetu ili waendelee na zoezi hili.

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, endapo *TRA* hawawezi, tafadhalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza, wananchi kukadiriwa gharama kubwa kwa ajili ya kulipa kodi ya majengo. Naomba niwaambie wananchi wa Tanzania kwamba dhamira njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli ya kuhakikisha Watanzania hawaumizwi tena na kodi hizi tayari Bunge hili lilishapitisha sheria.

Mheshimiwa Spika, sasa kila jengo ambalo ni la chini ni shilingi 10,000 kwa hiyo hakuna anayelipa zaidi ya 10,000 kwa kila jengo ambalo ni la chini na kwa majengo ya ghorofa kwa kila ghorofa moja naomba niwaambie Watanzania kwa kila *floor* ya ghorofa lako ni shilingi 50,000 kwa hiyo hakuna makadirio yoyote ambayo yako juu na Mheshimiwa kaka yangu Issa Ali Mangungu niko tayari kwenda na wewe Mbagala tukaongee na wananchi wetu tuwaeleweshe nini dhamira ya Serikali yao na nini tumeanza kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili; hili ni jambo la kiutaratibu, naomba nilichukue tutakwenda kulifanya kazi ili tuone ni lini sasa Wilaya ya Mbagala inaweza kuwa sasa ni Mkoa wa Kikodi ili tuweze kushughulikia ukusanyaji wa kodi hii kwa ufanisi.

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum; uliza swali lako Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia mwaka mwingine tena, leo ni siku yangu ya kuzaliwa. (*Makofii*)

Na. 63

## **Uhitaji wa Mifumo ya ATM Inayokidhi Mahitaji ya Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

*ATM* za Benki nyingi hapa nchini hazikidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa *ATM* za Benki zinawekewa mifumo inayokidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji tafadhalli.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali ilipoanza maboresho ya mifumo ya malipo nchini mwaka 1996, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kusimamia usimikaji wa mifumo ya kisasa, mahiri na salama ili kuendana na mahitaji ya soko na mabadiliko ya teknolojia. Maboresho hayo ya mifumo yanalenga pamoja na mambo mengine kukidhi mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii wakiwemo watu wenye mahitaji maalum, hususan walemaru.

Mheshimiwa Spika, Mei, 2017 Benki Kuu ya Tanzania ilitoa mwongozo wa mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao ikiwa ni mpango wa Serikali wa kuhakikisha kuwa huduma za malipo kwa njia ya mtandao yanafanyika kwa usalama na kukidhi mahitaji ya makundi yote katika jamii. Miongoni mwa vipengele muhimu na nyeti, hususan kwa watu wenye ulemavu vilivyoainishwa kwenye mwongozo huo ni alama

za utambuzi, usalama wa mifumo na uwezo wa mifumo wa kutunza siri za wateja. Pamoja na Serikali kutoa mwongozo huo, benki zetu zote hapa nchini hazijafanikiwa kusimika *ATM* maalum na rafiki kwa watu wenye ulemavu, hususan watu wenye ulemavu wa macho. Hii ni kutohana na ukweli kwamba teknolojia ya *ATM* kwa watu wenye ulemavu wa macho ni ngeni na pia ina mfumo au mahitaji ya ziada ikilinganishwa na *ATM* za kawaida.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya uduni wa baadhi ya miundombinu kwa watu wenye ulemavu, hususan walemavu wa miguu imetatuliwa kwa sehemu kubwa na hivyo kuwa rafiki katika maeneo mengi yanayotoa huduma za kibenki kwa kutumia mashine za *ATM*. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu suala hili ili kuhakikisha kuwa mifumo ya miamala kwa njia ya *ATM* inakuwa rafiki kwa makundi yote wakiwemo watu wenye ulemavu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, *okay, uliza swali lako la nyongeza.*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa unyenyekevu mkubwa ninakupongeza wewe, na nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kuwa mfano bora kutohana na miundombinu ya taasisi unayoingoza, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa rafiki, kila sehemu unapokwenda kwa kweli imejali mahitaji ya watu wenye ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati ninakupongeza na ninaomba taasisi nyingine waige mfano katika Bunge ambapo miundombinu kwa watu wenye ulemavu imezingatiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali yangu mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri kwa Naibu Waziri na kwa Serikali pia. Kama alivyosema kwamba Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu suala hili, ninapenda kufahamu sasa ni lini basi utekelezaji wake utakamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; baadhi ya benki hapa nchini pamoja na kwamba zimejali mahitaji ya watu maalum, hasa walemaru wa viungo, lakini bado *ramps* zilizojengwa zina mteremko mkali ambao ni hatari zaidi kwa watu wenye ulemavu. Je, ni hatua gani sasa zinachukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba, ikiwa ni pamoja na kutoa maagizo kwa wafanyakazi au wahudumu wa benki kuwahudumia watu wenye ulemavu kwa kuwafuata nje na kuwapa huduma hiyo pale wanapofika katika benki hizo?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ameuliza ni lini basi utekelezaji utakamilika. Kama ambavyo nimesema kwenye jibu langu la msingi, Serikali tunaendelea kufuatilia na nimeeleza wazi kwamba miundombinu hii ina gharama kubwa, hasa hii yenye nuktanundu kwa ajili ya ndugu zetu ambao wana mahitaji maalum, hasa walemaru wa macho. Serikali tunaendelea kufuatilia kwenye mabenki yote ili kuhakikisha angalau katika ATM hizi wanafunga kwa ucharaka mashine hizi ili kuwasaidia ndugu zetu waweze kupata huduma stahiki.

Mheshimiwa Spika, na hili alilolisema naomba nizielekeze benki zote nchini na naamini kwa Utanzania wetu, kwa utamaduni wetu tulivyolelewa Watanzania, huduma hizi zinatolewa, mtu mwenye ulemavu anapokuwa kafika benki kuhitaji huduma hizi watumishi wa benki zetu wamekuwa wakiwahudumia wakitoka nje kwenda kuwahudumia. Naomba tu nisisitize kwa zile benki na taasisi za kifedha ambazo hawajaanza kufanya huduma hizi basi waweze kuwahudumia ndugu zetu kutokana na uhitaji huo, nawaomba sana, na haya yachukuliwe kama maelekezo ya Serikali. Wakati huohuo benki zote kwenye miundombinu ya kuingia kwenye ATM ambapo wametengeneza *step slopes* basi warekebishe ili iwe rahisi kwa ndugu zetu wenye ulemavu kuweza kufikia huduma hizi kwenye mashine hizi.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Venance Mwamoto, swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya watu wenyewe ulemavu naomba niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na uhakiki wa simu, uhakiki wa *passports* zetu na shughuli za kibenki. Na kuna walemovu wengi ambao hawana vidole, na wanatumia vidole ili kuhakiki; je, Serikali imeweka mpango gani madhubuti wa kuhakikisha watu wenyewe ulemavu wanapata haki zao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Waheshimiwa nawaona wengine mmesimama huko sijui kuna nini. Endelea na majibu Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea changamoto hii na ninaomba tufanye kazi kwa pamoja Wizara yetu ya Fedha, hasa kwenye taasisi zetu za kifedha na mabenki yetu na Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano ili tuone jambo hili tunalishughulikia kwa haraka na ndugu zetu hawa waweze kupata huduma hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata ambalo linalekezwa kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, nalo linaulizwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Wanasi Konge; Mheshimiwa Kakunda.

Na. 64

#### **Matangazo ya *TBC* Kutosikika Kitunda – Sikonge**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

(a) Je, ni sababu zipo zinazosababisha matangazo ya Shirika la Habari Tanzania (*TBC*) hasa upande wa *Radio yasisikike* kwenye Tarafa za Kitunda na maeneo mengi ndani ya Jimbo la Sikonge?

(b) Je, ni lini Serikali itarekebisha tatizo hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Juliana Shonza.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuipongeza Timu yetu ya Taifa, *Taifa Stars*, kwa kutuheshimisha sisi kama Taifa kwa kuitoa Timu ya Burundi kwa mikwaju ya penati na hatimaye kuweza kutinga kwenye hatua ya makundi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye swali; kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TBC* kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 ilitekeleza mradi wa upanuzi wa usikivu katika wilaya tano zilizopo mipakani mwa nchi yetu; wilaya hizo ni pamoja na Wilaya ya Longido Mkoani Arusha, Wilaya ya Rombo Mkoani Kilimanjaro, Wilaya ya Tarime Mkoani Mara, Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma na Wilaya ya Kibondo Mkoani Kigoma. Aidha, Bajeti ya Mwaka 2017/2018 *TBC* ilitekeleza mradi wa upanuzi wa usikivu katika Mkoa wa Mtwara na Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga. Hadi kufikia tarehe 04 Mei, 2019 shirika lina vituo 33 vya kurushia matangazo katika masafa ya *FM* kwenye wilaya 102.

Mheshimiwa Spika, *TBC* inaendelea na mpango wa kupanua usikivu maeneo yote ya nchi nzima, kutegemeana na upatikanaji wa fedha ili kukamilisha wilaya zote 59 ikiwepo Wilaya ya Sikonge. Aidha, *TBC* ina mpango wa kufanya maboresho katika mitambo yake iliyopo Tabora *Kaze Hill* kisha kufanya tathmini ya usikivu na kubainisha maeneo

yanayopaswa kufungiwa mitambo mingine ili kuleta usikivu Mkoa mzima wa Tabora ikiwepo Wilaya ya Sikonge.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020, *TBC* inaendelea kutekeleza mradi wa upanuzi wa usikivu katika maeneo ya Mikoa ya Uguja, Pemba, Simiyu, Njombe, Songwe pamoja na Lindi. Mkakati wa Serikali ni kuiwezesha *TBC* kufikia usikivu katika maeneo yote ya Tanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda, nimekuona, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla kwa sababu wameelewa muktadha wa swali langu; halikuhusu jimbo langu peke yake bali lilihusu maeneo yote ambayo hayana usikivu wa *TBC* nchi nzima, na ameeleza mipango mizuri sana ya Serikali. Kwa hiyo, kwa kweli kwa muktadha na umuhimu wa *TBC* ninaamini kwamba Serikali sasa itaendelea kuongeza bajeti kuhakikisha kwamba mipango hii inatekelezeka. Kwa hiyo, nakubaliana na majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Devotha Minja nilikuona una swali la nyongeza.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa Redio Tanzania inaendeshwa na kodi za Watanzania na kwa sasa ni zaidi ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Redio Tanzania lakini maeneo ya pembezoni haisikiki na watu wanalazimika kusikiliza redio za nchi jirani. Hivi tunakwama wapi? Ni kwa nini *TCRA* isiondoe vikwazo kwa redio binafsi ili zipewe jukumu la kuhakikisha zinatoa huduma na kuwafikia Watanzania katika maeneo yote nchini? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Juliana Shonza.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri amependeza. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:** Mheshimiwa nashukuru, hizi zote ni neema za Mwenyezi Mungu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Devotha Minja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nitumie fursa hili kumtoa hofu kwamba *TCRA* kwa maana ya Serikali hajjaweka vikwazo kwa redio yoyote ya binafsi kuanzisha vituo vyake vya redio. Mara zote sisi kama Wizara ambao tunasimamia masuala yote ya habari lakini kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mawasiliano, tumekuwa tukisisitiza kwamba milango iko wazi kwa mtu na taasisi yoyote ambayo inataka kuanzisha redio waweze tu kufuata zile taratibu ambazo zinatakiwa katika kuanzisha redio hizo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, sisi kama Wizara ambao tunasimamia masuala ya habari nchini Tanzania tumekuwa tukihakikisha kwamba maeneo yote ya mipakani yanafikiwa na usikivu wa Redio yetu ya Tanzania. Katika kuthibitisha hilo, kwenye jibu langu la msingi nimesema wazi kwamba katika bajeti ya mwaka 2016/2017, *TBC* ilifanya uwekezaji mkubwa sana katika maeneo yote ya pambezoni ikiwemo katika wilaya zote ambazo zipo mipakani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali tunatambua *concern* yake kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa kuboresha usikivu wa *TBC* pamoja na Redio Tanzania katika maeneo yote ya mpakani.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na maswali baada ya dakika mbili, tatu, lakini naomba nichukue nafasi yenu fupi kuwalishwa kwamba ninaye mgeni maalum kabisa niliyemualika atembelee Bunge na kwa hiyo ningeomba nimtambulische na yuko kwenye Jukwaa la Spika, naye si mwagine isipokuwa ni Mheshimiwa Dkt. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya. (*Makof/ Vigelegele*)

Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya nimemwalika maalum kabisa hasa kwa Wabunge vijana muweze kumfahamu. Huyu ni Mbunge ambaye alitumikia Ubunge mfululizo kwa miaka 45. Hiyo ni rekodi ambayo wengine hapa hata mtambikie hamfikii. (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya ametumikia Ubunge kwa miaka 45, toka mwaka 1965 hadi mwaka 2010 akiwa Mbunge na alianza na akiwa Mbunge wa Jimbo la Ufipa Kusini enzi hizo ambalo leo sijui ni Majimbo mangapi ya kule, wako Wabunge kadhaa kwa Majimbo ya enzi hizo hivi sasa.

Pia, Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya katika maisha yake amewahi kuwa Mkuu wa Mkoa katika Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Kigoma na Rukwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya amewahi kupata tuzo na nishani mbalimbali za utumishi. Mwaka 1984 alipata tuzo ya Mwalimu Nyerere kwa kufanikisha kwa vitendo utekelezaji wa Sera ya Viwanda Vidogovidogo Nchini. Mwaka 1992 alitunukiwa na Umoja wa Vijana Nishani ya Mlima Kilimanjaro kwa kutambua mchango wake katika kufanikisha maendeleo ya kilimo na viwanda nchini. Mwaka 1993, Rais Mstaifu Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi alimuandikia barua ya kumpongeza kwa kuwa Mkuu wa Mkoa aliyeonesha utendaji bora wa kazi akiwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na Rukwa. (*Makof*)

Mwaka 2005, Rais Mstaifu Mheshimiwa Benjamin Mkapa alimwandikia barua ya kutambua mchango wake

katika mapambano dhidi ya rushwa kwa njia ya vitendo. Mwaka 2010, Marehemu Mheshimiwa Spika Samuel Sitta alimpa Hati Maalum ya Kutukuka katika kulitumikia Bunge kwa muda wa miaka 45. (*Makof*)

Hapa Mheshimiwa Mkapa alipomwandikia barua ya kutambua mchango wake katika mapambano dhidi ya rushwa, ni kwamba akiwa Mbunge kuna wakati aliwahi kuitwa 'Mzee wa Kulipua Mabomu'. Akiwa hapa Bungeni aliwahi kuibua ndani ya Bunge kashfa ilioitwa ya sukari ambayo ilimkabili Mheshimiwa Waziri Iddi Simba wakati ule akiwa Waziri wa Viwanda na Biashara iliyopelekea kujiuzulu wadhiba wake wa Viwanda na Biashara. Wabunge waliokuwepo wakati ule ni wachache wanaweza wakakumbuka shughuli ilivyokuwa pevu tukiwa kwenye ukumbi ule mwingine mdogo. (*Makof*)

Pia, aliwahi kuibua kashfa iliyomkabili Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Prof. Simon Mbilinyi, iliyopelekeea kujiuzulu wadhaba wake Waziri wa Fedha kufuatia sakata la misamaha katika uingizaji wa sukari nchini. Vilevile, kuliwahi kuibuka kashfa nzito humu iliyomkabili aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga kuhusiana na masuala ya vitalu na ilikuwa ni chupuchupu, ni hatihati humu ndani.

Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya katika maisha yake ameshaandika vitabu. Kimoja ni Joka la Vichwa Saba na kingine ni Wawindaji Kumi Msigombee Sungura Mmoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya ana Shahada ya Heshima ya Uduktari, kwa hiyo ni Dkt. Chrisant Mzindakaya. Hivi sasa mwanasiasa huyu mstaafu ni mwekezaji katika sekta ya mifugo, ni mjasiriamali anayemiliki kiwanda cha nyama na ni mfugaji mkubwa kule Rukwa ambaye anamiliki ranchi. (*Makof*)

Nichukue nafasi hii kumkaribisha sana Dkt. Mzindakaya. Karibu tena katika viwanja hivi ulivyokaa kwa

miaka mingi sana. Naomba tumpigie makofi ya kumkaribisha. (*Makofi/Vigelegele*)

Ahsante sana, basi Waheshimiwa na wengine tufuate nyayo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na maswali ya Wizara ya Maji, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa uliza swali lako.

Na. 65

### **Ujenzi wa Bwawa la Matwiga – Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Ujenzi wa Bwawa la Matwiga Wilayani Chunya umechukua zaidi ya miaka mitano bila kukamilika:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi huo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Aweso, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Mwambwalaswa, Mbunge wa Jimbo la Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa wilaya zenyeye asilimia ndogo ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini. Changamoto hii inatokana na wilaya hiyo kuwa na uhaba mkubwa wa vyanzo vya maji ikiwemo mito na chemchem ambazo zingeweza kutumiwa kuhudumia wananchi. Aidha, wilaya hii pia inakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji chini ya ardhi. Kwa kutambua hilo, Serikali ilianza ujenzi wa mradi wa maji wa Bwawa la Matwiga kwa lengo la kusaidia kupunguza shida ya maji iliyyopo. Utekelezaji wa mradi huo ulipangwa katika awamu mbili

ambapo awamu ya kwanza ilijikita katika ujenzi wa bwawa lenyewe kama chanzo cha maji na awamu ya pili ni ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kutoka kwenye bwawa kwenda kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa awamu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa bwawa lenyewe imekamilika ambapo bwawa hilo lina uwezo wa kuhifadhi maji lita 248,000,000 kwa mwaka. Hata hivyo, mnamo mwaka 2018 kulikuwepo na changamoto ya mvua kubwa iliyopekelea kuharibika kwa sehemu ya utoro wa maji (*Spillway*) ambayo kwa sasa mkandarasi (*DDCA*) yupo eneo la kazi na anaendelea na marekebisho ambapo kabla ya msimu wa mvua za mwaka huu kazi hiyo itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa awamu ya pili inayohusu ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji kwa wananchi. Ili kutumiza azma hiyo, Serikali imengia mkataba na Mtaalam Mshauri, *BICO* kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kufanya usanifu wa miundombinu ya kusambaza maji. Hadi sasa Mtaalam Mshauri huyo amewasilisha taarifa ya awali ya usanifu wa miundombinu ya kusambaza maji katika vijiji vinne (4) vya Kata za Matwiga na Mitanila. Kukamilika kwa hatua ya usanifu kutawezesha Serikali kutenga na kupeleka fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambalaswa, uliza swali la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda niseme tu nimefarijika sana kuona kwamba Serikali inatambua kwamba Wilaya ya Chunya ina changamoto ya uhaba wa maji vijijini sababu ya uchache wa vyanzo vya maji. Kwa hiyo, tunapoomba miradi ya Chunya, Serikali iitikie haraka kupeleka miradi hiyo Wilayani Chunya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni alitembelea Wilaya ya Chunya na pale Chunya Mjini alikuta kuna changamoto ya usambazaji wa maji katika Mji wa Chunya. Mheshimiwa Rais aliamuru Wizara itoe fedha ya ziada ili kurekebisha usambazaji wa mabomba ambayo yalikuwa yameharibika na nashukuru Serikali imetoa hiyo fedha na sasa hivi usambazaji unaendelea. Je, usambazaji huu utaisha lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Mradi wa Maji wa Mji 26 nchini Tanzania, Chunya ni mojawapo ya miji hiyo 26. Je, mkandarasi atakuwa *site* lini kuweza kurekebisha maji mjini Chunya?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Chunya, Lupa pale, Mheshimiwa Mwambalaswa umekuwa mionganoni mwa Wabunge ambao wamekuwa wakifuatilia sana suala la maji katika majimbo yao. Sisi kama Wizara ya Maji hatutokuwa kikwazo na ndiyo maana tumewapa fedha zaidi ya shilingi milioni 372 kwa ajili ya usambazaji wa maji kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mbeya katika kuhakikisha wanakamilisha mradi ule. Nachotaka kumhakikishia, kazi kama tulivyopanga itakamilika na tunaiagiza Mamlaka ya Maji ya Mbeya kuhakikisha mradi ule unakamilika kwa wakati ili wananchi wake waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Maji kwa Miji 28, kwa kutambua changamoto ya maji maeneo mbalimbali, Mheshimiwa Rais ametupatia fedha zaidi ya dola milioni 500, ni fedha za mkopo, kwa ajili ya miji 28. Mhandisi Mshauri ameshapita *site* zote, sasa hivi tunasubiri kibali kwa ajili ya kumpata mkandarasi ambaye tutahakikisha tunampata kwa wakati ili aweze kutekeleza miradi hiyo. Nataka nimhakikishie ndani ya mwezi Oktoba mkandarasi atakuwa amekwishapatikana na utekelezaji utakuwa umeanza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula halafu Mheshimiwa Aida.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa ucheleweshaji wa ukamilishwaji wa miradi ya maji wakati mwengine imepelekea kuwa na matatizo makubwa hasa kwa watumiaji. Hii inaenda sambamba na mamlaka zinazosimamia maji kulazimika kuangalia utaratibu mpya wa kuongeza gharama za maji kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) na matokeo yake *bill* za maji zimekuwa zikipanda sana kila wakati. Hivi tunavyozungumza kuna upandishwaji wa *bill* ambao unatokana tu na upungufu wa miradi mingi inayoweza ikazalisha maji kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nataka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, nini mkakati madhubuti wa Serikali wa kuendelea kuwapunguzia wananchi mzigo wa kulipa *bill* kubwa kila wakati kutokana na miradi mingi kukwama pengine kutokana na mikataba ya kifedha iliyocheleweshwa ili fedha hiyo iweze kutoka na miradi hii iweze kukamilika kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Stanslaus Mabula, kiukweli ni Mbunge ambaye anayefanya kazi na anawatendea haki wananchi wake wa Nyamagana.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha miradi ya maji inakamilika kwa wakati, sisi Wizara ya Maji tumejipanga baadhi ya miradi mingi tutaitekeleza kutumia *Force Account* kwa maana ya wataalam wetu kuweza kutekeleza miradi ile ili iweze kukamilika na wananchi wapate huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la bei za maji, tulipata malalamiko kwa wananchi wa Mwanza na Mheshimiwa Waziri ametoa maagizo maalum kwa *EWURA* kuhakikisha zile bei zinapitiwa ili wananchi wa Mwanza na maeneo mengine waweze kupata bei ambazo zitakuwa rafiki na waweze kupata huduma hii kwa urahisi. Katika kuhakikisha tunaondoa changamoto hii ya *bill*, sisi kama Wizara ya Maji tumejipanga na agizo maalumu la Mheshimiwa Waziri ni kuhakikisha kwamba tufunga *pre-paid meter* katika kuhakikisha wananchi wanalipa kutokana na kile ambacho wamekitumia.

Mheshimiwa Spika, kingine naomba niwasisitize wananchi matumizi ya maji yasiyokuwa na ulazima yanababishi kuongezeka kwa bili za maji. Leo mvua inanyesha lakini mwananchi anatumia bomba kumwagilia maji maua, halpendezi na wala haifurahishi. Hii ni changamoto lakini naomba Waheshimiwa Wabunge tutoe elimu hii ili kuhakikisha kwamba wananchi wanatumia vizuri maji na wanapata nafuu kabisa katika matumizi haya ya maji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Serikali imekuwa ikitenga fedha kupeleka katika miradi mbalimbali ya maji. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Mfili ambao uko Wilaya ya Nkasi lakini mradi huo umeshindwa kabisa kumaliza changamoto ya maji. Napenda kujua, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kuweza kumaliza changamoto hizo ili kuendena na kauli ya kumtua mama ndoo kichwani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha tunatatua tatizo la maji vijiji, Bunge lako Tukufu limetenga zaidi ya shilingi bilioni 301. Pia, tumepata zaidi ya dola milioni 500 kwa ajili ya kutatua tatizo la maji zaidi ya miji 28. Vilevile tumepata fedha zaidi ya shilingi bilioni 25.9 kwa ajili ya kukarabati vituo (*Payment by Result- PbR*) katika kuhakikisha tunatatua tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo tutahakikisha tunafuatilia miradi yetu na mingine tutaifanya kwa kutumia wataalam wetu wa ndani ili kukamilisha kwa wakati na wananchi wapate huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Tunahamia Wizara ya Kilimo, sasa swali linaulizwa na Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela ambako zamani ndiyo Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya alikuwa huko.

Na. 66

#### **Mradi wa Umwagiliaji Kata ya Illemba**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga mradi wa umwagiliaji uliopo katika Kata ya Illemba ambao ulijengwa na wananchi na ukabomolewa na mvua msimu wa 2018/2019?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri Mgumba, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini juhudui zilizofanywa na wananchi kwa kujenga Mradi wa Umwagiliaji Ilemba ambao umekuwa ukibomolewa mara kwa mara na mvua za msimu na kurudisha nyuma jitihada za wananchi kujiletea maendeleo. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa mradi huo kwa wananchi wa Jimbo la Kwela, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itatuma wataalam kufanya tathmini ili kuona sababu zinazosababisha miundombinu kubomolewa na kutafuta njia za kuondoa tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itatafuta fedha na kuingiza katika mipango yake ya kibajeti baada ya taarifa ya tathmini ya wataalam hao kukamilika. Aidha, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ili kuandika maandiko mbalimbali ya kuomba fedha kutoka taasisi za fedha, wadau wa maendeleo na Benki za Maendeleo na Biashara kwa ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma kupitia utaratibu wa Jenga, Endesha na Kabidhi ili kuweza kupata fedha za kukamilisha ujenzi wa Mradi wa Ilemba na hivyo kuwanufaisha wananchi wa Kata ya Ilemba na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malocha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kabla sijaenda kwenye maswali, nami niungane na wewe kumpongeza Mheshimiwa Mzindakaya, nami ndio mrithi wake katika Jimbo, naomba wananchi waniunge mkono miaka 45 washuhudie maendeleo. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naenda kwenye swalii. Namshukuru sana kwa majibu yenye ufanisi aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, japo tatizo hili nimelisema hapa Bungeni mara nyingi sana, sasa ifike wakati Serikali iende kwenye utekelezaji iwasaidie wananchi hao ambao wanajisaidia wenyewe Serikali iwaunge mkono.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, namwomba sasa Mheshimiwa Waziri afike kwenye eneo hili ili aone wananchi hawa wanavyohangaika kujinasua na umasikini. Waswahili wanasema kuona kunaongeza huruma kuliko kuambiwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Malocha *Inshallah*, tunakuombea na wewe. Naibu Waziri, Mheshimiwa Omary Mgumba, majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha anataka kufahamu hatua za utekelezaji wa mradi huu umefikia wapi kwa sababu ameshasema mara nyingi. Kama nillivyojibu kwenye swali langu la msingi, ni kwamba mradi huu umeibuliwa na nguvu wananchi na Serikali hii inawaunga mkono wananchi na ndiyo maana tumeanza kwanza kuboresha mfumo wa utendaji kazi wa Tume yetu ya Taifa ya Umwagiliaji. Kuanzia sasa tumeanza kujipanga Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ipo katika ngazi ya Wilaya, Mkoa, Kanda na Taifa.

Mheshimiwa Spika la pili, nachukua nafasi hii kuwaelekeza wataalam wa Taifa ya Umwagiliaji kwenda kwenye mradi huu haraka iwezekanavyo kufanya tathmini hiyo ili tuweze kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anataka kufahamu ni lini nitaenda pale kuona? Baada ya Bunge hili nimwahidi Mheshimiwa Mbunge, kuanzia tarehe 22 mwezi wa Tisa, nitakwenda huko kwenye Mikoa ya Rukwa na Katavi kwa ajili ya kufuatilia miradi hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Malocha. Mheshimiwa Dkt. Sware nimekuona, uliza swali la nyongeza.

**MBUNGE FULANI:** Ni Mheshimiwa Paresso.

**SPIKA:** Hawa watu wawili wanafanana sana. Mheshimiwa Paresso tafadhalii, samahani. (*Kicheko*)

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Tukitaka kufanya mapinduzi ya kilimo, hakika kilimo cha umwagiliaji ndicho ambacho kinaweza kumsaidia mkulima wa Tanzania. Katika Bonde la Eyasi Wilayani Karatu, wananchi wale wanatumia kilimo cha umwagiliaji lakini hakuna miundombinu ya uhakika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inawejenjea miundombinu ya uhakika ili umwagiliaji wao uwe endelevu na kilimo chao kiweze kuwasaidia?

**SPIKA:** Mheshmiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hili tafadhalii kuhusu Eyasi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli bonde hili la Eyasi ambalo mimi mwenyewe nilifika, ni bonde muhimu sana kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na ni chanzo kikubwa cha uchumi kwa watu wa Tarafa ile hasa kwenye zao la vitunguu.

Mheshimiwa Spika, katika bonde hili mikakati tuliyokuwa nayo kama Serikali, kwanza kama nillivyosema ni kwamba hatuwezi kusubiri pesa za kibajeti miaka yote hii. Kwa hiyo, sasa hivi kupitia Sheria ile ya *PPP* tumekuja na mpango kabambe kwa ajili ya kushirikiana na sekta binafsi kuendeleza miundombinu hii kwa utaratibu ule niliosema kwenye jibu la msingi la jenga, endesha na kabidhi baada ya yule mdau anayeendesha ule mradi kurudisha gharama zake.

Mheshimiwa Spika, pili, kupitia Serikai ya Halmashauri, ukizingatia Halmashauri hii ya Karatu zaidi ya 33% mapato yake yanatoka kwenye bonde hili. Kwa hiyo, tukasema zaidi ya mapato hayo ya ndani 20% warudushe kuwekeza katika bonde lile ili liweze kurudisha maendeleo kwa wananchi.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee, bado tupo Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo. Uliiza swali lako Mheshimiwa Shangazi.

Na. 67

### **Mazao ya Kimkakati ya Biashara**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Kwanza ilikuwa na mazao ya kimkakati ya biashara kama Kahawa, Pamba, 9 Pareto na Katani ili kuwa chachu ya kukuza Viwanda:-

Je, Serikali ya Awamu ya Tano ina mkakati gani mahsusni wa kuanzisha uzalishaji wa mazao na kaulimbiu ya Tanzania ya Viwanda?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, karibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano ni mwendelezo wa Serikali za Awamu ya Kwanza, Pili, Tatu na Nne, ambapo Sekta ya Kilimo ya kama ilivyokuwa katika awamu zilizopita, imeendelea kuwa uti wa mgongo kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kutoka Serikali za awamu zilizopita hadi sasa vipaumbele vya mazao vimekuwa vikibadilika kulingana na mahitaji na watu na wakati. Aidha, mazao ya kibiashara yameendelea kuwa kipaumbele kwa Serikali za awamu zote. Hata hivyo, fursa za mazao mengine kulingana na mahitaji ya watu zimeendelea kupewa kipaumbele katika

kupanga mipango na mikakati ya Sekta ya Kilimo katika Serikali ya Awamu ya Tano. Ongezeko la watu limesababisha mazao ya chakula na mazao ya bustani (*horticulture*) kuendelea kuwa sehemu muhimu ya mazao ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuendeleza mipango ya Serikali za Awamu zilizopita, sera mpya ya kilimo ya mwaka 2019 inatarajia kutoa vipaumbele vya Sekta ya Kilimo katika maeneo makuu manne ambayo ni mazao ya mkakati ambayo ni Pamba, Katani, Chai, Korosho na Kahawa, kwa ajili ya malighafi za viwanda. Mazao ya *horticulture* yenye thamani kubwa (*high value commodities*), uzalishaji wa mbegu ili kuifanya Tanzania kuwa muuzaji wa mbegu nje (*major seed exporter*) na mazao ya chakula ambapo lengo ni kuzalisha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, aidha, takwimu zinaonesha kuwa kufikia mwaka 2050 mahitaji ya chakula duniani yataongezeka kwa zaidi ya asilimia 50 ya sasa na hivyo Tanzania inatarajia kutumia fursa ya kijirografia kuzalisha zaidi mazao ya chakula kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa mipango hiyo, utekelezaji wa programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo *ASDP-II* unatarajiwala kuwa chachu ya kukuza Sekta ya Kilimo hasa kwa kuzingatia maeneo manne ya vipaumbele ya programu hiyo ambayo ni usimamizi endelevu wa matumizi ya ardhi na maji, kuongeza tija na faida katika kilimo, upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani na kuiwezesha sekta katika uratibu, ufuatilaji na utathmini. Mkakati ni pamoja na mkakati wa shirkishi na sekta nyingine, hususan sekta za kibiashara na viwanda kwa kuwa sekta hizo haziwezi kukuwa endepo sekta hii ya kilimo hususan *agro-processing* haitatimiza wajibu wake ipasavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali lakini nina maswali

mawili ya nyongeza. Kwa bahati Mheshimiwa Naibu Waziri ameanza kwa kusema kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ni mwendelezo wa Serikali zilizopita.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, zao la kahawa linaelekeea kupotea kwa kasi kubwa sana na sababu kubwa inalolifanya zao hili hili lipotee ni mabadiliko ya tabianchi. Je, Serikali ina mkakati gani wa kufanya utafiti upya ili kuleta mbegu ambazo zitaendana na hali ya hewa ambayo ipo sasa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mazao haya yalikuwa ni mkakati kwa ajili ya malighafi za viwanda. Sasa nataka aniambie, tulikuwa na kiwanda cha *VOIL* pale Mwanza, Kiwanda cha Magunia Morogoro, Kiwanda cha Magunia Moshi, tulikuwa na Kiwanda cha Nyuzi Tabora. Hivi viwanda havipo ilhalilwananchi wanaendelea kuzalisha: Je, hizi malighafi wananchi wanazozalisha, zinakwenda katika viwanda vipi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**

Mheshimiwa Spika, suala la mabadiliko ya tabianchi ni *challenge* ambayo inaikabili nchi yetu na dunia kwa ujumla. Wizara ya Kilimo kupita taasisi yake ya *TAR*/sasa hivi tunafanya utafiti wa kuwa na mbegu sitakazokabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hii imeonekana katika korosho ambapo tumepunguza muda wa mpaka zao la korosho kuja kuzalisha matokeo. Kwa hiyo, tunafanya hivyo hivyo katika mazao yote ya kimkakati na hata mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utafiti huu unaendelea pamoja na *soil profiling* ili kuweza kujua kwamba eneo hili ambalo tunalima kahawa je, bado litawenza kuhimili zao la kahawa au ama tuweze kuwashauri wananchi jambo lingine? Sasa hivi Wizara kupitia taasisi yake ya *TAR*/inaendelea na utafiti katika vyuo mbalimbali lakini wakati huo huo tunafanya suala la *soil profiling*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto ya tabianchi, zao la kahawa linakabiliiana na changamoto nyingi ikiwepo mfumo wa uzalishaji na mfumo wa uuzaaji kupidia ushirika, Wizara inapitia mfumo mzima wa kuanzia uzalishaji mpaka uuzaaji wa mazao yote ili kuweza kuleta tija kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la viwanda ni ukweli usiofichika kwamba Taifa letu limepitia nyakati mbalimbali na viwanda vyetu vingi vimepitwa na teknolojia. Sasa hivi Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara tunafanya *mapping* na *ku-develop new strategy* ili *ku-attract investors* ili waje kuwekeza katika Sekta ya Viwanda ili waweze *ku-take off* mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Nyuzi Tabora na viwanda alivyovitaja Mheshimiwa Waziri vikiwemo viwanda vya pamba, sasa hivi vingi vimepitwa na teknolojia. Tunaposema tunafufua, sisi kama Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda tumekubaliana mkakati wetu siyo suala la kufufua tu ni *ku-attract* uwekezaji mpya utakaoendana na teknolojia ya sasa ili mazao ya kilimo yaweze kupata tija na kuweze kupata masoko ya uhakika. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nimekuona Mchungaji Innocent Bilakwate, uliza swali lako.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Zao la kahawa ni mionganini mwa mazao ya kimkakati, lakini zao hili bei yake imekuwa ikisuasua kila mwaka; na ukilinganisha uzalishaji wa zao hili kwa mkulima gharama zinakuwa kubwa:-

Nini mkakati wa Serikali ili kuweza kuongeza bei ya kahawa ili mkulima aweze kuendeleza zao hili? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**

Mheshimiwa Spika, kwanza mkakati wa Serikali ni kutambua gharama halisi za uzalishaji za wakulima. Wizara ya Kilimo chini ya Naibu Katibu wa Mkuu Prof. Tumbo, sasa hivi tumeanza *program* ya kuanza kufanya *evaluation* ya mazao yote kujua mkulima anatumia shilingi ngapi.

Mheshimia Spika, kuhusu zao la kahawa, kama nilivyosema wakati namjibu Mheshimiwa Shangazi, ni kweli linakumbana na changamoto nyingi. Changamoto ya bei ya ni matokeo ya mfumo ambao umekuwepo muda mrefu ambao umemnyonya mkulima. Sasa hivi tunatumia Benki ya *TADB* ambayo imeanza kuzipa fedha taasisi za ushirika zilizopo katika Mkoa wa Kagera ili waanze kuchukua mazao ya wakulima kwa bei maalum na wakati huo huo tukitafuta masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge watupe muda kama Wizara, mazao yote haya tutayabadilisha mfumo wake na kuruhusu sekta binafsi iwe *competitive* wakati huo huo tukipunguza gharama za uzalishaji kama Serikali ili mkulima awezi kupata faida.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Saed Kubenea, kwa niaba yake Mheshimiwa Mwambe.

Na. 68

**Viwanda vya Sukari Kuagiza Sukari Nje Nchi**

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MHE. SAED A. KUBNEA)**  
aliuliza:-

Ni ukweli kwamba bei ya bidhaa za Viwandani kwa kiwango kikubwa zinatokana na gharama za uzalishaji kama vile maji, umeme, nguvu kazi na kadhalika:-

Je, kitendo cha kutoa kibali kwa Viwanda vya Sukari kuagiza sukari kutoka nje, siyo kuua kabisa Kilimo cha zao la

miwa ambacho wakulima wanategemea kuuza kwenye viwanda vya ndani?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Kilimo tafadhalii, Mheshimiwa Mgumba.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Sukari imeakuwa ikifanya tathmini ya mahitaji ya sukari nchini kwa mwaka na kwa kuzingatia matumizi ya kawaida na matumizi ya viwandani. Aidha, tathmini hiyo hufanyika sambamba na kujua uwezo wa viwanda vya kuzalisha sukari hapa nchini ambapo nakisi kati ya uzalishaji na mahitaji ndio kiasi cha sukari inayohitajika kuagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya mahitaji ya sukari kwa miaka miwili iliyopita, yaani 2017/2018 na 2018/2019 ilibaini kuwepo na utengamano wa soko la ndani kwa bei na upatikanaji wa sukari nchini. Aidha, utengamano huo ni matokeo ya maamuzi ya Serikali ya kutumia mfumo wa kuwapa leseni wazalishaji wa ndani kuagiza sukari kutohana na mahitaji badala ya mfumo wa kutumia wafanyabiashara kuagiza sukari toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mfumo huo umeweza kudhibiti uingizaji wa sukari ya ziada nchini kwani wazalishaji huagiza kuliangana na kiasi kilichoainishwa kwenye leseni husika. Aidha, kabla ya utaratibu wa kuwapata vibali wenyе viwanda kuagiza sukari, nakisi ya sukari (*Gap Sugar*) ilikuwa ni zaidi ya tani 130,000 nchini, lakini baada ya utaratibu wa kuwapa wenyе viwanda kuagiza, upungufu umepungua hadi kufikia tani 38,000.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho uzalishaji wa miwa kwa wazalishaji wadogo umeongezeka kutoka tani 568,083 msimu wa 2017/2018 hadi tani 708,460 msimu wa 2018/2019. Ongezeko la uzalishaji wa miwa kwa wakulima madogo limekwenda sambamba na ongezeko la kipato cha mkulima ambapo mapato ghafi kwa wakulima wa Kilombero, kwa mfano wakulima wa Kilombero yamefikia thamani ya shilingi bilioni 68.7 msimu wa 2018/2019 kutoka shilingi bilioni 48.1 misimu wa 2017/2018.

Aidha, kutohana na ongezeko la uzalishaji wa miwa kwa wakulima wadogo, uzalishaji wa sukari nchini umeongezeka kwa asilimia 16.8 kutoka wastani wa tani 307,431.26 hadi tani 359,219.25 katika msimu wa 2018/2019 wa kilimo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu marefu sana Mheshimiwa Waziri, lakini kinagaubaga kabisa hajasema wazi ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha sukari pamoja na miwa ya wananchi inapata bei nzuri ukilinganisha na sukari inayoletwa toka nje?

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kufahamu kwa Mheshimiwa Waziri, ili kuweza kulinda viwanda vya ndani, anasema nini kuhusu sukari inayoingizwa nchini kwa bei nafuu kuliko sukari inayozalishwa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, utakumbuka mwaka 2018 Serikali ilichukua maamuzi mazuri kabisa ya kuamua kukusanya korosho zote kwa wakulima na baadaye kutangaza bei nzuri na kusema watawalipa wakulima wote. Hivi sasa kumekuwa na sintofahamu kubwa sana kwenye mikoa yote inayolima korosho Tanzania kwa sababu mpaka sasa hivi Serikali haijakamilisha malipo kama ambavyo iliahidi. Utakumbuka maelekezo ya Mheshimiwa Rais na maneno yake alisema kwamba Serikali imeshatenga pesa na sasa hivi pesa hizo zinatakiwa kulipwa kwa wakulima kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu, nataka nipate *commitment kutoka wa Serikali*, ni lini hasa watakamilisha malipo ya pesa za wakulima wa korosho wa Tanzania kwa sababu walisema pesa hizo wanazo? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya Maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwambe anasema katika majibu yetu hakuna mkakati. Angerudia kwenye swali lake la msingi, hilo halikuwa swali la msingi, sisi tumejibu majibu yetu kwa kuzingatia swali la msingi tuliloulizwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake hili la nyongeza la kwanza anasema kwamba sukari inatoka nchi na ina bei ndogo kuliko sukari inayozalishwa hapa nchi. Nini mkakati wa Serikali kulinda viwanda vya ndani? Kwanza ni kweli sukari yote inayotoka nje kule twa hapa nchini ina bei ndogo kuliko sukari yetu. Ni kwa sababu wenzetu gharama za uzalishaji zipo chini kuliko gharama za hapa ndani kwa sababu wenzetu wanakwenda mpaka kwenye *by product* nyingine kwa hiyo wanashusha gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, sisi ili kulinda viwanda vya ndani kama tulivyosema, hii Serikali ya Awamu ya Tano ni Serikali ya Viwanda na ndiyo maana mkakati wa kwanza tumewapa ile *gap sugar*, wenye viwanda vyenyewe ndio waagize sukari ile pungufu ili kuivilinda viwanda vya ndani viweze kuongeza uwezo wa kimtaji na kulinda masoko yako.

Mheshimiwa Spika, hili limetupa manufaa makubwa. Kwa mfano, kiwanda cha sukari cha mtibwa, kabla ya utaratibu huu, uwezo wake wa kuzalisha ni zaidi ya tani 60,000 lakini ulikuwa unazalisha tani 15,000 tu kwa mwaka. Baada ya utaratibu huu, mwaka 2018 kwa mara ya kwanza imefikia kuzalisha tani zaidi ya tani 32,000. Kwa hiyo, hayo ni mafanikio makubwa sana katika kulinda viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo swali lake la pili anataka kujua malipo ya watu wa korosho. Ni kweli tumesema Serikali fedha tunazo na kweli Serikali fedha tunazo. Ndiyo maana katika hili la utaratibu wa sukari, tulielekeza kampuni yetu au Taasisi ya Serikali ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kununua korosho zote kutoka kwa wakulima. Taasisi hii ilienda kukopa kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea ni kwamba ile *limit* ambayo walipangiwa kwamba wameshafikia ukomo ilikuwa lazima kwamba wauze korosho kwanza ili wapunguze lile *gap* waweze kuuza tena. Sasa tumeshauza korosho hizo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kabda ya msimu huu kuanza wakulima wote watakuwa wamelipwa fedha zao. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha twende kwenye matangazo mbalimbali na utambulisho wa wageni tulionao. Kwanza ninae mgeni katika jukaa la Spika kutoka Afrika Kusini anaitwa Jakobus Pritorius karibu sana ni mgeni wetu anatutembelea kutoka Afrika Kusini. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni kama ifuatavyo:-

Wageni 31 wa Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini, ni rafiki zake kutoka Mikoa mbalimbali nchini ambao alisoma nao St. Augustine *University of Tanzania* wakiongozwa na Ndugu Hawa Kunya. Hawa na wenzako ahsanteni sana. Hawa ndiyo ma-mate wa Mheshimiwa Waziri wakiwa kule St. Augustine enzi hizo. (*Makofii*)

Mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Viwanda na Biashara ambae ni Diwani wa Kata ya Kibondo Karagwe. Karibu sana, karibu sana Mheshimiwa Diwani.

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao

ni wapiga kura wake kutoka Pangani Mkoa wa Tanga, Ndugu Khadija Mwinyihaji, Ndugu Akida Bahorera na Ndugu Omar Ibrahim. Karibuni sana wale pale. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Bhagwanji Maganal Meisuria amba ni rafiki zake kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Profesa Bajarng Bali Lal Sri na Dkt. Denis O'connell. Ni hao hapo karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Fredy Mwakibete ambae ni Baba yake Mdogo kutoka Jijini Mbeya, Ndugu Godlove Mwamsojo. Karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 41 wa Mheshimiwa Mussa Ntimizi amba ni wanafunzi kutoka shule ya Sekondari Jitegemee Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwalimu wao Ndugu Elijah Mutabora, karibuni sana watoto wa Jitegemee karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 24 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi amba ni wanakikundi cha Mlalo *Group* kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Anuary Mlugu. Karibuni sana Wananchi wa Mlalo, karibuni sana Dodoma. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Esther Matiko ambae ni mdogo wake kutoka Jijini Mwanza, Ndugu Arafat Kisiri. Karibu sana Arafat. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Cecil Mwambe amba ni watoto wake, Beatrice, Agripina, Celia, Delyth na Nicole. Karibuni sana watoto wa Mheshimiwa Mwambe. Hawa watano ni wale amba ana taarifa zao. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji amba ni Walimu wa Mazoezi wa Kikundi cha Kitambi Noma *Fitness Club* cha

Visiwani Zanzibar, Bimkubwa Siyah na Farida Mohamed. Karibuni sana. Hao ndiyo Wanakitambi noma hao. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, wageni walipo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 100 na walimu 10 kutoka shule ya sekondari ya Adili ya Jijini Arusha. Adili Arusha, karibu sana mmependeza kweli watoto wa Adili, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni watatu kutoka Kanisa la Tanzania *Assemblies of God* la Mkonze. Wale wa Mkonze karibuni sana, ahsante sana na Mwalimu Yohana Leguna kutoka Jijini Dar es Salaam. Ahsante sana Yohana. (*Makof*)

Bunge *Sports Club* siku ya JUmamosi tarehe 07/09/2019 walifanya Mechi ya mpira wa miguu, Bunge *Sports Club* walitoka sare na Gymkhana *Sports* bao mbili kwa mbili. Jana kulikuwa na Bonanza kwa michezo ya mpira wa miguu, Bunge *Sports Club* 2-Moshi *Veteran* 2, Bunge *Sports Club* 2 na Morogoro *Veteran* 3, kwenye michezo wa mpira wa Pete, Bunge *Queens* walipata 24 na Morogoro *Veteran* 18.

Ningependa kuwapongeza sana timu yetu ya Bunge *Sports Club* pia Bunge letu linaipongeza sana Taifa *Stars* kwa ushindi ambao tumeupata jana dhidi ya Burundi, tunawaombea vijana wetu waendelee kwa ari kubwa zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani, Mratibu wa timu ya *Basketball* ya Bunge *Sports Club* anawaomba wachezaji wa timu hiyo waendelee na mazoezi na pia anawatangazia wachezaji wote wa michezo huo kuwa mazoezi hayo yanafanyika katika viwanja vya CBE. *Basketball* CBE, Mratibu na Mwalimu wenu Ramo Makani anawaomba muendelee na mazoezi pale CBE. Mama Margaret Sitta anawaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote kutakuwa na semina leo Saa 7:00 Mchana katika Ukumbi wa Msekwa.

Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo

anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo ya Sheria Ndogo leo baadae, baada ya kuahirisha shughuli hizi za asubuhi kuanzia Saa Tano na kuendelea kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo katika Ukumbi Namba Tisa Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yameisha, Mheshimiwa Mlinga au nani amesimama? Mheshimiwa Mlinga.

### **MAELEZO BINAFSI YA MHE. GOODLUCK A. MLINGA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa ruhusa yako naomba kutoa neno kidogo.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 23 Agosti, 2019, Ndege yetu ya *ATCL* aina ya *Airbus A220-300* ilikamatwa huko South Africa kwa amri ya Mahakama ya Jimbo la Gauteng. Sharti la kuachiwa kwa ndege hiyo ilikuwa Serikali kumlipa Ndugu Hermanus Steyn USD milioni 30 ambayo ni sawa na zaidi ya bilioni 70 za Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, wasiojua bilioni 70, shilingi bilioni 70 tungejenga vituo zaidi ya 150 vya afya, hospitali zaidi ya 40 za Wilaya, *ambulance* zaidi ya 500 hii naamini hata vituo vya *private* wangepata hizo *ambulance*, viwanda vidogo vidogo na vya kati zaidi ya 3,000 ambavyo ukigawanya kila Mkoa unapata viwanda 96, kila Wilaya zaidi ya viwanda 10 ina maana hata mimi Ulanga ningepata viwanda 10, barabara kilometra zaidi ya 70 za lami na mimi Ulanga ningepata.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilituma jopo la Mawakili kwenda kupambana kisheria likiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Daniel Ndumbaro. Wasiomjua Mheshimiwa Ndumbaro mwaka 1999 na mwaka 2000 aliwahi kumtetea Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe asifukuzwe Chuo na akashindwa kesi hiyo anaendelea na Chuo mpaka leo hii ana *degree*. Pia Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro aliwahi kumtetea Katibu Mkuu wa CHADEMA sasa hivi Dkt. Mashinji asifukuzwe Chuo mpaka leo hi ni Daktari na anatusumbua. Jopo na Mawakili hao

alikuwepo Mheshimiwa Dkt. Ally Possi, Dkt. Arnold Gasesa, Ndugu Vincent Tango, Ndugu Gabriel Malata, Ndugu Job Mrema, Ndugu Charles na jopo la Wanasheria hawa likiwa *controlled kwa remote* na Mwanasheria Mkuu wetu mahiri wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kuna watu walibea na kibaya zaidi wengine ni viongozi katika nchi yetu na wengine ni Wawakilishi wa Wananchi walibea huo mchakato walisema Wanasheria wasio na vigezo walikwenda huko South Afrika. Tarehe 4 Septemba, 2019 Mahakama Kuu *South Africa* ya Jimbo la Gauteng ilitoa amri ya kuachiwa Ndege bila sharti lolote, bila kulipa hata senti 10 na Mahakama ikaamuru tulipwe gharama za kesi na upotevu wa pesa ambayo tulitakiwa tupate katika biashara hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Septemba, 2019 Saa 02:30 Usiku, Ndege yetu aina ya *Airbus* ilitua katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere. Kwa namna hiyo naomba Bunge lako Tukufu kutoa neno kwa Mawakili wetu hawa ikiwezekana waletwe Bungeni na kupewa heshima yao wanayostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mlinga umeongea jambo la maana sana, kwa kweli Watanzania wote nasi Wawakilishi wa Wananchi tunatoa salamu kubwa za shukrani kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa juhudhi hiso kubwa ambazo zilifanywa na Serikali yetu kuhakikisha chombo chetu hiki kinarudi hapa nchini kikiwa salama kabisa. Tunawapongeza sana Mawakili hawa waliofanyakazi hiyo nzuri sana tunazidi kuwapa moyo.

Waheshimiwa Wabunge, nilimwona Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro hapa?

**MBUNGE FULANI:** Yupo!

**SPIKA:** Naomba usimame angalau tukupongeza.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro ahsante sana na kwa niaba ya wenzako tunakupongeza sana, nasi tungeshangaa kama ungeshindwa kurudi na hiyo Ndege maana yake ye ye mwenyewe Mzulu na Dada yake Jenista wote asili yao ni huko, kwa hiyo tunashukuru sana kwa kurudi na chombo hiki. Tunakushuru sana Mheshimiwa Mlinga kutukumbusha jambo hilo na kama kuna cha ziada tutaongea katika vikao vyetu kuona nini zaidi cha kufanya, tutashauriana. (*Makofi na Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyokuwa mnafahamu tulikuwa na Mkutano wa Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Afrika (*CPA*) ambapo sisi ndiyo Sekretarieti yake tulikuwa tukiufanya Zanzibar wiki iliyopita. Mkutano huu umemalizika salama na ulikuwa na mahudhurio makubwa sana kutoka Mabunge yote Afrika. Mnapewa salamu nyingi sana na viongozi wa Mabunge haya yote ambayo wamehudhuria Mkutano ule Zanzibar, kwa kweli mahudhurio yake yalikuwa na mafuriko makubwa kabisa, haijapata kutokea mahudhurio makubwa kiasi hicho. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, katika makubaliano yetu kwenye Mkutano huo mojawapo ilikuwa ni kuyahimiza Mabunge ya Afrika ya Jumuiya ya Madola kuendelea kupunguza kadri iwezekanavyo matumizi ya karatasi ili kuhifadhi mazingira kwenda katika utaratibu wa *e-Parliament* ambao nasi tumeanza kidogo na tutaendelea katika Bunge lijalo tutaendelea sana na hata kuanzia sasa baadhi hata ya matangazo haya yanatuchukulia muda itabidi yaende kwenye mtandao huko kwa wanaohusika ili kurahisisha shughuli zetu zilizo nyingi na *document* nyingi sana tutakuwa tunawatumia katika taratibu za kimtandao na tutazidi kuelimishana namna bora zaidi ya kufanya jambo hilo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia katika Mkutano huo, tuliani dika andiko la pamoja kama tamko la Wabunge wa Afrika kulaani mauaji yanayoendelea Afrika Kusini yanayoitwa *Xenophobia* kwa niaba yenu. Palikuwa na mjadala mkali sana na Wabunge wenzetu wa kutoka Afrika Kusini walikuwa na uwakilishi tu mkubwa pale lakini kwa kweli lilijadiliwa kwa undani na tulionesha hisia na hasira zetu kwa jambo hili la ukatili dhidi ya binadamu ambalo limekuwa likiendelea mara kwa mara kule Afrika Kusini na andiko letu hilo tutawatumia pia katika njia za mtandao mpate katika nakala zenu muweze kuona ni kitu gani ambacho tulikiongea kwa Viongozi wa Nchi ya Afrika Kusini kuwaomba sana wajitahidi basi kuwalinda raia wa kigeni wanaouawa kule Afrika ya Kusini. Kilicho cha aibu kuliko yote ni kwamba hakuna Mzungu anayeuawa, wala Muhindi, wala Mchima, wala nani, wanaouawa ni Waafrika yaani Waafrika kwa Waafrika wanauawa kikatili sana, kwa hiyo tumetoa ujumbe huo kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo sasa Katibu naomba tuendelee.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH-KATIBU MEZANI**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Azimio la Kuridhia Mapendekazo ya Ubudilishaji Hadhi  
Sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Selous kuwa  
Hifadhi ya Taifa ya Nyerere**

**SPIKA:** Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla ili aweze kuwasilisha Azimio hili. Mheshimiwa Waziri karibu sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa jukumu la kusimamia rasilimali za wanyamapor, misitu, malikale na uendelezaji wa utalii. Usimamizi wa maeneo ya hifadhi za wanyamapor unajumisha hifadhi za Taifa 19, mapori ya akiba 23, mapori tengefu 42, Jumuiya za hifadhi za wanyamaopori 22 zilizosajiliwa na 16 ambazo zipo katika hatua mbalimbali za usajili. Aidha, tofauti ya msingi ya maeneo ya hifahi za wanyamapor ni aina ya matumizi yanayoruhusiwa kisheria katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, mnano Julai 26, 2019 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa anaweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme katika Bonde la Mto Rufiji (*The Rufiji Hydropower Project*) alitoa maelekezo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba sehemu ya Pori la Akiba la Selous ipandishwe hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo na maombi yaliyordhiwa na Mheshimiwa Rais, sehemu ya Pori la Akiba la Selous lenye ukubwa wa kilometra za mraba 30,893 kati ya 50,000 kilometra za mraba za pori hilo lilioanzishwa kwa tangazo la Serikali Namba 275 la mwaka 1974...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane tafadhali. Waheshimiwa Wabunge nitawataja kwa majina sasa. Waheshimiwa mna kikao ambacho siyo halali hapo naomba mnaomgeuka Spika tuangalie mbele na wengine wote nawaombeni tuwe na usikivu tumsikilize Mheshimiwa Waziri anachowasilisha. Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuzingatia maelekezo na maombi yaliyordhiwa na Mheshimiwa Rais, sehemu ya Pori la Akiba la Selous lenye ukubwa wa kilometra za mraba 30,893 katika ya kilometra za mraba kilomita za mraba 50,000 za pori hilo lilioanzishwa kwa tangazo la Serikali Namba 275 la mwaka 1974 inapendekezwa kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza maelekezo na ridhaa ya Mheshimiwa Rais ya kupandisha hadhi pori tajwa kuwa Hifadhi ya Taifa, Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 282 katika Kifungu cha Tatu na cha Nne inaelekeza utaratibu wa kuzingatia kama ifuatavyo na ninaomba kunukuu:-

*Section 3 inasema: "The President may with the consent of the National Assembly by proclamation published in the Gazette declare any area of land to be a National Park for the purposes of this Act."*

Mheshimiwa Spika, section 4 inasema; "*notwithstanding anything contained in the interpretation of laws Act no proclamation made under the provisions of section 3 of this Act shall be amended, varied or revoked except under the authority of an Act of Parliament provided that the president may with the consent of The National Assembly by proclamation publishing the gazette, alter the boundaries of any area declared to be a national park under the provisions of section 3*" mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maagizo ya Mheshimiwa Rais, Wizara inapendekeza sehemu ya pori la akiba Selous lenye kilometra za mraba 30,893 itangazwe kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere. Aidha, utekelezaji wa mapendekezo haya kwa wakati kutawezesha kuinua Pato la Taifa kutokana na ongezeko la idadi ya watalii, kuweshesha jamii kunufaika na fursa za utalii, kuimarisha uhifadhi, kutun za vyanzo vya maji, kuhifadhi mazalia ya samaki na chemchem ya maji moto ambayo ni vivutio vya utalii na utamaduni.

Mheshimiwa Spika, ninaomba katika hatua hii kuwasilisha hoja ya kubadilisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba Selous lenye ukubwa wa kilometra za mraba 30,893 kati ya 50,000 kwa Bunge lako tukufu ili liridhie sehemu ya pori hilo iwe hifadi ya Taifa Nyerere.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana.

Katibu, hebu njoo!

Nakuomba uendelee Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

KWA KUWA Sera ya Wanyamapori ni kudumisha uhifadhi endelevu kwa kuanzisha na kuboresha maeneo wakilishi yaliyohifadhiwa na kulinda bayoanuai katika mtandao wa hifadhi za Taifa, mapori ya akiba na mapori tengefu na kwa kuwa Sera ya Utalii ni kukuza uchumi na maisha ya wananchi hasa katika kupunguza umaskini kwa njia ya kuhimiza maendeleo ya utalii endelevu unaokubalika kiutamaduni na kijamii na unaojali mazingira na wenye faida kiuchumi.

NA KWA KUWA Pori la Akiba la Selous lilianzishwa kwa tangazo la Serikali Namba 275 la Mwaka 1974 ambapo imekusudiwa tangazo hilo lifutwe ili kubadilisha sehemu ya pori hilo kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

NA KWA KUWA Kifungu cha 3 che Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 kinampa Rais kwa idhini ya Bunge na kwa tangazo la Rais litakalochapishwa katika gazeti la Serikali mamlaka ya kutangaza eneo la ardhi kuwa Hifadhi ya Taifa kwa madhumuni ya sheria hiyo.

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha tatu cha Sheria ya Hifadhi ya Taifa Sura 282 ili kuanzisha Hifadhi ya Taifa ni sharti kupata ridhaa ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

NA KWA KUWA kwa kubadilisha hadhi ya uhifadhi wa sehemu ya Pori la Akiba Selous yenye ukubwa wa kilometra za mraba 30,893 kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere kutaimarisha uhifadhi wa bayoanuai hususan za

wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na hivyo kuongeza utalii wa ndani kukuza uchumi wa jamii inayozunguka hifadhi, utafiti na kutoa elimu ya vitendo kwa wanafunzi na wananchi watakaotembelea hifadhi hiyo.

NA KWA KUWA kwa kuridhia Azimio hili, Taifa litapata manufaa yafuatayo:-

(a) Kuimarisha uhifadhi wa maliasili hususan wanyamapori, mimea na mazalia na makuzio ya samaki na viumbe wengine kwenye maji;

(b) Kuongeza Pato la Taifa kwa msingi kuwa unadilishaji hadhi wa sehemu ya pori hilo utasababisha hifadhi hiyo kuwa kivutio cha utalii.

HIVYO BASI kwa kuzingatia manufaa ya utangazaji wa hifadhi tajwa ya Taifa, ninaomba sasa Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Sita na kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282, iridhie Azimio la Ubadilishaji hadhi sehemu ya pori la akiba la Selous yenyeye ukubwa wa kilometra za mraba 30,893 kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere hivyo mipaka ya hifadhi ya Taifa Nyerere itasomeka kama inavyoainishwa katika kiambatisho cha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Dkt. Hamis Kigwangalla. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunawashukuru sana, ahsanteni sana.

Sasa kwa hatua hii nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Utalii. Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kemilembe karibu sana.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(6)(b) cha Nyongeza ya

Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la kubadilisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa kueleza chimbuko, manufaa na maoni ya Kamati kuhusu uamuzi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 26 Julai, 2019, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa mto Rufiji (*Rufiji Hydro Power Project*) ndani ya eneo la Pori la Akiba la Selous alitoa maagizo yafuatayo:-

(i) Sehemu ya Kaskazini ya pori la Akiba la Selous ibadilishwe hadhi kuwa hifadhi ya Taifa ya Nyerere;

(ii) Sehemu kubwa ya pori la Akiba la Selous iwe Hifadhi ya Taifa ya Nyerere angalau kilometra za mraba 30,000;

(iii) Sehemu ndogo ya Kaskazini ya Pori la Akiba la Selous inayopakana na Wilaya ya Kisarawe imegwe kwa ajili ya matumizi ya wananchi yanayoendana na uhifadhi;

(iv) Bwawa la kufua umeme Mto Rufiji litaitwa Bwawa la Nyerere na litaendelea kusimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na;

(v) Kuboresha ukusanyaji mapato yatokanayo na shughuli za kitalii katika maeneo ya hifadhi nchini.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uliamua kuileta hoja hiyo kwenye Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na masharti ya Kanuni ya 53(4) ya Kanuni za Bunge, tarehe 4 - 7 Septemba, 2019, Kamati ilifanyia kazi hoja hii muhimu iliyotokana na maagizo

ya Rais. Kutokana na kazi hiyo, sasa nawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni, ushauri, manufaa na uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya hoja hii. Imeelezwa umuhimu wa kiikolojia wa pori la Selous ambayo ni pamoja na uwepo wa , mito, misitu, vijito, maeneo oevu na vyanzo vya maji. Pia, pori la Selous lina miinuko na vilima mbalimbali vinavyopendezesha mandhari ya Pori hili. Uwepo wa aina mbalimbali za baioanuai ikijumuisha wanyamapori, ndege na mimea kulichangia kulifanya pori la Akiba la Selous kuwa mionganoni mwa maeneo yanayotambulika na Shirika la umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*) kama urithi wa dunia (*World Heritage Site*).

Mheshimiwa Spika, vile vile Pori la Selous linapitiwa na vijito na mito ambayo inatiririsha maji kwenye bwawa la kufua umeme la (*Stiegler's Gorge*) ambalo litakuwa kivutio muhimu cha utalii na ni mazalia ya samaki na chanzo cha maji kwa wanyamapori na baioanuai nyingine.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kuipandisha hadhi sehemu ya pori la Akiba la Selous ni mwendelezo wa jitihada za Serikali ambapo mwaka huu mwezi Februari iliyapandisha hadhi mapori ya akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika kuwa Hifadhi za Taifa za Burigi - Chato, Ibanda - Kyerwa na Rumanyika - Karagwe.

Mheshimiwa Spika, kupandisha hadhi sehemu ya p ori la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere siyo tu kutaimarisha ulinzi, kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hiyo bali pia ni kumuenzi na kuenzi jitihada za Hayati baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ambaye tunaweza kusema alikuwa mhifadhi namba moja wa Taifa hili. Aidha kupandisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kutaimarisha jitihada za Serikali za kulinda Maliasili zetu.

Mheshimiwa Spika, kupandishwa hadhi kwa sehemu ya pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutachangia sana kufungua fursa za utalii katika Kanda ya

Kusini na hivyo kukuza kipato cha wananchi wanaopakana na hifadhi hii kutokana na shughuli za utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kipekee Kamati inapenda kumpongeza sana kwa dhati Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake kwa jitihada zake za kulinda maliasili yetu na kuhakikisha inatumika kwa ajili ya kuwanufaisha watanzania. Ni vyema kila mtanzania akatambua jitihada hizi za Rais wetu mpendwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na kumuunga mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati. Uamuzi wa kupandisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutaimarisha ulinzi na kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii katika ukanda wa Kusini na kukuza pato la wananchi wa Kusini na Taifa kwa ujumla. Kamati inalishawishi Bunge lako tukufu kuipitisha hoja hii muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kuepusha uwezekano wa hifadhi mpya kukabiliwa na migogoro, Kamati inashauri Serikali kuhakiki mipaka husika kwa kuwashirikisha wananchi ili kuepuka kuwepo na migogoro ya mipaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na uamuzi makini wa Serikali kuipandisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na kwa kuzingatia jiografia ya Pori la Akiba la Selous na maeneo yanayopakana nayo ambapo sehemu kubwa inafaa kwa shughuli za uwindaji wa kitalii, na kwa kutilia maanani uwepo wa mradi wa kufua umeme ndani ya pori hili na kwa kuzingatia dhamira ya Serikali ya kumuenzi Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na kuongeza mapato yatokanayo na maeneo ya hifadhi, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa badala ya kuchukua kilomita za mraba 30,893 kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ilihali sehemu inayofaa kwa matumizi ya utalii wa picha ni kilomita za mraba 5,000 tu na kwa sababu eneo linalobaki la kilomita za mraba 25,893 halina mazingira rafiki kwa utalii wa picha na kwamba litaigharimu Serikali fedha

nyingi kulihifadhi na kuweka miundombinu rafiki kwa ajili ya utalii wa picha.

Mheshimiwa Spika, ili kulipa jina la Mwalimu Nyerere uzito unaostahili, Kamati inapendekeza kuwa kwa wakati ambaao Serikali itaona inafaa, eneo lote la Pori la Akiba la Selous na maeneo ya jirani kama Pori Tengefu la Kilombero na mengine yanayopakana na Selous pamoja na bwawa la kufua umeme vyote kwa pamoja vibadilishwe kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Mwalimu Nyerere (*Mwalimu Nyerere Conservation Area*) kama ambavyo ilivyo Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, faida ya uamuzi huu ni kwamba Serikali itakuwa na wigo mpana wa kupanga matumizi mseto ya ardhi kama vile utalii wa picha, uwindaji wa kitalii, uvuvi wa kitalii (*Sport fishing*) ambavyo vyote kwa pamoja vitachangia kukuza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kuliweka eneo hili chini ya Mamlaka moja, utaepusha mgongano wa kimenejiment kwani eneo lote litasimamiwa na Menejiment moja tofauti na pendekezo la sasa ambapo Serikali eneo la Pori la Akiba la Selous linakuwa chini ya Mamlaka mbili yaani kilomita za mraba 30,893 sawa na asilimia 62 zinakuwa chini ya *TANAPA* na sehemu iliyobakia yenye kilomita za mraba 18,971 sawa na asilimia 38 linakuwa chini ya *TAWA*. Aidha Bwawa la kufua umeme la Rufiji nalo linasimamiwa na Taasisi mbili yaani sehemu moja ya Bwawa la kufua umeme itakuwa chini ya *TAWA* na sehemu nyingine itakuwa chini ya *TANAPA*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hatua ya hivi karibuni ya Serikali kuyapandisha hadhi mapori ya akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika na kuanzisha Hifadhi za Taifa tatu mpya za Burigi - Chato, Ibanda - Kyerwa na Rumanyika - Karagwe, Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) linasimamia jumla ya hifadhi kumi na tisa. Kati ya hizo ni hifadhi tatu tu yaani Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro

zinazalisha zaidi kwa ajili ya kujidesha na kuzaidia hifadhi nyingine kumi na nne ambazo ni tegemezi. Hifadhi mbili yaani Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara na Hifadhi ya Taifa ya Arusha zinazalisha kiasi cha kutosheleza kujidesha zenyewe tu. Kwa kuanzisha Hifadhi mpya ya Nyerere, Shirika la Hifadhi za Taifa (*TANAPA*) sasa litakuwa na jumla ya hifadhi ishirini na hivyo kuwa na mzigo mkubwa ikilinganishwa na uwezo wake wa kuzihudumia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Kamati inaona utaratibu wa kuyachukua baadhi ya maeneo "potential" yaliyo chini ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (*TAWA*) ni kuipunguzia Mamlaka hiyo uwezo wa kukusanya mapato na hivyo kuifanya ishindwe kujidesha. Mfano katika mapendekezo ya kubadili hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, jumla ya vitalu vytaangukia katika eneo la Hifadhi ya Taifa na kubakisha vitalu kumi (10) tu chini ya *TAWA* hali ambayo kwa vyovyyote vile itaathiri mapato ya *TAWA* ambayo inategemea sana biashara ya uwindaji wa kitalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali iangalie uvezekano wa kuwa na Mamlaka moja nchini inayosimamia uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori kama ilivyo kwa nchi jirani za Kenya, Zambia, Zimbabwe na Afrika Kusini tofauti na Tanzania ambako wanyamapori wanasihamiwa na taasisi zaidi ya moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Kwa kipekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kuchambua Azimio hili na hatimaye kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili, Katibu wa Kamati

Ndugu Haika Mtui kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshmiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuunga mkono Azimio. (*Makofi*)

**AZIMIO LA KUBADILI SEHEMU YA PORI LA AKIBA LA  
SELOUS KUWA HIFADHI YA TAIFA YA NYERERE –  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(6)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Azimio la Bunge la kubadilisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa kueleza chimbuko, manufaa na maoni ya Kamati kuhusu uamuzi wa Serikali.

**2.0 CHIMBUKO LA AZIMIO**

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 26 Julai, 2019, Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi wa kufua umeme mto Rufiji (Rufiji Hydro Power Project-RHPP) ndani ya eneo la Pori la Akiba la Selous alitoa maagizo yafuatayo:-

- (i) Sehemu ya Kaskazini ya Pori la Akiba la Selous ibadilishwe hadhi kuwa hifadhi ya Taifa ya Nyerere;
- (ii) Sehemu kubwa ya Pori la Akiba la Selous iwe hifadhi ya Taifa ya Nyerere angalau kilometra za mraba 30,000;
- (iii) Sehemu ndogo ya Kaskazini ya Pori la Akiba la Selous inayopakana na Wilaya ya Kisarawe imegwe kwa ajili ya matumizi ya wananchi yanayoendana na uhifadhi;

(iv) Bwawa la kufua umeme Mto Rufiji litaitwa Bwawa la Nyerere na litaendelea kusimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii; na

(v) Kuboresha ukusanyaji mapato yatokanayo na shughuli za kitalii katika maeneo ya hifadhi nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Nafurahi kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uliamua kuileta hoja hiyo kwenye Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na masharti ya Kanuni ya 53(4) ya Kanuni za Bunge, tarehe 4-7 Septemba, 2019, Kamati ilifanyia kazi hoja hii muhimu iliyotokana na maagizo ya Rais. Kutokana na kazi hiyo, sasa nawasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maoni na ushauri kwa kuanza na manufaa ya uamuzi.

### **3.0 MANUFAA**

**Mheshimiwa Spika**, imeelezwa umuhimu wa kiikolojia wa Pori la Selous ambayo ni pamoja na uwepo wa , mito, misitu, vijito, maeneo oevu na vyanzo vya maji. Pia, Pori la Selous lina miinuko na vilima mbalimbali vinavyopendezesha mandhari ya Pori hili. Uwepo wa aina mbalimbali za baioanuai ikijumuisha wanyamapor, ndege na mimea kulichangia kulifanya Pori la Akiba la Selous kuwa miongoni mwa maeneo yanayotambulika na Shirika la umoja wa Mataifa la Elimu,Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kama urithi wa dunia yaani (*World Heritage Site*).Vile vile Pori la Selous linapitiwa na vijito na mito ambayo inatiririsha maji kwenye bwawa la kufua umeme la (*Stiglers Gorge*) ambalo litakuwa kivutio muhimu cha utalii na ni mazalia ya samaki na chanzo cha maji kwa wanyamapor na baioanuai nytingine.

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa Serikali wa kuipandisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous ni mwendelezo wa jithada za Serikali ambapo mwaka huu mwezi februari iliyapandisha

hadhi mapori ya akiba ya Biharumulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika kuwa Hifadhi za Taifa za Burigi-Chato, Ibanda-Kyerwa na Rumanyika-Karagwe. Kupandisha hadhi sehemu ya Pori la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere siyo tu kutaimarisha ulinzi, kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii na kukuza pato la wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hiyo bali pia ni kumuenzi na kuenzi jitihada za Hayati baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ambaye tunaweza kusema alikuwa mhifadhi namba moja wa Taifa hili. Aidha kupandisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kutaimarisha jitihada za Serikali za kulinda Maliasili zetu.

**Mheshimiwa Spika**, kupandishwa hadhi kwa sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutachangia sana kufungua fursa za utalii katika Kanda ya Kusini na hilyo kukuza kipato cha wananchi wanaopakana na hifadhi hii kutohana na shughuli za utalii.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee Kamati inapenda kumpongeza kwa dhati Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Serikali yake kwa jitihada zake za kulinda maliasili yetu na kuhakikisha kuwa inatumika kwa ajili ya kuwanufaisha watanzania. Ni vyema kila mtanzania akatambua jitihada hizi za Rais wetu mpewda Dr John Pombe Joseph Magufuli na kumuunga mkono.

#### **4.0 MAONI YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, uamuzi wa kupandisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutaimarisha ulinzi na kujenga mazingira bora kwa ajili ya kuendeleza utalii katika ukanda wa Kusini na kukuza pato la wananchi wa Kusini na Taifa kwa ujumla. Kamati inalishawishi Bunge lako tukufu kuitisha hoja hii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuepusha uwezekano wa hifadhi mpya kukabiliwa na migogoro, Kamati inashauri Serikali kuhakiki Mipaka husika kwa kuwashirikisha wananchi ili kuepuka kuwepo na migogoro ya mipaka.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uamuzi makini wa Serikali kuipandisha hadhi sehemu ya Pori la Akiba la Selous kuwa hifadhi ya Taifa ya Nyerere na kwa kuzingatia jiografia ya Pori la Akiba la Selous na maeneo yanayopakana nayo ambapo sehemu kubwa inafaa kwa shughuli za uwindaji wa kitalii, na kwa kutilia maanani uwepo wa mradi wa kufua umeme ndani ya pori hili, na kwa kuzingatia dhamira ya Serikali ya kumuenzi Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na kuongeza mapato yatokanayo na maeneo ya hifadhi, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa badala ya kuchukua kilomita za mraba 30,893 kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ilihali sehemu inayofaa kwa matumizi ya utalii wa picha ni kilomita za mraba 5,000 tu, na kwa sababu eneo linalobaki la kilomita za mraba 25,893 halina mazingira rafiki kwa utalii wa picha na kwamba litaigharimu Serikali fedha nydingi kulihifadhi na kuweka miundombinu rafiki kwa ajili ya utalii wa picha.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulipa jina la Mwalimu Nyerere uzito unaostahili, Kamati inapendekeza Eneo lote la Pori la Akiba la Selous na maeneo ya jirani kama Pori Tengefu la Kilombero na mengine yanayopakana na Selous pamoja na Bwawa la kufua umeme vyote kwa pamoja vibadilishwe kuwa Mamlaka ya hifadhi ya Mwalimu Nyerere( Mwalimu Nyerere Conservation Area) kama ilivyo kwa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

**Mheshimiwa Spika**, Faida ya uamuzi huu ni kwamba Serikali itakuwa na wigo mpana wa kupanga matumizi mseto ya ardhi kama vile utalii wa picha, uwindaji wa kitalii, uvuvi wa kitalii( Sport fishing) ambavyo vyote kwa pamoja vitachangia kukuza pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu huu wa kuliweka eneo hili chini ya Mamlaka moja, utaepusha mgongano wa kimenejiment kwani eneo lote litasimamiwa na Menejiment moja tofauti na pendekazo la sasa la Serikali ambapo eneo la Pori la Akiba la selous linakuwa chini ya Mamlaka mbili yaani kilomita za mraba 30,893 sawa na asilimia 62% zinakuwa chini ya TANAPA na sehemu iliyobakia yenye kilomita za

mraba 18,971 sawa na asilimia 38% linakuwa chini ya TAWA. Aidha Bwawa la kufua umeme la Rufiji nalo linasimamiwa na Taasisi mbili yaani sehemu moja ya Bwawa la kufua umeme itakuwa chini ya TAWA na sehemu nyingine itakuwa chini ya TANAPA.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hatua ya hivi karibuni ya Serikali kuyapandisha hadhi mapori ya Akiba ya Biharamulo, Burigi, Kimisi, Ibanda na Rumanyika na kuanzisha hifadhi za Taifa tatu mpya za Burigi-Chato, Ibanda-Kyerwa na Rumanyika- Karagwe, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) linasimamia jumla ya Hifadhi kumi na tisa. Kati ya hizo ni hifadhi tatu tu yaani Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro zinazalisha ziada kwa ajili ya kuijendesha na kuzisaidia hifadhi nyingine kumi na nne ambazo ni tegemezi. Hifadhi mbili yaani Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara na Hifadhi ya Taifa ya Arusha zinazalisha kiasi cha kutosheleza kuijendesha zenyewe tu.Kwa kuanzisha Hifadhi mpya ya Nyerere, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) sasa litakuwa na jumla ya hifadhi ishirini na hivyo kuwa na mzigo mkubwa ikilinganishwa na uwezo wake wa kuzihudumia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwengine Kamati inaona utaratibu wa kuyachukua baadhi ya maeneo "**potential**" yaliyo chini ya Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) ni kuipunguzia Mamlaka hiyo uwezo wa kukusanya mapato na hivyo kuifanya ishindwe kuijendesha. Mfano katika mapendekezo ya kubadili hadhi sehemu ya Pori la Akiba la selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, jumla ya vitalu vya uwindaji 37 vitaangukia katika eneo la Hifadhi ya Taifa na kubakisha vitalu kumi (10) tu chini ya TAWA hali ambayo kwa vyovyyote vile itaathiri mapato ya TAWA ambayo inategemea sana biashara ya uwindaji wa kitalii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na Mamlaka moja nchini inayosimamia uhifadhi wa raslimali za wanyamapori kama ilivyo kwa nchi jirani za Kenya, Zambia, Zimbabwe na Afrika

ya Kusini tofauti na Tanzania ambako wanyamapor  
wanasimamiwa na taasisi zaidi ya moja.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuwasilisha maoni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano waliooutoa wakati wa kuchambua Azimio hili na hatimaye kuwasilisha Maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg.Gerald Magili, Katibu wa Kamati Ndg Haika Mtui kwa kuratibu vema shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Kemilembe Julius Lwota,Mb  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**  
**ARDHI, MALIASILI NA UTALII**  
**9 Septemba, 2019**

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili Mheshimiwa Kemilembe Lwota, tunakushukuru sana. Sasa naomba nimuite Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Maliasili na Utalii ambaye atatoa maoni ya upinzani kuhusiana na Azimio lililopo mbele yetu. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, karibu.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni Maoni

ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusiana na Azimio la Bunge la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadiishaji wa hadhi sehemu ya Pori la Akiba Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere. Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6) (c)

Mheshimiwa Spika, kupandisha hadhi mapori tengefu na mapori ya akiba kuwa Hifadhi za Taifa ni jambo la kawaida na lenye afya katika maendeleo ya tasnia ya uhifadhi kwa ujumla wake. Hata hivyo, yapo mambo muhimu ambayo hayana budi kuzingatiwa wakati wa upandishaji hadhi mapori husika. Mambo hayo ni pamoja na uungwaji mkono hatua hiyo; faida au hasara inayoweza kupatikana kwa kufanya uamuzi huo, athari za kimazingira na kiuchumi zinazoweza kutokea kwa jamii inayozunguka eneo husika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ili mambo hayo niliyoyataja yawewe kuchambuliwa vizuri na kuwezesha kufikia uamuzi wenye tija, Serikali haina budi kuwashirikisha wadau mbalimbali watakaoathiriwa na umuzi huo ili ipate maoni ya kutosha yatakayoisaidia kufikia uamuzi mzuri utakaoteklezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Kuhusu Utekelezaji wa Maagizo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyyoatoa wakati wa uwekaji wa jiwe la Msingi la Ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme Mto Rufiji ya tarehe 26 Julai, 2019; Azimio hili ni matokeo ya maagizo ya Rais kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha kwamba inaandaa mchakato wa kubadili hadhi ya sehemu ya Kaskazini ya Pori la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kipindi cha muda tangu agizo hilo lilipotolewa tarehe 26 Julai, 2019 mpaka leo tarehe 9 Septemba, 2019 siku ambayo Bunge linapitisha Azimio ni takriban kipindi cha mwezi mmoja na nusu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina hakika kama kwa kipindi hiki kifupi namna hiyo, Serikali imeweza kukutana na wadau mbalimbali wa uhifadhi, mazingira, utalii, miundombinu na

kuchambua fursa na changamoto mbalimbali zinazoweza kutokea kutokana na uamuzi huo ili kuwa na tija na uendelevu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Azimio. Moja ya athari za Azimio hili ni kuendelea kuiongezea mzingo *TANAPA* na hivyo kuifanya ishindwe kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii ni kwa sababu zipo hifadhi nyingi ambazo hazina uwezo wa kuijendesha na kwa hiyo zinakuwa zinahudumiwa na *TANAPA* kwa kiasi kikubwa jambo ambalo linaidhoofisha *TANAPA* kimapato.

Mheshimiwa Spika, Abraham Lincoln, Rais wa 16 wa Marekani aliwahi kusema, naomba kunukuu: “*You cannot strengthen the weak by weakening the strong. You cannot help little men by tearing down big men. You cannot lift the wage earner by pulling down the wage payer. You cannot help the poor by destroying the rich*”. Mwisho wa kunukuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tafsiri isiyo rasmi ya maneno hayo ni kwamba: “Huwezi kumsaidia mtu dhaifu awe na nguvu kwa kumdhoothisha mwenye nguvu. Huwezi kuwasaidia watu wadogo kwa kuwaangusha chini watu wakubwa. Huwezi kumpandisha anayelipwa mshahara kwa kumshusha chini mlipaji wa mshahara. Huwezi kuwasaidia maskini kwa kuwaangamiza matajiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maneno haya ya Abraham Lincoln yana mantiki katika mahusiano yaliyopo katika ya *TANAPA* na hifadhi zilizopo chini yake pamoja na *TAWA*. Kinachofanyika sasa, ni kuibebesha *TANAPA* mzigo wa kuhudumia hifadhi badala ya kuziimarisha taasisi nyingine ili zifanye wajibu huo pia.

Mheshimiwa Spika, takwimu za *TANAPA* zinaonyesha kuwa kati ya hifadhi 18 zilizopo chini yake ni hifadhi 5 tu zinazojiedesha kwa faida na hivyo kuweza kuijendesha hifadhi nyingine zilizobaki. Hii inatokana na uwekezaji duni

unaofanywa na Serikali katika hifadhi zetu na hivyo kuzifanya kukosa ushindani na hifadhi nyingine katika nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuziimarisa taasisi na idara nyingine za uhifadhi kama vile *TAWA*, Mali Kale na nyinginezo ili kuipunguzia mzigo *TANAPA* kwa malengo ya kuiongezea ufanisi. Sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili imeandaa mpango gani wa kuipatia *TANAPA* motisha (*incentives*) kama vile kuipunguzia kodi, ushuru na tozo mbalimbali ili ipate unafuu na hivyo kuweza kuhudumia hifadhi zilizoko chini yake ambazo haziwezi kuijendesha.

Mheshimiwa Spika, athari nyingine ya Azimio hili, ni hatari ya nchi kukosa fedha za utekelezaji wa miradi ya uhifadhi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo Duniani. Inafahamika kwamba, Selous ni moja ya maeneo yaliyoainishwa na Umoja wa Mataifa kuwa Urithi wa Dunia. Kutokana na hali hiyo, Tanzania iliridhia Mkataba wa UNESCO kuhusu usimamizi wa maeneo ya Urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ni kwamba kupitia mkataba huo, ipo miradi mikubwa miwili inayotekelawa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo. Miradi hiyo ni Mradi wa Uhifadhi na Utekelezaji wa Mfumo wa Kutegemeana kwa Viumbe Hai wa Selous (*Selous Ecosystem Conservation and Development Project (SECAD)*). Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya Euro milioni 18 ikiwa ni fedha za msaada kutoka Serikali ya Ujerumani. Mradi wa pili ni wa Usimamizi wa Maliasili Himilivu kwa ajili ya Ukuaji wa Tasnia ya Utalii (*Resilient Natural Resources Management for Tourism Growth Project (REGROW)*) unaotekelawa kwa Dola za Kimarekani milioni 37.7 ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa vyovoyote vile, Washirika hawa wa Maendeleo walikubali kutoa fedha hizo kwa Pori la Akiba la Selous kwa ukubwa wake wote wa kilometa za mraba 50,000 na sio kwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere wala

kipande kingine kilichobakia baada ya Hifadhi ya Nyerere kumegwa kutoka katika pori hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza Bunge hili ni kwa kiasi gani mabadiliko haya ya ghafla ya kupandisha hadhi Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutaathiri utoaji wa fedha zilizokuwa zinatolewa na washirika wa maendeleo katika utekelezaji wa miradi tajwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kujua kama kuna makubaliano au mkataba wowote kati ya Serikali na Benki ya Dunia kama itaendelea kutoa fedha hizo za utekelezaji wa miradi hiyo baada ya kuitishwa kwa Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Azimio hili, mbali na kuwa na viashiria vya kuikosesha nchi fedha zinazotolewa na washirika wa maendeleo katika miradi tajwa, fedha ambazo zinalenga kukuza uhifadhi wa mazingira yetu wakiwemo wanyamapori ambao ni mojawapo ya vivutio vya utalii, litaiingiza nchi katika rekodi mbaya ya kutoheshimu mikataba na makubaliano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkataba wa UNESCO kuhusu Usimamizi na Utunzaji wa Maeneo ya Urithi wa Dunia, Tanzania ilitakiwa kutoa taarifa na kuomba kibali kwa UNESCO kuhusu uamuzi inaotaka kuchukua lakini Serikali haijafanya hivyo kwa hoja kwamba utaratibu huo hauzuii Serikali kuendelea na mpango wake.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuifahamisha Serikali kwamba suala la uhifadhi ni suala la kidunia (*trans-boundary issue*) na linahitaji nguvu na ushirikiano wa kimataifa. Mabadiliko ya tabia nchi tunayoyashuhudia leo yanatokana na athari za kimazingira kutokana na uhifadhi duni wa mazingira katika maeneo ya mbali au nchi nyingine. Hivyo, kusema kwamba hiyo mikataba ya kimataifa haizuii Serikali kuendelea na mipango yake ni hoja ambayo inaweza kuwa na madhara huko baadaye kutokana na kukosekana kwa utashi wa kimataifa

(international will) katika mambo tunayoyafanya bila kuzingatia diplomasia na mahusiano ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, athari nyingine ya Azimio hili ni kuporomoka kwa utalii katika Mbuga ya Selous ambayo imekuwa na umaaarufu mkubwa kama Pori la Akiba kubwa kuliko yote nchini, lenye utajiri wa wanyama wa kila aina, uoto mzuri wa asili ambaao haujaathiriwa na shughuli za binadamu (*undisturbed nature*) yote hayo yakiwa yanatokana na sifa ya kipekee ya Selous ya kuwa eneo oevu (*wetland*) inayowezesha wanyama na mimea kuishi na kustawi.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyyote vile, baada ya kumega eneo la kilomita za mraba 30,000 kuwa Hifadhi ya Nyerere na baada ya kuharibu mazingira ya asili ya Selous kupitia Mradi wa Stiegler's Gorge, Selous haiwezi tena kubaki na vivutio vilevile vilivyoipewapo hapo mwanzo vilivyoipa sifa ya kuwa urithi wa dunia. Kwa sababu hiyo, wale watalii walioifahamu Selous na kuvutiwa na upekee wake wa asili watapata tabu sana kuitembelea kutokana na mabadiliko yaliyofanyika, jambo ambalo linaweza kupunguza mapato yatokanayo na utalii wa picha katika eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lipo jambo lingine ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani ingependza kujua kabla ya Bunge kuridhia Azimio hili. Inavyojulikana, eneo kubwa la Selous limevunwa miti mingi kupisha ujenzi wa Mradi wa Stieglers Gorge. Miti hiyo ni sehemu ya rasilimali za nchi kwa kuwa magogo yaliyopatikana baada ya kukata miti yana thamani kubwa na yanaweza kuchangia mapato ya Serikali kupitia biashara ya moja kwa moja au tozo na ushuru mbalimbali kwa wafanyabiashara wa magogo kwa mazao yatokanayo na misitu.

Mheshimiwa Spika, tangu zoezi la ukataji miti lianze huko Selous, Kambi Rasmi ya Upinzani haijawahi kusikia chochote kuhusu idadi ya miti iliyokatwa wala fedha

iliyopatikana kutokana na thamani ya magogo yaliyovunwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tunauliza jambo hili, kwa kuwa wananchi wanaweza kupambwa na maneno mazuri ya ujenzi wa mradi wa umeme kumbe ndani ya mradi huo kuna mtu au kikundi cha watu kinachojinufaisha na uporaji wa rasilimali za misitu zilizopatikana kutokana na usafishaji wa eneo la mradi. Ili kuondokana na sintofahamu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili ni magogo mangapi yanatarajiwa kuvunwa kutokana na zoezi la usafishaji wa eneo la mradi wa umeme wa Stiegler' Gorge, yatakuwa na thamani ya shilingi ngapi na soko liko wapi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Ifahamike kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina mgogoro wowote na wala haipingi dhamira njema ya Serikali ya kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kwa kutumia jina lake katika vitu vyenye wasifu wa kitaifa kama vile hifadhi hii mpya inayoanzishwa. Hata hivyo, kwa muktadha wa Pori la Akiba la Selous, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona ingekuwa na mantiki zaidi kubadili hadhi ya Pori hilo kwa ujumla wake na sio kukata vipande vipande. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kama ambavyo wadau mbalimbali wanaona kwamba Pori lote la Akiba la Selous lipandishwe hadhi na kuitwa Mwalimu Nyerere *Conservation Area*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusema kwamba *conservation is about business and it's all about boosting our economy*. Uhifadhi ni biashara na biashara hiyo inatakiwa ilenge kujenga uchumi wetu. Kama uhifadhi tunaoufanya hauna mchango wowote katika uchumi basi uhifadhi huo hauna maana yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, ni lazima Serikali izingatie dhana ya matumizi endelevu ya hifadhi zetu ili ziweze kunufaisha kizazi cha sasa na cha baadaye. Huo ndio msingi wa *sustainable use of natural resources* kwamba tunahifadhi, tunavuna na kutumia rasilimali zilizopo kwa namna ambayo kizazi cha sasa kitanufaika bila kuathiri kizazi kijacho. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali izingatie kipengele hicho cha nchi kunufaika na hifadhi inayoanzishwa, si kwa kutegemea fedha za watalii peke yake, bali pia kufikiria kuvuna maliasili zilizopo katika hifadhi hiyo kwa namna ambayo ni endelevu kwa ajili ya usitawi wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU  
AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MAPENDEKEZO YA  
UBADILISHAJI HADHI SEHEMU YA PORI LA AKIBA SELOUS  
KUWA HIFADHI YA TAIFA YA NYERERE KAMA  
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c)*

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, kupandisha hadhi mapori tengefu na mapori ya akiba kuwa hifadhi za taifa ni jambo la kawaida na lenye afya katika maendeleo ya tasnia ya uhifadhi kwa ujumla wake. Hata hivyo, yapo mambo muhimu ambayo hayana budi kuzingatiwa wakati wa upandishaji hadhi mapori husika. Mambo hayo ni pamoja na uungwaji mkonowa hatua hiyo; faida au hasara inayoweza kupatikana kwa kufanya uamuzi huo, athari za kimazingira na kiuchumi zinazoweza kutokea kwa jamii inayozunguka eneo husika nk.
2. **Mheshimiwa Spika**, ili mambo hayo niliyoyataja yaweze kuchambuliwa vizuri na kuwezesha kufikia uamuzi wenye tija, Serikali haina budi kuwashirikisha wadau

mbalimbali watakaoathiriwa na umuzi huo ili ipate maoni ya kutosha yatakayoisaidia kufikia uamuzi mzuri utakaoteklezeka.

**3. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii, Kuhusu Utekelezaji wa Maagizo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa wakati wa uwekaji wa jiwe la Msingi la Ujenzi wa Mradi wa Kufua Umeme Mto Rufiji ya tarehe 26 Julai, 2019; azimio hili ni matokeo ya maagizo ya Rais kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha kwamba inaandaa mchakato wa kubadili hadhi ya sehemu ya kaskazini ya Pori la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

**4. Mheshimiwa Spika**, ukiangalia kipindi cha muda tangu agizo hilo lilitipotolewa tarehe 26 Julai, 2019 mpaka leo tarehe 9 Septemba, 2019 siku ambayo Bunge linapitisha azimio ni takriban kipindi cha mwezi mmoja na nusu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina hakika kama kwa kipindi kifupi namna hiyo, Serikali imeweza kukutana na wadau mbalimbali wa uhifadhi, mazingira, utalii, miundombinu na kuchambua fursa na changamoto mbalimbali zinazoweza kutokea kutokana na uamuzi huo ili kuwa na tija na uendelevu.

## **B. UCHAMBUZI WA AZIMIO**

**5. Mheshimiwa Spika**, moja ya athari za azimio hili ni kuendelea kuiongezea mzingo TANAPA na hivyo kuifanya ishindwe kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii ni kwa sababu zipo hifadhi nyingi ambazo hazina uwezo wa kuijiendesha na kwa hiyo zinakuwa zinahudumiwa na TANAPA kwa kiasi kikubwa jambo ambalo linaidhoofisha TANAPA kimapato.

**6. Mheshimiwa Spika**, Abraham Lincoln; Rais wa 16 wa Marekani aliwahi kusema; naomba kunukuu *"You cannot strengthen the weak by weakening the strong. You cannot help little men by tearing down big men. You cannot lift the*

*wage earner by pulling down the wage payer. You cannot help the poor by destroying the rich”* mwisho wa kunukuu.

7. **Mheshimiwa Spika**, tafsiri isiyo rasmi ya maneno hayo ni kwamba; Huwezi kumsaidia mtu dhaifu awe na nguvu kwa kumdhooifisha mwenye nguvu. Huwezi kuwasaidia watu wadogo kwa kuwaangusha chini watu wakubwa. Huwezi kumpandisha anayelipwa mshahara kwa kumshusha chini mlipaji wa mshahara. Na huwezi kuwasaidia maskini kwa kuwaangamiza matajiri.

8. **Mheshimiwa Spika**, maneno haya ya Abraham Lincoln yana mantiki katika mahusiano yaliyopo katika ya TANAPA na hifadhi zilizopo chini yake. Kinachofanyika sasa, ni kuibebesha TANAPA mzingo wa kuhudumia hifadhi badala ya kuziimarisha taasisi nyingine ili zifanye wajibu huo pia. Takwimu za TANAPA zinaonyesha kuwa katil ya hifadhi 16 zilizopo chini yake, ni hifadhi 5 tu zinazojendesha kwa faida na hivyo kuweza kuziendesha hifadhi nyingine 11 zilizobaki. Na hii inatokana na uwekezaji duni unaofanywa na Serikali katika hifadhi zetu na hivyo kuzifanya kukosa ushindani na hifadhi nyingine katika nchi jirani.

9. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuziimarisa taasisi na idara nyingine za uhifadhi kama vile TAWA, Mali Kale na nyinginezo ili kuipunguzia mzigo TANAPA kwa malengo ya kuiongezea ufanisi. Sambamba na hilo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili; imeandaa mpango gani wa kuipatia TANAPA motisha (incentives) kama vile kuipunguzia kodi, ushuru na tozo mbalimbali ili ipate unaafuu na hivyo kuweza kuhudumia hifadhi zilizoko chini yake ambazo haziwezhi kujijendesha.

10. **Mheshimiwa Spika**, athari nyingine ya azimio hili, ni hatari ya nchi kukosa fedha za utekelezaji wa miradi ya uhifadhi kutoka kwa Washirika wa Maendeleo Duniani.

11. **Mheshimiwa Spika**, inafahamika kwamba, Selous ni moja ya maeneo yaliyoainishwa na Umoja wa Mataifa kuwa

Urithi wa Dunia. Kutokana na hali hiyo, Tanzania iliridhia Mkataba wa UNESCO kuhusu usimamizi wa maeneo ya Urithi wa Dunia. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ni kwamba; kuititia mkataba huo, ipo miradi miwili mikubwa inayotekelawa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo. Miradi hiyo ni Mradi wa Uhifadhi na Uendelezaji wa Mfumo wa Kutegemeana kwa Viumbe Hai wa Selous ( Selous Ecosystem Conservation and Development Project (SECAD). Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya EURO milioni 18 ikiwa ni fedha za msaada kutoka Serikali ya Ujerumani.

**12. Mheshimiwa Spika**, mradi wa pili ni mradi wa Usimamizi wa Maliasili Himilivu kwa ajili ya Ukuaji wa tasnia ya Utalii (Resilient Natural Resources Management for Tourism Growth Project (REGROW) unaotekelawa kwa Dola za Kimarekani milioni 37.7 ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

**13. Mheshimiwa Spika**, Kwa vyovyyote vile washirika hawa wa Maendeleo walikubali kutoa fedha hizo kwa Pori la Akiba la Selou kwa ukubwa wake wote wa Kilometa za Mraba 50,000 na sio kwa hifadhi ya Taifa ya Nyerere wala Kipande kingine kilichobakia baada ya Hifadhi ya Nyerere kumegwa kutoka katika pori hilo.

**14. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza Bunge hili ni kwa kiasi gani mabadiliko haya ya ghafla kupandisha hadhi Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kutaathiri utoaji wa fedha zilizokuwa zinatolewa na washirika wa maendeleo katika utekelezaji wa miradi tajwa? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kujua kama kuna makubaliano au mkataba wowote kati ya Serikali na Benki ya Dunia kama itaendelea kutoa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo baada ya kuitishwa kwa azimio hili.

**15. Mheshimiwa Spika, Azimio hili**, mbali na kuwa na viashiria vya kuikosesha nchi fedha zinazotolewa na washirika wa maendeleo katika miradi tajwa; fedha

ambazo zinalenga kukuza uhifadhi wa mazingira yetu wakiwemo wanyamapori ambao ni mojawapo ya vivutio vya utalii; litaiingiza nchi katika rekodi mbaya ya kutoheshimu mikataba na makubaliano ya Kimataifa. Kwa mujibu wa Mkataba wa UNESCO kuhusu usimamizi na utunzaji wa maeneo ya Urithi wa Dunia; Tanzania ilitakiwa kutoa taarifa na kuomba kibali kwa UNESCO kuhusu uamuzi inaotaka kuchukua lakini Serikali hajafanya hivyo kwa hoja kwamba utaratibu huo hauzuii Serikali kuendelea na mpang wake.

**16. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuifahamisha Serikali kwamba suala la uhifadhi ni suala la kidunia (trans-boundary issue) na linahitaji nguvu na ushirikiano wa kimataifa. Mabadiliko ya tabia nchi tunayoyashuhudia leo yanatokana na athari za kimazingira kutokana na uhifadhi duni wa mazingira katika maeneo ya mbali au nchi nyingine. Hivyo, kusema kwamba hiyo mikataba ya kimataifa haizuii Serikali kuendelea na mipango yake ni hoja ambayo inaweza kuwa na madhara huko baadaye kutokana na kukosekama kwa utashi wa kimataifa (international will) katika mambo tunayoyafanya bila kuzingatia diplomasia na mahusiano ya Kimataifa.

**17. Mheshimiwa Spika**, athari nyingine ya azimio hili ni kuporomoka kwa utalii katika Mbuga ya Selou ambayo imekuwa na umaarufu mkubwa kama Pori la Akiba kubwa kuliko yote nchini, lenye utajiri wa wanyama wa kila aina, uoto mzuri wa asili ambao haujaathiriwa na shughuli za binadamu (undisturbed nature) yote hayo yakiwa yanatokana na sifa ya kipekee ya Selou ya kuwa eneo oevu wetland) inayowezesha wanyama na mimea kuishi na kustawi.

**18. Mheshimiwa Spika**, kwa vyovyote vile, baada ya kumega eneo la kilomita za mraba 30, 000 kuwa hifadhi ya Nyerere, na baada ya kuharibu mazingira ya asili ya Selou kuititia Mradi wa Stiegler's Gorge, Selous haiwezi tena kubaki na vivutio vile vile vilivyoipao hapo mwanzo vilivyoipa sifa ya kuwa urithi wa dunia. Kwa sababu hiyo,

wale watalii walioifahamu Selous na kuvutiwa na upekee wake wa asili watapata tabu sana kuitembelea kutokana na mabadiliko yaliyofanyika; jambo ambalo linaweza kupunguza mapato yatokanayo na utalii wa pitcha katika eneo hilo.

**19. Mheshimiwa Spika**, lipo jambo jingine ambalo Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa kujua kabla ya Bunge kuridhia azimio hili. Inavyojulikana, eneo kubwa la Selous limevunwa miti mingi kupisha ujenzi wa mradi wa Stiegler's Gorge. Miti hiyo ni sehemu ya rasilimali za nchi kwa kuwa magogo yaliyopatikana baada ya kukata miti yana thamani kubwa na yanaweza kuchangia mapato ya Serikali kupertia biashara ya moja kwa moja au tozo na ushuru mbalimbali kwa wafanyakishara ya magogo, mbao na mazao yatokanayo na misitu. Tangu zoezi la ukataji miti lianze huko Selous, Kambi Rasmi ya Upinzani haijawahi kusikia chochote kuhusu idadi ya miti iliyokatwa wala fedha iliyopatikana kutokana na thamani ya magogo yaliyovunwa.

**20. Mheshimiwa Spika**, tunauliza jambo hili, kwa kuwa wananchi wanaweza kupambwa na maneno mazuri ya ujenzi wa mradi wa umeme kumbe ndani ya mradi huo kuna mtu au kikundi cha watu kinachojinufaisha na uporaji wa rasilimali za misitu zilizopatikana kutokana na usafishaji wa endo la mradi.

**21. Mheshimiwa Spika**, ili kuondokana na sintofahamu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili ni magogo mangapi yanatarajiwa kuvunwa kutokana na zoezi la usafishaji wa eneo la mradi wa umeme wa Stiegler's Gorge, yatakuwa na thamani ya shilingi ngapi na soko liko wapi.

#### C. HITIMISHO

**22. Mheshimiwa Spika**, ifahamike kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina mgogoro wowote na wala haipindi dhamira njema ya Serikali ya kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kwa kutumia jina lake katika vitu vyenye wasifu wa kitaifa kama vile hifadhi hii mpya

inayoanzishwa. Hata hivyo, kwa muktadha wa Pori la Akiba la Selous, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona ingekuwa na mantiki zaidi kubadili hadhi ya Pori hilo kwa ujumla wake na sio kukata vipande vipande.

**23. Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekaze kama ambavyo wadau mbalimbali wanaona kwamba, Pori lote la Akiba la Selous lipandishwe hadhi na kuitwa "Nyerere Conservation Area"

**24. Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusema kwamba "**conservation is about business, and it's all about boosting our economy**" Uhifadhi ni biashara, na biashara hiyo inatakiwa ilenge kujenga uchumi wetu. Kama uhifadhi tunaoufanya hauna mchango wowote katika uchumi basi uhifadhi huo hauna maana yoyote. Kwa mantiki hiyo, ni lazima Serikali izingatia dhana ya matumizi endelevu ya hifadhi zetu ili ziweze kunufaisha kizazi cha sasa na cha baadaye. Huo ndio msingi wa "**Sustainable Use of Natural Resources**" kwamba; tunahifadhi, tunavuna na kutumia rasilimali zilizopo kwa namna ambayo kizazi cha sasa kitanufaika bila kuathiri kizazi kijacho.

**25. Kwa hiyo Msheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali izingatia kipengele hicho cha nchi kunufaika na hifadhi inayoanzishwa, si kwa kutegemea fedha za watalii peke yake, bali pia kufikiria kuvuna maliasili zilizopo katika hifadhi hiyo kwa namna ambayo ni endelevu kwa ajili ya usitawi wa uchumi wetu.

**26. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha,

Mch. Peter Simon Msigwa (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
KATIKA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

9 Septemba, 2019

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mch. Msigwa, Msemaji Wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Sasa tunaingia katika uchangiaji wa Azimio, Mheshimiwa Hamidu Bobali utaanza na atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Wabunge wenzangu wa Chama cha CUF, naomba niseme kwamba sisi tunaliunga mkono Azimio hili. Tunaliunga mkono sehemu hii ya Selous kuchukuliwa kufanya kuwa ni hifadhi na kiukweli yapo mafanikio ama faida ambazo zitaonekana hapo baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ni Mbunge ninayetoka Mkoa wa Lindi, naomba nieleze machache ambayo Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja anaweza akawa na majibu. Kwanza, ifahamike mbuga ya Selous inachukua asilimia 38 ya Mkao wa Lindi. Mkao wenyewe ukubwa wa *square kilometer* 67,000 asilimia 38, zaidi ya *square kilometer* 24,000 ni Msitu wa Hifadhi wa Selous.

Mheshimiwa Spika, jambo la kupandisha hadhi sisi kama Mkao wa Lindi utaathiri moja kwa moja, inawezekana athari zikawa za faida (*positive*) ama *negative*. Nataka nihoji mambo kadhaa, sasa hivi ukiwa unatembea unatoka Nangurukuru Kilwa unaelekea Liwale hasa muda wa asubuhi, ajabu sana utakutana na malori yanabeba magogo yanayotoka kwenye Selous, tena malori yenye hata *plate number* hayana, yaani yale malori ya zamani, yaliyochakaa na ni mengi. Mimi nimefanya ziara hivi karibuni nimekutana na malori mengi yanakata miti nikastaajabu hii ni kwa mujibu wa vibali ambavyo vimetolewa ama imekuwaje.

Mheshimiwa Spika, pia wafugaji sasa, ukitoka eneo linalopakana kati ya Kilwa na Liwale, maeneo ya Zinga unaelekea Liwale kumekuwa na uvamizi mkubwa wa

wafugaji, ng'ombe wako wengi, kule msituni kuna ng'ombe wengi na kuna ukataji hovyo wa miti katika eneo lile. Sasa tunakupandisha hadhi swali linakuja hawa wafugaji ambaao wamevamia kwa kiwango kikubwa, wafugaji wengi Mkoa wa Lindi wako Liwale na unapozungumza Selous Mkoa wa Lindi unazungumzia Wilaya za Liwale na Kilwa na Halmashauri ya Lindi Vijijini ya kwetu sisi, hawa wafugaji mtawapeleka wapi, ni wengi mno na wana mifugo mingi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Lindi ambayo ina eneo kubwa la Selous na nimeangalia ramani ya eneo ambalo linachukuliwa kupelekwa Selous, tuna vivutio vingi kabisa ambavyo kupandishwa hadhi kwa pori hili kunaweza kukaunganisha utalii wa Kusini *especially* utalii wa Lindi. Mfano, tunao mji mzuri wenye historia, Mji wa Kilwa Kisiwani ambaao ni kivutio kizuri kabisa cha watalii na inafanya vizuri sasa hivi ukiangalia ile *channel* yetu ya Tanzania Safari huwezi kuangalia siku mbili kama hujaona inaonyeshwa Kilwa Kisiwani. Nadhani upandishaji wa hadhi wa pori hili unaweza ukaunganisha sasa utalii ukaenda moja kwa moja kwenye Mji wa Kilwa Kisiwani na fukwe nzuri zilizopo katika Pwani ya Kusini maeneo ya Lindi mpaka Mtwara hasa eneo la Mikindani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia mimi nina hakika kwamba jambo hili ili liwe jema sana hizi fedha za *REGROW* ambazo zinataja *Southern Circuit* ya utalii ziguse na Mkoa wa Lindi, hazitugusi. Hili ni swali Mheshimiwa Waziri kwako. Fedha za *Southern Circuit* zinakwenda Mkoa wa Morogoro, Iringa na Njombe, ni fedha zilizosababishwa na Selous, sisi ambaao tunachangia kilometra za mraba 24,000 kwa nini fedha hizi hazitugusi? Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha ajibu na swali hili fedha za *REGROW* sisi watu wa Lindi tunazikosaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesema tunaunga mkono jambo hili lakini liendane na uboreshaji wa miundombinu ya barabara. Barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale zile kilometra 230 ni ya vumbi. Kwa hiyo, watalii watakwendaje ikiwa ile barabara haipitiki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mnaweza mkastaajabu, Lindi tumepakana na Mkoa wa Morogoro kule kwa Mheshimiwa Mlinga, watu wanatoka Liwale wanakwenda Mahenge wanatembea kwa miguu wanatumia zaidi ya siku 5, 6 na wanasindikizwa na wale askari wanyamapori. Naomba upandishaji wa hadhi wa msitu huu uendane na ujenzi wa miundombinu ili na sisi watu wa Lindi tuweze kunufaika na hifadhi ya Nyerere. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wenzangu wote na mimi tunaunga mkono Azimio hili. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere nilishakutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, kimsingi ukiangalia alipowakilisha Mwenyekiti wa Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani ni kama wamekubaliana. Rafiki yangu Mchungaji amezungumza mambo mengi lakini ametoa na majibu. Mchungaji anapoizungumzia *UNESCO* ni kama vile kuna kachombo fulani hivi ka nchi kanapodhibiti mambo fulani hivi ya nchi fulani. *UNESCO* imeanzishwa mwaka 1945 inaitwa *United Nation Education, Scientific and Cultural Organization*. Mwaka 2014, *UNESCO* ilikuja kwenye Pori la Selous kuweka tahaadhari ya Pori la Selous kwa ajili ya mauaji ya tembo. *UNESCO* ilikuja kuangalia mauaji ya tembo yanayofanyika kwenye Pori la Selous. *UNESCO* kazi yake ni kuangalia usalama wa maeneo maalum katika nchi mbalimbali kwa vizazi vilivyopo na vijavyo kama alivyosema Mheshimiwa Msigwa hapa *sustainable development*.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho *UNESCO* wanafanya kwa sasa ni kumpa kumzawadia Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kutunza mazingira ambayo sasa wameiondoa Selous kwenye hatari wameiweka kwenye usalama. Sasa leo nashangaa unaposema *UNESCO* kwamba itaondoa miradi, yaani umeitengenezea miradi

ambayo unaitunza kwa vizazi nya sasa na vijavyo halafu waondoe mradi, sijawahi kuona. Kwa hiyo, UNESCO ipo pale kuangalia usalama wa maisha ya maeneo mbalimbali kwa vizazi nya sasa na vinyavyokuja.

Mheshimiwa Spika, nafikiri wote waliota ripoti hapa, Kambi ya Upinzani waliposoma, Mwenyekiti wa Kamati alivyosoma wamefanya sawa. Mheshimiwa Msigwa amesema sasa kwa kuwa Pori la Akiba Selous lilikuwa linasaidia *TAWA* kwenye mapato na sasa limekwenda *TANAPA*, kwa hiyo, Serikali ifanye jitihada kwa sababu *TAWA* na *TANAPA* ni mali ya Serikali, hakuna nchi zinazojitegemea hapa, hakuna kusema *TAWA* ina hela zake na *TANAPA* ina hela zake, ni mali za Serikali. Kwa hiyo, sasa kwa sababu *TANAPA* inapungukiwa mapato mengine ya kusaidia maeneo mengine kwa hiyo Serikali isaidie *TAWA* kwa kuwapa hela za kuisaidia kwenye maeneo mengine. Tuna mapori ya akiba 23 yanatosha kuifanya *TAWA* ipate fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilichokiona hapa na ambacho kwa kweli tunatakiwa kukifanya ni kwamba katika Pori la Selous kuna wafanyakazi 700 wa *TAWA* na wafanyakazi wa *TAWA* na *TANAPA* wanalipwa tofauti. Wafanyakazi wa *TAWA* wanalipwa mshahara wa laki nne na zaidi wakati wafanyakazi wa *TANAPA* wanalipwa shilingi milioni moja na laki tano. Sasa inakuja hoja, wafanyakazi wa *TAWA* ambao wametunza hilo pori toka likiwa bovu, wameliwekea miundombinu, wengine wamezeeka wamebakiza miaka 3, 4 kustaafu, sasa leo kwa mujibu wa sheria zilizopo mtawaondoa wote waende *TAWA* halafu wataajiriwa wa *TANAPA* kufanya kazi ile.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge wafanyakazi 700 walio kwenye Pori la Selous wabaki pale pale na wenyewe wafaidi hizo hela za *TANAPA* ambazo zitawekwa mule ndani na wenyewe wapate hiyo mishahara. Naomba tusiwaondoe mule ndani ili mishahara itakayokuja iwakute mle ndani na wenyewe wafaidi. Wamefanya kazi kwa muda mrefu wa kutunza lile pori tusiwaondoe wakaenda kusononeka huko, ni kama vile umetengeneza kitu halafu wewe

unanyang'anywa. Kwa hiyo, niombe Serikali na niombe tulunge mkono ili wafanyakazi 700 wa Selous waliopo pale wabaki kwenye maeneo yao wapandishwe vyeo, wahamishwe waende *TANAPA* ili na wenyewe wapate kilichoko mule ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine kilichopo ni kwamba *TAWA* nayo imetumika sana kutengeneza yale maeneo, imeweka miundombinu na vitu vingi. Kwa hiyo, kama kuna uwezekano kama tulivyo sema wengine basi Serikali sasa kupitia *TANAPA* ione namna gani kwenye mapori ya akiba yaliyobaki kuimarisha namna ya kutengeneza kitega uchumi ambacho kitawasaidia kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli hakuna jipya, mambo yote yameenda vizuri. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii amehangaika sana na habari ya kusema wadau, habari ya kusema nani, lile ni pori la akiba, wadau walishasikilizwa muda mrefu na ni mali ya Serikali. Kwa hiyo, Serikali imefanya uhifadhi kwa kulitoa kwenye pori la akiba na kupeleka kwenye *national park*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi sioni kama kuna tatizo ambalo liko hapa. Mimi naipongeza Serikali, nampongeza Mheshimiwa Rais ametuvekeea ule mradi pale na watu wengine wajue jamani kuweka Pori la Akiba Selous kuwa hifadhi maana yake ni kama tunatunza kiota chetu, tuna mradi wa *Stiegler's Gorge* mkubwa, Mradi wa Nyerere ambao umeanzishwa pale, tunatakiwa tuuwekee mazingira mazuri na waliosema eneo lote liwe hifadhi mimi nakubaliananao ili eneo lile lilindwe vizuri ili tuweze kuutunza ule mradi wetu vizuri kwenye maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, lakini naona hoja hii imeisha, naomba niunge mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mchengerwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa dakika tano, tano.

**MHE. MOHAMED O. MCHENERWA:** Mheshimiwa Spika, kila Mtanzania atakubaliana nami kwamba Taifa hili kwa miaka mingi sana lilihitaji kuwa na Rais mwenye kufanya maamuzi, kutoa matamko ambayo kesho na kesho kutwa yatafanyiwa kazi na kuwa sheria. Kwa hiyo, sisi wananchi tunaotoka kwenye eneo la Pwani ya Kusini tunapendekeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa tamko la kuamua sasa eneo hili la Selous kuwa ni Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Spika, huu ni utaratibu mzuri kabisa wa kizalendo wa kuwaenzi wapigania uhuru akina Mwalimu Nyerere, lakini pia ninaamini huko tunakokwenda mbele katika eneo letu la Rufiji, basi kutapatikana eneo ambalo pengine tutaliita Bibi Titi Mohamed ambaye yeye alikuwa ni Mbunge wetu wa kwanza kule Rufiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi wa Pwani ya Kusini tunaamini kabisa kwamba kwa miaka mingi sana tulipuuzwa na hili lilitokana na mgawanyo hafifu wa pato la Taifa na ilisababisha kuwepo kwa umasikini wa hali ya juu, lakini Watanzania na wananchi wote wa Tanzania pamoja na dunia nzima inatambua uwepo wa utajiri mkubwa sana katika eneo la Pwani ya Kusini. Kwa hiyo, sisi wananchi wa Rufiji tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini lazima nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Maliasili na Utalii, Waziri wa Maliasili na Utalii anachapa kazi kweli kweli, kwa hiyo, sisi tunampongeza sana na maamuzi haya ni maamuzi sahihi, lakini tunatambua vipo vikwazo viwili pengine katika kuelekea uanzishwaji wa Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere yako mambo ambayo pengine ni lazima tuyazingiatie na tuyatekeleze sasa.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba miaka ya 2006 Serikali iliamua kuhamisha mifugo kutoka Hifadhi ya Bonde la Ihefu na kupeleka katika eneo la Kusini pamoja na Pwani kule Rufiji na kuendelea Kilwa na Mtwara. Tatizo la uwepo wa mifugo katika eneo la Hifadhi hii ya Mwalimu Nyerere litakuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa kukua kwa eneo hili la hifadhi.

Mheshimiwa Spika, tuiombe Wizara sasa kufanya maamuzi magumu, maamuzi sahihi. Taifa hili lina eneo kubwa sana, Tanzania hatupaswi kugombana kati ya wakulima na wafugaji, lakini pia hata wafugaji wanapaswa kuwepo katika maeneo yaliyoidhinishwa na Serikali. Tuiombe Serikali kufanya maamuzi ya makusudi kabisa kuondoa mifugo kwenye eneo hili la Hifadhi ya Mwalimu Nyerere kuanzia Rufiji katika Kata za Mkongo, Ikwiriri na kuendelea; maeneo haya ni maeneo yote ambayo tunayategemea sasa baada ya kuanzishwa kwa Hifadhi hii ya Mwalimu Nyerere. Uwepo wa mifugo katika eneo letu kutaathiri hata uanzishwaji au ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme pale, Bwawa la mwalimu Nyerere.

**SPIKA:** Ahsante sana. Ahsante sana dakika tano, Mheshimiwa Hawa Ghasia dakika tano pia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika azimio hili la kupandisha hadhi Pori la Selous kuwa Hifadhi ya Taifa. Niipongeze Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Rais na nimpongeze Waziri pamoja na Kamati ya Maliasili kwa kuridhia pori hili kuwa hifadhi.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sana ambapo hili ombi lilikuwa linaenda linarudi, linaenda linarudi kwamba, Selous iwe hifadhi na sio Pori la Akiba. Kwa kuifanya kuwa hifadhi tutakuwa tunaiihifadhi zaidi Selous kuliko ambavyo sasa hivi liko pori ambalo uwindaji wa kitalii ndani yake mle unaruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nipingane na Mheshimiwa Msigwa ambaye anasema hatujatoa taarifa *UNESCO* kwa sababu eti kuhifadhi tunahitaji ushirikiano wa kimataifa. Ndio tunahitaji ushirikiano wa kimataifa, lakini tunachokifanya sisi ni kupandisha hadhi, ina maana tunaendeleza uhifadhi zaidi, daraja kama ni uhifadhi tunaenda daraja la juu zaidi kuliko tulipo, tunachokifanya ndicho *UNESCO* inachokitaka. Tungeomba kibali cha *UNESCO* kama tungekuwa tunashusha hadhi kutoka

kwenye pori na kuwa eneo la kawaida tu ambalo mtu yejote anaweza akafanya kitu chochote.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuunga mkono hili wazo na niiombe Wizara ya Maliasili na Utalii suala hili la kupandisha hadhi Pori la Selous kuwa hifadhi liende sambamba na kutangaza vivutio vingine vilivyopo Kusini mwa Tanzania ikiwemo *beach* nzuri za Msimbati ambazo unaweza ukaenda na gari lako na ukaendesha kama ambavyo unaweza ukaendesha kwenye barabara yoyote ya lami kwa *speed* yoyote unayoitaka.

Mheshimiwa Spika, pwani hizi ziko chache sana duniani na kwa Afrika nadhani ni moja tu ambayo inapatikana Msimbati na pia tunayo hifadhi yetu kule ya Ruvula ambayo inazo bustani nzuri sana chini ya ardhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa vile umenipa dakika tano, naunga mkono Azimio la Kupandisha Hadhi Selous kuwa Hifadhi na pia tuiombe Serikali basi itangaze ukanda wote wa Kusini, ili watalii wakija Selous wawe na maeneo mengi zaidi, awe akifika Kusini awe amejitosheleza kwa kila kitu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri hii Hifadhi ya Msimbati ndio katika zile *marine reserve* ambazo huwa nazongelea mara kwa mara ni moja ya maeneo mazuri mno ya kuhamia *TANAPA* siku zijazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Riziki Lulida dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Hussein.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru na niunge mkono kwa asilimia 100 azimio hili la kuunga suala la Selous. Nafikiri utaniatambua uwepo wangu katika miaka yote niliyokaa katika Bunge hili nikiitambua

Selous ni pori kubwa sana na ni kubwa na linahitaji mapato ambayo yatasaidia kuchangia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, umenipa dakika tano kwangu nitazifanya kazi. Pori la Selous kwa ukubwa wake lina eka za mraba 154,000 ni kubwa zaidi ya Serengeti, Serengeti ni 12,500 ni zaidi ya mara 12. Sasa leo *TANAPA* mnavyopatia nafasi ndogo katika Pori la Selous atapata wapi mapato, maana yake atakuwa amehifadhi?

Mheshimiwa Spika, ombi langu la kwanza Selous yote iwe ndani ya Hifadhi ya Mwalimu Nyerere kwa sababu za msingi. Tuna *corridor* ya Nyasa Selous ambayo ya Tanzania, ile *corridor* lazima iwe *potential* kwa ajili ya ile wanyama wanapotoka Mozambique wakija Tanzania itakuwa tayari *migration* ile inafanyiwa kazi, nani ataifanyia kazi hiyo *migration*? Leo *TANAPA* ina mapori au hifadhi 16, lakini zinazofanya kazi ni nne tu ambayo ni Serengeti, Kilimanjaro, Mikumi na kidogo Manyara, mmeiongezea pori hili kubwa, mapato yatapatikana wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba usimvalishe shati, mvalishe na suruali anataka awe suti na kama itakuwa ni suti tunahakikisha pori zima la Selous liwe na hadhi moja tu na ninaomba hadhi hii itengezwe katika mazingira matatu; yenye Selous kwa vile ni kubwa itengenezwe *zone* ya Kusini, ya Mashariki na ya Magharibi ambayo ni Matambwe.

Mheshimiwa Spika, mkilifanya Pori la Selous mmelimega sehemu ndogo mtaleta migogoro mikubwa sana ambayo mtashindwa kuiendeleza. Ombi langu tembo ambao wanamalizwa ndani ya Pori la Selous ili kuwalinda na kuweza kuzaliana na nchi kuweza kupata mapato ningeomba Pori la Selous liwe lote moja tu hakuna kubagua, kumega na namwomba ujumbe huu ufile kwa Mheshimiwa Rais, ananitambua kama mimi Mama Selous na kama ni Mama Selous ni lazima Selous iwe neno moja tu Hifadhi ya Nyerere basi, masuala mengine italeta *misunderstanding* kwa vile kutakuwa na mapato yanataka kuingia ndani ya Selous, hapa kumechukua hifadhi ndogo pale Kibiti au Rufiji,

ni eneo dogo sana bado kuna migogoro mikubwa ya wafugaji ambao wako ndani ya Selous, sasa tutaifanya iwe hifadhi hakuna mfugaji mle ndani wala ukulima mle ndani wala uchimbaji mle ndani, utaifanya nchi ipate mapato makubwa.

Mheshimiwa Spika, wewe ulikuwa Liwale unaijua Selous kwa undani wake. Leo Selous hii kuimegamega ni tayari unaitengenezea mazingira magumu na *TANAPA* mtawapa mzigo ambao watashindwa kuitengeneza. Leo *TANAPA* inaweza kuingiza mapato makubwa, lakini mapato yale kama hamjayatengenezea mazingira yake mazuri ina maana mtaifanya *TANAPA* iwe *paralysed*.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tena kusema Pori la Selous kuliweka katika hifadhi mmeiingizia uchumi nchi, ile migogoro tillyokuwa tukizungumza kila siku na kelele tulizokuwa tunapiga sasa hivi tutakuwa tumemaliza kabisa. Matumaini yangu nendeni mkakae, mkajitathmini je, kwa nini tuchukue sehemu ndogo wakati Selous yote ile ni kubwa pori zima liingie katika hifadhi, msibague...

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, endelea.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji mama yangu, ukichukua Selous yote uifanye kuwa *National Park* utakuwa hujaisaidia, chukulia tu mathalani *Serengeti National Park* imezungukwa na *game reserve*, imezungukwa na *WMA*, hizi hapa ni zile ambazo zinasaidia pia wananchi ambao wanazunguka, ili kuona ya kwamba hii *national...*, kumbuka *National Park* huwezi kuwinda, huwezi kufanya chochote zaidi ya kupiga picha, lakini unapokuwa na *game reserve* pembeni unaruhusiwa kuwinda na kuvuna wanyama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nataka tu aone kwamba hili jambo lina umuhimu kwamba, sehemu iwe

*National Park* na sehemu nyingine iwe *game reserve* kwa ajili ya kusaidia wananchi wanaozunguka. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Unaipokea hiyo taarifa, Mheshimiwa Riziki?

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, siipokei kwa vile hajitambui na hajui ninachokizungumzia ni nini, mimi nazungumzia mapato ya nchi, ye ye anazungumzia ubinafsi na inabidi akalisome Pori la Selous ajue maana yake ni nini na *potentiality* ikoje. Na toka tumeanza uwindaji hakuna faida tunayoipata, tunataka Selous iwe ya mapato na maendeleo sio mabishano hapa tunataka kuijenga nchi, tunataka kumsaidia Rais, tunataka kumfanya Rais wetu aweze kutukuka ajue anachokifanya ni nini. Sio kutaka kuleta ushabiki wa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, hapa mimi sizungumzi siasa, ninazungumzia uchumi wa nchi ambao utaifanya nchi yetu iweze kupaa na Rais vilevile anachokifanya wao ambao walikuwa wanapingana nae anataka kuiweka nchi ikae katika *reform*, hivyo sikubalianinae na ninaomba aje nimuekeleze ajue mimi Mama Selous najua Selous kwa undani wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo niiunge mkono hoja na ninasema tena ninawaunga mkono kwa vile leo *TANAPA* inapewa mzigo mkubwa sana. Sasa tutapompa Selous ambayo haina *potential* kama ilivyo kwa Kitulo, Kitulo imepewaa katika hifadhi haina *potential*, Katavi iko katika hifadhi haina *potential*, Buruwando iko katoka hifadhi haina *potential*, Gombe iko katika hifadhi haina *potential*, haya tunakwenda maeneo mbalimbali ya hifadhi ambayo wamepewaa hayana *potential* wanategemea maeneo manne tu na Selous kwa vile yana *potential*/na Selous watalii wanaijua kama Selous ni eneo *potential*.

Mheshimiwa Spika, ni Serikali ya kusimama kuwashakikishia dude hili tunalifanyaje ili iingize mapato. Masuala ya ushabiki, siasa, hakuna, hapa tunataka uchumi

ambao utakuwa endelevu na utamsaidia Rais Magufuli katika maendeleo yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hapo nawashukuruni sana. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Yussuf Hussein dakika tano.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami niungane na wenzangu kuunga mkono azimio liliilo mbele yetu, ila niendelee kuishauri Serikali katika hili kwamba, eneo hili sisi tunapendekeza lote eneo la Selous liwe *Nyerere Conservation Area*. Kwa nini tunapendekeza eneo lote liwe *conservation area*; ni kwa sababu hili eneo tutalilinda lote na hatutaligawa ikawa sehemu moja tunaithamini zaidi nyingine tunaidharau, lakini pia tutaifanya Serikali iweze kuwekeza miundombinu na kuwashamasisha wawekezaji kuja kuwekeza mle ndani ili pato la Taifa liwe kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuigawa vipande vipande utakichukua kipande kimoja utakithamini zaidi na kingine utakichukua kama ni cha kwako tu. Kwa hiyo, tunapendekeza hii Selous iwe *Nyerere Conservation Area* yote na isiwe vipande vipande, ili uhifadhi uwepo zaidi, lakini tuweze kuiendeleza zaidi kwa maana ya kwamba, tuone faida na pato la Taifa linakua.

Mheshimiwa Spika, napendekeza vilevile kama tunalipa jina la Nyerere basi tusimkate, Mwalimu alikuwa na heshima yake kubwa sana hapa Tanzania, Afrika na duniani kote, kwa nini tusiliite *Mwalimu Nyerere Conservation Area?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, neno Mwalimu linaleta heshima na hadhi yake kwa Baba wa Taifa. Kwa hiyo, tusikate tu ikawa Nyerere, nadhani itakuwa, kwa mimi nahisi kama kutakuwa kuna mapungufu fulani hivi katika kumpa ile heshima ambayo amekusudiwa kupewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo nataka kuchangia ni suala la *marketing*. Tunapoipa jina la *Mwalimu Nyerere Conservation Area* au *Mwalimu Nyerere National Park*, whatever na inatoka kutoka Selous wakati duniani Selous ni *worldwide* inajulikana itabidi hapo Wizara isimame vizuri sana kufanya suala la *marketing* kwamba unapoisema hii *Mwalimu Nyerere Conservation Area* au *Mwalimu Nyerere National Park* wale wageni kule au wanaokuja kutembelea waelewe kwamba ni ileile Selous na imebadilishwa jina tu.

Sasa hiyo kazi ya *marketing* kubadilisha inachukua muda kidogo; nafahamu ugumu wa *marketing* katika biashara hii ya utalii. Kwa hiyo, lazima Serikali iwe makini sana katika kulipeleka suala hili huko kuiuza hiyo Selous.

Mheshimiwa Spika, la mwisho Mheshimiwa Waziri wakati mnabeba jukumu hili la kubadilisha Selou kutoka kuwa pori la akiba na kuifanya kuwa *national park* na sisi tunapendekeza kwamba liwe *conservation area* basi tulikuwa tunaomba ile miundombinu kama ambavyo ameeleza Mbunge anayetoka katika mikoa hiyo kwamba, ile miundombinu mle iboreshw. Utakapoboresha ile miundombinu mle na ukafanya vilevile *marketing* kuwahamasisha wawekezaji kuja kuwekeza mle ndani basi, lile suala zima la kuhifadhi lile eneo na lile suala zima la kwamba tunataka kuikusudia kuitangaza hii *Stiegler's* ambayo inajengwa pale itakuwa imepata maana kamili maana wawekezaji watakapoongezeka mle ndani baada ya kuboreshwa kwa miundombinu maana yake ni kwamba, pato la Taifa litaongezeka na uhifadhi utaongezeka zaidi kuliko kuacha tu sehemu ikawa inahifadhiwa na sehemu ikaachwa kuwa nini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapendekeza iwe *Mwalimu Nyerere Conservation Area* eneo lote la Selous badala ya kuchukua kipande tu. Hii tunapendekeza sana kitaalamu Mheshimiwa Waziri na tunaomba Serikali ikae iliflikirie hili na hili eneo tusiligawe vipandevipande itakuwa tunaliharibu ule uasilia wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba Selous ni *worldwide*, kwa hiyo, tukiigawa tunaanza kuipotezea ile heshima yake. Jina kubadilika tu sio tatizo, lakini ile heshima ya Selous ibaki kama ilivyo na tunapendekeza iwe *Mwalimu Nyerere Conservation Area*, ili iweze kukidhi mahitaji na matakwa ya dunia, lakini mahitaji na matakwa yetu na pato la Taifa liongezeke. Nakushukuru. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Kiwanga, kwa sababu CHADEMA hamjaongea, utapata dakika 10.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, sijui kama nitazimaliza kwa sababu nina mambo machache tu ya kuchangia, nashukuru sana kwa kunipa hizo dakika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niko hapa na mimi ntoka kwenye eneo la Selous, lakini kwa mujibu wa hii ramani nachanganyikiwa sijui ndio ipi, kama ni hifadhi, kipande fulani kinahifadhiwa? Sasa najiuliza je, kule Mlimba ambako kula wale puku hawapatikani mahali popote isipokuwa kwenye lile pori, ndio eneo ambalo linaenda kuhifadhiwa? Kwa sababu, hii kwenye ramani imenichanganya kidogo, sielewi ni eneo lipi?

Mheshimiwa Spika, hata mimi nilikuwa na mawazo kwamba labda lote sasa linahifadhiwa na hi itasaidia kwanza wananchi tunaoishi pembedi ya hilo pori sasa *TANAPA* wakiingia na sisi tutaanza kupata mapato ukiachilia mpaka...

**SPIKA:** Kinachohifadhiwa ni ile mipaka inayoitwa Selous hivi sasa vilevile ilivyo. Vilevile ilivyo Selous kwa mipaka yake ya sasa, endelea Mheshimiwa.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa hiyo, mimi naungana na wenzangu waliosema bora tulinyanyue lote kwa sababu itatusaidia, kwa nini nasema hivi?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kinachoendelea huko kwenye maeneo ambayo sio mipaka ya Selous watu wanaingia wanalima, yaani kunakuwa na ugomvi, mara zimewekwa *beacon*, mara zinaondolewa, watu wanalima, watu wanafuga, lakini huko huko kuna mhanganyiko na wanyama. Kwa mfano kwenye lile eneo lile kuna puku wanapatikana duniani ndio kule tu, sasa hivi wanaisha, wanaitwa sheshe, kitaalamu wanaita puku, sheshe.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu sheshe ni mnyama fulani kama swala pala, lakini mdogo kama mbuzi hivi, lakini mkubwa kidogo kuliko mbuzi, lakini yeze *characteristic* yake ni kwamba badala ya kwato kukaa kama kawaida zile za mbuzi au nini kwato zake yeze zinakuwa ziko wima namna hii. Anapenda kukaa kwenye maeneo ya mafuriko, halafu panapokuwa na kamuinuko hivi basi anakaa hapo juu hivi. Ni mnyama anapatikana eneo hilo peke yake.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, sasa kuna vivutio kama hivi tunafanyaje? Hiyo mipaka ya Selous kwanza mimi sijui vizuri eeh! Basi kama ndiyo hivyo? Tupandishe lote ili kuondoa muingiliano wa wanadamu katika hili eneo ambalo tunaita la hifadhi urithi wa dunia. Wakati tunapanga kupandisha hivyo na tunaita hiyo hifadhi Mwalimu Nyerere tuone namna gani wananchi katika maeneo hayo vijiji vinavyozunguka haya maeneo wapewe elimu watafaidika vipi na uhifadhi huo, bila hivyo kutakuwa na ugomvi.

Mheshimiwa Spika, hapa tunasema tu tunapandisha, lakini je wananchi kule wameenda katika maeneo hayo? Je, wamepewa elimu? Mimi naona tutumie nguvu ya ziada tuende tukaoe elimu katika maeneo hayo

lakini ushauri wangu naomba tupandishe hilo pori lote hadhi ili tuhifadhi urithi wa dunia ulioko ndani yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Itete wale *Swala Energy* wameenda kuchoronga choronga visima pale vy a gesi kama sikosei ndani ya Selous lakini pale Itete wanakwenda kuchoronga vile visima vy a gesi ndiyo wanyama wako pale, wale wachorongaji wako pale na wanyama wako pale na Swala hao aina ya Puku ninaosema ndiyo walikuwepo kwenye maeneo hayo. Kwa sababu ya mwingiliano na watu sasa hivi wamekimbia wamejificha kule Utengule sijui unakujua? Kule Utengule kule ndiyo waliko wanahangaika hawajui waende wapi. Je tunahifadhi nini? Hamuoni kama hiyo ni rasilimali kubwa ya Taifa? Tunafanyaje? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wale watu ambao bado wanapendelea pendelea bado kula nyama za porini wanawawinda wale wanawala. Mimi ni-*declare* hapa *interest* kwamba zamani nilivyokuwa mdogo tulikuwa tunakula nyama ya Sheshe ni tatu balaa lainii! Lakini siku hizi hatuli tena kwa sababu hamna, sasa hawa waliopo mnawalindaje? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hebu tuone namna ya kulinda hizo hifadhi, huo urithi wa dunia ambao uko Tanzania tuone kwamba na wananchi watapata mafanikio.

Mheshimiwa Spika, pia hapo hapo sijui Selous labda Mheshimiwa Dkt. Kigwangwala ataniambia pale Kilombelo North Safari Kitalu cha Uwindaji nasema kila siku, yule jamaa mipaka yake hajulikani, mara anachoma nyumba za watu, mara anachoma vyakula, mara ukienda Polisi havieleweki na nimeomba mara nyangi mje muangalie pale, kwa sababu lile eneo ni kero kubwa.

Mheshimiwa Spika, kingine tukihifadhiwa hilo eneo lote, Serikali ione haja sasa ya kuweka uzio kwasababu ninavyosema mpaka leo tembo wanashinda kwenye kijiji cha Iduindembo kule Utengule, wanatoka kwenye haya maeneo

ya hifadhi, wanakuja vijijini wanakesha vijijini yaani watu wako hoi. Kibaya zaidi Wilaya ya Kilombero ni kubwa sana kuanzia Kidatu mpaka huko mpakani mwa Njombe, hata huyo Afisa wa Maliasili aliyepo pale hata ukimpigia anahangaika tu tembo wanakatiza mara Mkula hapo wanatoka Selous wanaingia Udzungwa, nadhani mnaelewa, wanaingia huko kila mahali sasa huyu mtu mmoja, gari moja hana uwezo, hivi atasaidia vipi kwahiyio wananchi wanataabika na tembo. Kwa hiyo mapendelekezo yangu ni bora sasa tukatoa elimu kwa wananchi tukahifadhi hili eneo lote ili tutenganishe. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan kule Zanzibar wanaitwa ndovu.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ndovu! Sasa hapa siyo Zanzibar hapa ni Tanzania Bara hawa wa Zanzibar watajua wenyewe huko, tukienda Zanzibar tutababilisha Kiswahili. Kwa hiyo, mimi najua ni tembo na wananchi wangu kule wakisikia tembo ndiyo wataelewa mambo ya ndovu wanajua zile pembe tu sijui unayo habari? Ukisikia ndovu kwetu ni zile pembe tu lakini lile ‘limnyama’ lenyewe linaitwa tembo, lile linaenda kusumbua kule vijijini. Kwahiyio, ningependelekezo pamoja na mambo hayo naomba muwaongezee nguvu watu wa Maliasili walioko kule Wilaya ya Kilombero ya magari na wafanyakazi ili watusaidie katika kudhibiti tembo wanaokuja katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote kuanzia huku Mkula, Magombela wapi kote ni shida tupu, Sanje tunaopakana na Udzungwa tunashida sana, tembo wanakatiza wanaenda Udzungwa wanarudi Selous, kwa hiyo wanapita katika majumba ya watu. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana dakika tano zimeisha.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, dakika tano ulinipa dakika 10 nilisema sijui kama nitamaliza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan mwenyewe ukazipunguza.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, nikajipunguzia Saba siyo Tano.

**SPIKA:** Haya malizia Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba Kurudia tena hebu mtusaidie mpandishe hilo pori lote, kwa sababu kuna mwingiliano, ng'ombe kule ndiyo usiseme! Kila siku ninasema wale ng'ombe walioko kule wako Tanzania, nyama tunakula, maziwa tunakunywa na ngozi tunazihitaji, kwa nini msiweke miundombinu badala ya kuwaswaga swaga wale wanyama mara waende Rufiji mara wapi, kwa nini msiwatafutie maeneo na hifadhi ziko nyingi? Kwa mfano, hapa Kongwa kwako hivi tunashindwa nini hiyo hifadhi ya Kongwa, kuwaleta wafugaji amba wana uwezo wao kuwapatia *block*, kuwawekea miundombinu ya kuotesha nyasi za kisasa, kuweka malambo Madaktari, viwanda vyta maziwa, viwanda vyta ngozi ili tufurahie urithi wa Tanzania na hao ng'ombe wetu hivi mnashindwa nini? Hapa Kongwa hakuna ng'ombe kula nguchilo tu hili pori, kwa nini msiwalete hawa wafugaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa mnapopandisha hadhi wale ng'ombe watakwenda wapi? nasi wakulima kwa sababu kule hatulimi tena mtuwekee miundombinu katika vijiji vyetu, kutuchimbia mabwawa kutuwekea kilimo cha umwagiliaji, uvuvi wa samaki kwa sababu Kilombero tutakuwa hatuvui tena. Ninyi mna matatizo gani Serikali? Kwa nini hamyaoni hayo? (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumekuja hapa kushauri hayo ndiyo wanayosema wananchi, huo ni ushauri wangu ndiyo maana wakati wa maliasili tulivyopendekeza Wizara zitumbuliwe hapa na mtu wa mifugo tulimtumbua kwa sababu haisaidii Serikali kuwapa miundombinu ni namna gani kuwalea hawa wafugaji ili watupatие uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na Mungu atubariki sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Suzan ahsante sana. Baadae watafute Wazanzibar wakupe tofauti ya maneno hayo mawili. Tunamalizia kama yupo Dkt. Kiruswa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga dakika tano tano.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja hii ya hili Azimio lilitoko mezani. Kwanza *declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati na moja ya mambo ambayo tumeyachekecha katika kupitia na kutolea maoni Azimio hili ni uhalisia wa eneo ambalo limependekezwa limeguliwe na sehemu fulani ibakie kuwa Hifadhi ya Taifa na sehemu nyingine ibakie kama Pori la Akiba.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wetu kwenye Kamati ambayo maoni yetu nayaunga mkono asilimia 100 pamoja na wazo la Mheshimiwa Rais la kupanua wigo wa maeneo yaliyohifadhiwa nchini na kuweka sehemu ya Selous kuwa mojawapo, tumeona kwamba kuna faida mara mbili endapo eneo hili litachukuliwa katika ujumla wake na kuhifadhiwa kama mamlaka sawa na ile ya Ngorongoro. Kwa maana hiyo sasa tutakuwa na mamlaka mbili ya maeneo yaliyohifadhiwa yenye matumizi ya aina mbalimbali badala ya kuwa matumizi ya aina moja tu kwa maana ya tofauti ya *National Park* na *Conservation Area* ni kwamba kwenye *National Park* ni *exclusive use* ya matumizi ya kupiga picha tu utalii wa picha, lakini kwenye *conservation area* kuna matumizi mseto ndiyo maana kwa sababu eneo hili lilikuwa ni eneo la akiba la uwindaji, tutakapokuwa tumekubaliana kwamba sasa na yenyewe liwe mamlaka kama Ngorongoro, tutakuwa na hiyo fursa ya kuwekeza kwenye utalii wa picha katika yale maeneo ambayo utalii wa picha unawezekana hasa eneo la Kaskazini maana nimeangalia katika kumbukumbu zilizopo hili pori linaweza likatengwa katika maeneo manne. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo la Kaskazini ambalo limepakana na Hifadhi ya Mikumi ni eneo safi kabisa kwa utalii wa picha na eneo la Mashariki na eneo la Kusini na

eneo la Magharibi haya ni mapori ambayo hata leo tukisema yote iwe *National Parks* itatuchukua miaka mingi sana kuyaendeleza, kuwekea miundombinu, kuna milima kuna misitu kuna maeneo oevu na ningefikiri kwamba tunapochukua kama ni eneo la hifadhi kama la Ngorongoro tunakuwa tumepata faida ya kuwa na maeneo ya utalii wa picha na yale matumizi mengine ya uwindaji wa kitalii ambayo yatafanya yale mapato yawe maradufu.

Mheshimiwa Spika, tutapata mapato kutokana na utalii wa picha katika eneo ambalo lina hadhi ya kama *National Park* na tunapata matumizi ya ule uwindaji wa kitalii ambao pia utatuletea manufaa makubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo katika Kamati tuliona kwamba mapendekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo tunayaunga mkono asilimia 100, yallitamka Nyerere *National Park*, tukasema tusipoteze jina la Mwalimu wetu kwa sababu Mwalimu ni cheo ambacho mtu hata ukipandishwa hadhi ukawa Rais bado utaendelea kuitwa Mwalimu na ndiyo maana Mwalimu anaitwa Mwalimu milele.

Kwa hiyo, ibakie kwamba Mwalimu Nyerere *Conservation Area* kama ndiyo moja ya majina ambayo tunapendekeza kama Kamati nami naunga mkono, pia lisimamiwe na *TAWA*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu unaweza ukajiuliza hapo ulipo kwamba Ngorongoro ndiyo waje wasimamie? Jibu ni hapana *TAWA* tayari walikuwa wanalisimamia kama pori la akiba nasi katika maoni yetu na maoni yangu binafsi naona kwamba *TAWA* nao wapewe fursa ya kusimamia eneo la hifadhi inayofanana na Ngorongoro, wakachukue somo kule Ngorongoro wamefanikiwaje na wawekewe kabisa bajeti ya kutosha kwa sababu lile pori ni kubwa wawewe kuli-manage likiwa na sehemu mbili. Sehemu ambayo ina utalii wa picha, linalofanana kabisa na Mbuga yoyote ya Taifa na eneo lingine liliobaki ambalo litaendelea na yale matumizi ambayo yalikuwa yameshabainishwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa najiuliza na naomba hili nitoe kama maoni binafsi kwamba huku sasa tunaelekea kuwa na taasisi mbalimbali za uhifadhi hapa nchini, tunayo *TAWA*, tunayo Misitu, tuna *TANAPA*, na sasa pia tuna Ngorongoro, kwanini tusifikirie tuunganishe hivi vyombo vyote tukawa na chombo kimoja? Kwa mfano Kenya, wao wanayo 'Kenya Wildlife Service', Uganda wanayo 'Uganda Wildlife Service' nasi labda tuje na pendeleko nilikuwa najisemesha mwenyewe hapa kwa kufikiria nikasema kwanini tusiwe na Tanzania *Wildlife and Nature Conservation Authority* ikachukua hizi Taasisi zote pamoja zikaunganishwa tukawa na mamlaka moja inayosimamia uhifadhi wa wanyamapori na mazingira yake katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tukija na huo *model* basi tutakuwa tunaya-*manage* maeneo yote bila kuwa na utengano na kuwa na moja ambayo inajiona kwamba ni dhaifu, nyingine ni bora kuliko nyingine na kwa njia hiyo tutakuwa tumehifadhi rasilimali yetu ya Tanzania katika upeo na mtizamo mpana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba maono ya Mheshimiwa Rais na hekima yake tumepokea kwa furaha kabisa na tunampongeza kwa kuwa na maono ya kuhifadhi Selous kama *National Park* na tunamuongezea maoni yetu kwamba iwe ni mamlaka ambayo inasimamiwa kwa ujumla wake bila kugawanywa na isimamiwe na taasisi moja ambayo ni *TAWA*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kuwasilisha na naunga Azimio mkono asilimia 100. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Mlinga halafu Mheshimiwa mtoa hoja Mheshimiwa Waziri.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami naomba nitoe maoni yangu machache kuhusiana na upandishaji wa hadhi wa pori hili kuwa *National Park*.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kupandisha hadhi pori hili kwa sababu tukiangalia wenzetu wa Kaskazini kule Mji kama wa Arusha umeendelea sana kutokana na utalii, namii kwa mfano Jimbo langu la Ulanga sehemu kubwa sana ni *Selous Game Reserve* sasa kwa kupandisha hadhi kuwa *National Park* kuna vitu vingi sana tutapata fursa vikaweza kuonekana. Kwa mfano tu nilienda maeneo ya Monduli nikakuta watalii wanaangalia ngoma za Maasai ambao wanaruka ruka, lakini kwetu Ulanga tuna ngoma inaitwa Sangula ni ngoma nzuri sana, nadhani itajulikana hata Kimataifa pia kuna milima mizuri na mambo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba niongelee suala la Stigler's. Mheshimiwa Rais wakati anatoa kauli wakati wa anazindua ujenzi wa bwawa hili alisema kuwa watu watakuwa wanaruhusiwa kwenda kufanya uvuvi lakini tunafahamu sheria za *TANAPA* na Sheria za Uhifadhi haziruhusu watu kwenda kwenye maeneo haya, kwa hiyo naomba hili liwekwe *clear*.

Mheshimiwa Spika, pia tunapokuja kutoa matamko hayo pia tuangalie na Sheria hizi za Uhifadhi na Sheria za *TANAPA* kwa sababu Sheria ya Uhifadhi wa Misitu ya Wanyamaporin inasema kuwa, ng'ombe wakikamatwa au mifugo ikikamatwa inatalfishwa lakini ile Sheria ya *TANAPA* ni ya kupiga faini, hivyo tunataka sheria moja *uniform* ambayo itakuwa haiathiri mifugo yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala langu zito nililokuwa nataka niongelee ni kuhusu wafanyakazi, naona Wizara wanaliwepa na Kamati wanaliwepa. Wote tunafahamu *Game Reserve* inakuwa chini ya *TAWA*, mfanyakazi wa *TAWA* kima cha chini cha mshahara hakizidi shilingi laki nne. Leo hii inapandishwa hadhi inaenda kuwa chini ya *TANAPA* na *TANAPA* mshahara kima cha chini siyo chini ya shilingi milioni moja, leo hii inapoenda kupandishwa hadhi *TANAPA* hawataki kuwarithi hawa wafanyakazi ambao wamefanyakazi kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Waziri wakati ana-*wind up* atuambie hawa wafanyakazi wa TAWA na wenyewe waende wawe chini ya TANAPA irithi pori pamoja na wafanyakazi kwa sababu wamefanyakazi muda mrefu, vyuo wanavyosoma ni vilevile, fani ni ile ile, mapori ni yale yale wanyama ni wale wale, kwa nini TANAPA ing'ang'anie kwenda kuajiri wafanyakazi wengine wakati wafanyakazi wapo amba wana uzoefu na taaluma zile zile. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba atoe kauli kuhusiana na hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni suala la vitendeakazi. TAWA wana miliki wanyama wote amba wako ndani ya mbuga na nje ya mbuga lakini vifaa hawapewi, TANAPA wanamiliki wanyama wachache amba wako kwenye *National Park* tu lakini wanapewa kila kitu resources zote wanazo, tunaona kwa mfano tembo walioonekana Dodoma TAWA ndiyo wanahuksika, tembo wanaoingia maeneo ya makazi yote ni TAWA lakini hawana vifaa kama alivyosema Mheshimiwa Suzan unakuta Kanda nzima wanapewa gari moja ama mawili. Kwa mfano wa Ulanga kule sasa hivi tembo wanasumbua mitaani lakini hawana vifaa. Kwa hiyo naomba TAWA waongezewe vitendeakazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja lakini naomba suala la wafanyakazi litolewe kauli. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mlinga, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri aje hapa mbele dakika 10 karibu sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nianze kusema kwamba naunga mkono hoja na niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote amba wametoa maoni na ushauri kwa hoja ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwenye wasilisho lake mapori yetu yote Hifadhi za Taifa na Mapori ya Akiba kinachotofautiana ni matumizi ya maeneo lakini yote yanasmamiwa na yanalindwa na yana ulinzi wa kutosha. Tunapopandisha hadhi pori la akiba la Selous na kuliita Nyerere *National Park* kinachobadilika pale ni matumizi tu ya eneo hilo, kwamba sasa tunakwenda kufanya zaidi utalii wa picha badala ya utalii wa awali ambaao ulikuwa unaruhusu utalii wa picha na uwindaji, lakini matumizi mengine yote na namna ambavyo yanasmamiwa na ulinzi yanafanana. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi kabisa Waheshimiwa Wabunge ambaao wameonesha kana kwamba kubadilika kwa hadhi sasa Wizara iende kuanza upya kufikiri namna ya kuhifadhi eneo hilo lakini na kuondoa wafugaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wote ambaao tumewaona kwenye maeneo ya hifadhi na mapori ya akiba ni wavamizi na wamekuwa katika maeneo hayo kinyume cha sheria, kwa hiyo wawe ndani ya *National Park* au wawe ndani ya *Game Reserve* hawa wako kinyume cha sheria na wanashughulikiwa na sheria ile ya Uhifadhi ambaao hawatakiwi kuwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nijibu tu maeneo mawili matatu ambayo Waheshimiwa Wabunge wamesema na Kamati, moja ni la kushirikisha wadau, wadau wameshirikishwa na mchakato huu tangu Mheshimiwa Rais alipotoa maelekezo pale wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa bwawa la umeme wadau mbalimbali wameshirikishwa wakiwemo hao wenye mahotelii lakini pia wakiwemo wadau wanaofanya biashara za utalii na wananchi wa Mikoa ya jirani ya maeneo hayo. Kwa hiyo niwatoe wasiwasi kwamba suala hili halijakimbizwa kwa haraka, hakuna mdau ambaye hakusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, katika wadau wakubwa ambaao walikuwa katika maeneo yale, hasa ambaao wanaathirika na ujenzi wa bwawa, Wizara kuititia Serikali wapo ambaao wameguswa na wamepata fidia na wamepewa maeneo mengine ya kwenda kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo limeonekana lina shida kidogo ni kwamba eneo la hifadhi hii ni kubwa sana na kwa sababu hiyo yako maeneo ambayo hayatumika kwa leo kwa faida, ni kweli kilometra za mraba elfu 30 ni nyingi na huwezi kuziendeleza na kuzitumia kwa mara moja. Kama mnavyofahamu tumekuwa na *traditional product* mbili sana Tanzania ni mbili tu ya kwanza ni Safari ambayo ni ya kupiga picha, na nyingine ni ya kupanda Mlima Kilimanjaro sasa maeneo haya ambayo yalikuwa yanatumika zaidi kwa uwindaji ni maeneo ambayo *terraining* hairuhusu utalii wa picha na wakati mwingine utalii wa safari tuliozoea, lakini huu ni muda muafaka wa ku-develop aina nyingine ya *product* kwenye maeneo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, labda tu nitoe mfano, ukienda leo Serengeti utakutana na *balloons* nyingi zipo mle ndani ambapo wawekezaji kadhaa wameingiza *balloons* ambazo zinaweza kutoa watu sehemu moja kwenda sehemu nyingine lakini pia tunafikiria hii milima mingi iliyomo katika pori la akiba la Selous tunaweza ku-*introduce cable cars* pamoja na maboti yanayopita kwenye maeneo ambayo sisi tunaona kwamba hayapitiki lakini kuna hiking na michezo mingi ambayo inatumika kwenye maeneo ambayo hayatumiki kwa utalii wa picha. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi kabisa Waheshimiwa Wabunge kwamba eneo hili tutakapolichukua litabaki bila matumizi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, imezungumzwa hapa kuhusu vivutio vingi vya utalii vilivyopo mikoa ya kusini. Ni kweli kwamba mchakato huu unakwenda kufungua Mikoa ya Lindi na Mtwara na tunakwenda kufungua ukanda wote wa mashariki (ukanda wa bahari) na kwa sasa hivi baada ya mchakato huu kukamilika, kwanza nilitaka nitoe taarifa kwamba maeneo yale ya Mikindani na Kilwa yote haya mwanzo yalikuwa hayajidhesi vizuri kwenye shughuli za utalii lakini Wizara ilikaa na kufikiri na kuona kwamba ili yaweze kuwa sehemu ya *package* ya watalii wanaotembelea maeneo haya na kwa juhudzi za sasa za kupandisha hadhi eneo hili kuwa hifadhi ya Taifa ambazo

zitaongeza miundombinu na kufungua maeneo haya yote, tuliyauunganisha pamoja na taasisi zetu zote kama *TAWA*.

Mheshimiwa Spika, na juzi nilikwenda Mafia nimekuta *TAWA* wapo pale wanaimarisha miundombinu lakini Mikindani pale wapo na hata maeneo yote ambayo ameyasema Mheshimiwa Hawa Ghasia ni maeneo ambayo tayari tumeyaweka kwenye mpango kazi wa kuyafungua.

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba hata huu mradi wa *REGROW*ambao sasa ulikuwa sehemu ya juu ya Selous, awamu hii ya kwanza ya mradi huu wakati inaendelea kutekelezwa, Wizara imo katika mchakato kabambe wa Awamu ya II ya *REGROW* ambao sasa utaenda kuunganisha mikoa hii miwili ya huku chini na kuifungua kabisa na kuifanya iwe ni mikoa muhimu kwa ajili ya utalii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba tunatambua vivutio vingi viro maeneo hayo, tunaamini kwamba tutakapoimarisha miundombinu na utangazaji wa maeneo hayo na tutakapokamilisha sasa uwekezaji, tutahamasisha biashara ya utalii ambayo imekuwa ni kivutio na chanzo kikubwa cha mapato kwa mikoa ya kaskazini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Costantine Kanyasu. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Waziri aje ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Waziri karibu una dakika 20.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. awali ya yote nianze kwa kukupongeza wewe na mfumo mzima wa taasisi yetu ya Mhilimi wa Bunge kwa kukubali hoja hii iingie hapa Bungeni siku ya leo lakini pia zaidi kwa kutoa ushauri, mchango na mapendekezo mbalimbali ambayo yanalenga katika kuboresha utekelezaji

wa majukumu ya usimamizi ambayo Serikali imepewa na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili; nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa uamuzi wake wa kuamua kubadili matumizi ya sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Selou kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere. Na niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote pamoja na Serikali kwa ujumla, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri na mwongozo katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kuleta hoja hii hapa Bungeni siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara yetu wakiongozwa na Katibu Mkuu Prof. Adolf Mkenda kwa kuendelea kutupa ushauri wa kiufundi ambao umetuwezesha kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe ufanuzi kwenye maeneo machache ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa wabunge lakini pia niwaahidi kwamba kwa yale ambayo sintoweza kuyagusa, hususan yaliyoletwa kwa maandishi na hata mengine ambayo yamechangiwa kwa kusema hapa Bungeni, basi tutayazingatia katika kutekeleza maagizo haya baada ya azimio hilli kufanikiwa kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo naona kubwa na limejitokeza sana ni suala la kwa nini eneo lote la *square kilometer* 50,000 za Pori la Akiba la Selous lisigeuzwe kuwa eneo la uhifadhi maalum la Nyerere. Niliona alitoa taarifa hapa Mheshimiwa mchangiaji mmoja kwamba pengine huu mfumo ulivyo kwa sisi kupandisha hadhi sehemu tu ya ikolojia nzima una maana yake. Japokuwa pia hata kama tungetaka kuutazama mfumo huo wa *conservation area* tukaunganisha na maeneo mengine pia ingeweza kufaa tu. Lakini kwa sasa tunaona mapendekezo haya ambayo yanatokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais inafaa zaidi kwa hivyo ambavyo tumeyaleta na tunaomba Waheshimiwa Wabunge wapitishe mapendekezo haya kama yalivyo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza; ni ukweli kwamba Hifadhi za Taifa kwa mfumo wa ikolojia ambao upo katika nchi yetu, huwa zinakuwa zimefichwa na maeneo yenye hadhi nyingine za uhifadhi katika mzingo wake. Kwa maana ya kwamba kama kuna Hifadhi ya Taifa katikati kwenye kiini ambayo inatengeneza kiini cha ikolojia hiyo basi pembezoni mwake kunakuwa aidha na mapori ya akiba, mapori tengefu, misitu ya hifadhi ama maeneo ya jumuiya za uhifadhi za wananchi. Na haya maeneo mengine yanafanya kama vile *buffer* ya hiki kiini ambacho kinakuwa ni Hifadhi ya Taifa. Na huu ndio muundo ambao utaupata katika ikolojia zote.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hata ikolojia maarufu zaidi hapa nchini na duniani kote kwa ujumla wake ikolojia ya Serengeti kuna mapori ya akiba kama ya Ikolongo, Gurumeti, Pori la Akiba la Maswa, Poli Tengefu la Loliondo, kuna eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; yote haya yanaizunguka ikolojia pia Lake Natroni kwa kule juu yote haya yanaizunguka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Kwa hivyo, kunakuwa kuna maeneo mengi ambayo yapo katika hadhi tofauti tofauti za uhifadhi ambapo katikati yake ndio kunakuwa kuna Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, na muundo huu haupo kwa bahati mbaya, muundo huu unatuwezesha kuwa na uhakika wa kuwa na hifadhi ya Taifa katika kiini lakini pia unasaaldia matumizi mengine kufanyika katika maeneo ambayo yana hadhi nyingine tofauti, kwa mfano kama ni kwenye mapori ya akiba na mapori tengefu na kama kuna wanyamapori basi inaruhusiwa kuwindha wale wanyama lakini pia kama ni maeneo ya misitu basi hapo itaruhusiwa kuvuna ile misitu ili iweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu malengo ya nchi yetu sio kuwa na maeneo ya hifadhi na kuwa nayo tu, malengo ya nchi yetu ni kuwa na maeneo ya hifadhi lakini pia kuyafanya maeneo haya yatusaidie katika kupambana na umasikini. Yatupe kipato ambacho kitatusaidia kutekeleza miradi mingine. Kwa hivyo, tunaangalia siku zote tunafanya

*trade off kwamba eneo hili tutafaidika zaidi tukifanya nini, tukifanya utalii wa picha ama tukifanya utalii wa picha na uwindaji ama tukivuna miti. Kwa hivyo hivyo ni vigezo katika vigezo ambavyo vinatufanya tuamue eneo gani liwe nini kama Taifa na ni muundo ambao umedumu kwa muda mrefu na haujawahi kutuangusha.*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, tunaomba kwa kweli muundo huu tuendelee kuulinda na hata kwenye hii Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kuna jumuiya za uhifadhi wa wanyamaporu ambazo zipo zinazunguka hifadhi hii; kuna misitu kama alisema Mheshimiwa Mchengerwa na Mheshimiwa Bobali ambapo wanavuna miti wale hawavuni miti Selous, wanavuna miti kwenye misitu ya hifadhi ambayo ipo pembezoni mwa Selous. Kwa hivyo, ni vitu kama hivyo kwamba hii maliasili tunaitumia kwa kuvuna, tunapovuna tunauza tunapata faida kama nchi inatusaidia kuhifadhi maeneo yenyewe lakini pia inatusaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii ikiwemo barabara, shule, afya na vitu vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, hata pale Selous inapozunguka watu wengi hudhani kwamba miti inavyovunwa pale ama mikaa inayochomwa pale basi imetoka Selous kwa sababu wananchi katika nadharia yao wanadhani eneo lote lile tu kwa sababu tu ni msitu basi lote ni Selous, hapana pembezoni mwa Selous kuna hifadhi za misitu hususan katika eneo hilo la Wilaya ya Liwale lakini pia ukipanda kwa juu zaidi kuna jumuiya ya hifadhi ya wanyamaporu, jumuiya ya Gonabis ipo pale kutoka kule Wilaya za Kibiti mpaka kule eneo la Kisarawe. Lakini pia kwa upande wa huku utakuta kuna Hifadhi ya Misitu ya Udzungwa, kuna Kilombero Pori Tengefu la Kilombero ambalo alikuwa analizungumzia Mheshimiwa Suzan Kiwanga.

Mheshimiwa Spika, na hapa labda niseme kidogo kwa sababu amelzungumza kwa kirefu kwamba wale Sheshe wanapaswa kuwa katika Pori Tengefu la Kilombero na kwa sasa katika ramani mpya ya kutengeneza hii ikolojia ya huku

kusini upya, tumeamua kupandisha hadhi Pori Tengefu la Kilombero ili sasa liende likawe Pori la Akiba la Kilombero yaani iwe *Kilombero Game Reserve*. Na sababu kubwa ni pamoja na kuhifadhi hao Sheshe. Walikuwa zaidi ya 40,000 mwaka 1990 leo hii wamebaki 4,000 tu na hao Kampuni ya Kilombero North Safaris wanasaidia sana katika kutoa ulinzi kwa hao Sheshe ambao wamesalia.

Mheshimiwa Spika, pia Kilombero ilikuwa mashuhuri kwa makundi makubwa ya Nyati na Tembo ambayo sasa hivi huyaoni tena. Kwa hivyo, tumekusudia kwa kweli kwa dharti kuimarisha ulinzi katika eneo hili. Pia naomba ifahamike kwamba Milima ya Udzungwa, Milima ya Mahenge na Milima ya Mbalika kwa ujumla wake ndiyo inatusaidia kupata Bonde la Kilombero ambalo linafanya kazi kama chujio la kupeleka maji katika Mito hiyo ya Luwegu pamoja na Mto Kilombero kutengeneza Mto Ulanga ambao unaenda kutengeneza hilo Bonde la Stiegler ambalo tunakusudia kuzalisha umeme takribani megawati 2115.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, uhifadhi wa eneo hili *upstream* huku Kilombero ni muhimu sana na kwa maana hiyo tumeamua kupandisha hadhi eneo hili lakini pia Milima ya Mahenge na misitu yake, Milima ya Mbalika na misitu yake na maeneo ya jirani ambayo bado hayana watu tunayapandisha hadhi kuwa Pori la Akiba la Kilombero. Pia tunatoa sehemu kubwa kutoka 6,500 square kilometer mpaka kubakisha 2,500 za kiini cha bonde kurudisha kwa wananchi kwa ajili ya kupunguza presha ili waweze kuishi kihalali na waweze kufanya shughuli zao za kilimo na ufugaji katika eneo ambalo sasa litakuwa halali kuliko ilivyo hivi sasa ambapo wanahesabika kama wavamizi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, tumeangalia sana suala hilo kwa ujumla wake na haswa kwa faida hizo kubwa za kiuhifadhi lakini pia faida pana zaidi za kitaifa za kuzalisha umeme katika Bonde la Mto Rufiji.

Mheshimiwa Spika, pia ilijitokeza kwa kina sana hoja ya *TANAPA* kubebeshwa mzigo. Na sisi tunaona lakini tofauti

ya maeneo yanayohifadhiwa na kusimamiwa na *TANAPA* na yale yanayohifadhiwa na kusimamiwa na *TAWA* kwa kweli ni matumizi tu, umuhimu wa maeneo haya ni uleule bioanuai iliyopo kwenye maeneo haya ni ileile na pengine wakati mwininge mapori ya akiba yanaweza yakawa yana bioanuwai nzuri na nyeti zaidi kuliko hata Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, hii lugha ya kwamba tunapandisha hadhi ni lugha tu rahisi lakini kimsingi hatupandishi hadhi, tunachokifanya tunabadiilisha matumizi ya eneo kwamba eneo hili matumizi yanaruhusiwa, eneo hili matumizi ya *resource* iliyopo pale hayaruhusiwi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, maeneo haya ni muhimu sana na kwa takwimu za haraka haraka *TAWA* ambayo kwanza ni taasisi changa sana inasimamia takribani maeneo yenye ukubwa wa kilomita za mraba 250,000 wakati *TANAPA* inasimamia eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 60,000 baada ya kuongeza na hizi hifadhi mpya tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ukiangalia pia bajeti ya *TANAPA per square meter* nukubwa sana, ni zaidi ya asilimia 157 katika *standard* ambazo zimewekwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhifadhi wa Bioanuai (*ICUN*) wakati *TAWA* wapo kwenye asilimia 83, kwa hivyo bado hawajafikia hata ile asilimia 100 ya *per square meter* ya eneo ambalo wanapaswa kusimamia. Ngorongoro wameshafika zaidi ya *per square meter* kwa asilimia 600 zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, ukipiga hesabu hizo unaona kabisa kwamba kwa kweli mgawanyo wa *resources* ambazo zinapatikana *per square meter* ya eneo ambalo linahifadhiwa bado unaipa *disadvantage* kubwa sana taasisi hii ambayo bado ni changa pia ya *TAWA*.

Mheshimiwa Spika, hivyo, katika uelekeo wetu wa mbele, tunaona kwamba ili kuondoa hii *fragmentation* ya mgawanyo mbovu wa rasilimali katika taasisi ambazo zinafanya kazi ileile ambayo ina umuhimu uleule, tunakusudia ndani ya Serikali bado tunaendelea na mchakato wa ndani

kufanya kidogo *amalgamation* ambayo tutamtenga *TANAPA* atabaki peke yake na tutamchukua *TAWA* tutamuunganisha na Ngorongoro kutengeneza taasisi moja yenye nguvu lakini pia itakuwa ina nguvu ya rasilimali ili iweze kusaidia ku-*balance* kidogo uwiano *per square meter* wa uhifadhi kwa maana ya kipimo cha rasilimali. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, tunafikiria kufanya hivyo, hatukusudii kuunganisha zote kwa pamoja, tunaona pia itatuletea changamoto lakini kwa sasa tunakusudia walau kuunganisha *TAWA* na Ngorongoro ili tuweze kugawanya *resources* ziende zikasaidie zaidi kuimarissha uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kwamba nani ana mzigo mkubwa zaidi, na kwamba tunamuongeze mzigo *TANAPA*, mwenye mzigo mkubwa zaidi ni *TAWA*. Na hata hivyo, kwamba *TAWA* maeneo yake yanachukuliwa, ni kweli yanachukuliwa lakini pia maeneo ya mapori ya akiba pia yanaongezeka; kwa mfano hapa nimeataj Pori la Akiba la Kilombero linaongezeka na linaongezeka ukubwa pia kwa zaidi ya *square kilometer* 5,000, sasa hivi lina *square kilometer* 2,500, hicho kiini ambacho bado kipo hai.

Mheshimiwa Spika, lakini tunapoongeza na hii milima na misitu ambayo ipo hapa jirani katika Pori la Akiba la Kilombero litakuwa na zaidi ya *square kilometer* 7,500. Kwa hivyo, litakuwa eneo kubwa sana na eneo lote hili linaweza likatumika kwa shughuli za uwindaji na shughuli nyingine za matumizi ya rasilimali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tunaongeza pia mapori ya akiba mengine ambayo yapo katika pipeline katika hatua mbalimbali ndani ya Serikali ikiwemo eneo la Wamimbiki, Lake Natron na Wembele tumesema hapa asubuhi kwenye swalii. Maeneo yote haya pia tunaongeza kule magharibi eneo la Luganzo Tongwe, tunatengeneza pori la akiba, haya maeneo ni makubwa sana na yataenda kuimarissha shughuli za uwindaji wa kitalii ambao unasimamiwa na Taasisi ya *TAWA* na kama tutafanikiwa

kupitisha mapendeleko yetu kama yatakuja hapa Bungeni basi tutakuwa na hiyo taasisi moja mpya ambayo itasimamia maeneo yote ya hifadhi za wanyamapori nje ya maeneo ya Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Spika, swali lingine ambalo limejitokeza sana ni eneo la Mradi wa *REGROW*, Mheshimiwa Naibu Waziri amefafanua hapa kiasi fulani. Nilipenda tu kuongeza kwamba Mradi wa *REGROW* ambao unalenga kukuza utalii kanda ya kusini, ni mradi wa kuhifadhi lakini pia kukuza shughuli za utalii. Kwa hivyo, tunachokifanya katika Pori la Akiba la Selous kubadilisha matumizi ya sehemu ya eneo hilo kuwa Hifadhi ya Taifa ni katika jitihada hizohizo za kuimarisha uhifadhi lakini pia kukuza utalii. Kwa hivyo, Benki ya Dunia hawajasema neno lolote lile kwamba watasitisha utekelezaji wa mradi huu katika eneo hilo na wanaunga mkono kwa sababu malengo yapo palepale.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kuna suala la *UNESCO* kwamba hatujawaarifu *UNESCO* kwamba pengine tutapoteza hadhi ya kuwa eneo la Urihi wa Dunia, hapana. Eneo hili bado ni mali ya Serikali na kwa kuwa lipo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, linasimamiwa na msimamizi mmoja kwa maana ya *administration* yake na msimamizi huyu ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, hizi taasisi zote zinafanya kazi kusimamia mali ambazo zipo chini ya Wizara ambazo ziko chini ya *custodian* wake mkuu ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara. Kwa hivyo, iwe katika hadhi ya pori la akiba ama Hifadhi ya Taifa bado msimamizi/mmiliki ni yuleyule mmoja ambaye amepewa dhamana ya kusimamia naye ni Katibu Mkuu. Kwa hivyo, *UNESCO* hawatoweza kubadili kutunyang'anya hiyo hadhi kwa sababu tumepandisha tu hadhi ya kiuhifadhi zaidi tumebadilisha matumizi sasa inakuwa Hifadhi ya Taifa kwa sababu eneo ni lilelile na simamizi ni yuleyule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa mujibu wa kanuni za *UNESCO* ile kanuni ya 172 ambayo inaeleza namna kama

nchi itaamua kubadilisha mipaka ya usimamizi katika eneo lake ama itaamua kumbadilisha msimamizi. Taratibu ambazo zitapaswa kufuatwa na nchi yetu ni kupeleka taarifa ya mabadiliko hayo ya matumizi ambayo tumeifanya na wala hakuna shida yoyote kwa sababu hatubadilishi mipaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni eneo la mifugo, kwanza hakuna makazi wala mifugo ndani ya Pori la Akiba la Selous. Mifugo ambayo inaonekana ipo katika ukanda huo wote, ipo katika maeneo mengine nje ya Pori la Akiba la Selous na haya ni maeneo ambayo pia yanahifadhiwa katika hadhi nydingine mbalimbali tofauti. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna mifugo mingi sana katika eneo la Kisarawe na pale ilipo inavamia kwenye Hifadhi ya Jumuiya ya Gonabis ambayo ni *WMA* ya wananchi. Na tumeona sasa ili kupunguza presha katika ikolojia hiyo yote basi tutamega sehemu ya hifadhi hii ya Jumuiya ya Wanyapori ya Gonabis na kuwapa wananchi ambao ni wafugaji lakini *tuta-restrict* matumizi badala ya kuruhusu wajenge makazi na waishi humo ndani ya *WMA* tutawaruhusu katika kipindi fulani fulani cha mwaka waweze kuingiza Mifugo yao katika eneo ambalo tutaliwekeea mipaka ili waweze kuchunga. Lengo ni kupunguza *pressure* katika ikolojia hiyo nzima ili wananchi pia waweze kupumua, wafugaji nao kupata mahitaji yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu, hii ni habari njema kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu wote wanaotokea mikoa ile, kwa sababu tunavyoenda kuweka mkakati wa kutengeneza Hifadhi ya Taifa pale, miundombinu ni jambo la lazima. Ilivyokuwa zamani ili ufile Selou njia rahisi zaidi ilikuwa ni kuruka kwa ndege hizi ndogo ambazo ni gharama kubwa sana lakini utalii wa picha kwa kiasi kikubwa unahitaji miundombinu mbalimbali ikiwemo usafiri wa reli, Mheshimiwa Rais tayari yuko katika mkakati wa kufanya mazungumzo lakini pia

kutekeleza mradi wa kuboresha reli ya *TAZARA*, kwa hivyo, itakuwa ni njia mojawapo ya kufika katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, pia kuna barabara tayari Mheshimiwa Rais alishaagiza ijengwe kwa kiwango cha lami. Katika mradi huu, Serikali sasa itajipanga kuhakikisha Selou na *Nyerere National Park* panafikika kirahisi zaidi kuliko ilivyo sasa kwa sababu watalii wa picha wakiwemo wa ndani ni rahisi zaidi kufika kwa njia ya barabara kuliko hizi ndege ndogo ambazo ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia kupitia mradi *REGROW* tutajenga viwanja yya ndege vidogo vidogo visivyopungua vitano. Vilevile kwa sasa tunafanya utafiti ili tuweze kujenga kiwanja kimoja cha ndege kikubwa eneo la Kisaki, nje kidogo ya hifadhi ya Taifa ya Nyerere ili iwe ni rahisi kufika katika eneo hill. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu hizo ni fursa ambazo zitakuja kwa kupata hifadhi mpya ya Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba utalii utaporomoka, hapana. Utalii hauwezi kuporomoka ndiyo utakua sasa kwa kasi zaidi kwa sababu tunaenda kuwekeza kwa nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, mapato ya *TAWA*, nimeshajibu hayatashuka. Labda moja ambalo napenda kulifafanua tena, naona na muda umenitupa mkono ni kuhusu wafanyakazi, Mheshimiwa Mlinga ameliongea kwa uchungu sana naomba nilifafanue.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi hawa ni wa Serikali kwa ujumla wake, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma, kwamba yuko kwenye taasisi gani ni jambo moja lakini jambo lingine ambalo ni la ukweli sana ni kwamba kwa kuwa ni watumishi wa Serikali stahiki zao zote za msingi kwa mujibu wa taratibu za Serikali ziko pale pale. Kwa hiyo, kama yupo kwenye *parastatal* ambayo inatoa zaidi ya kile ambacho kinatolewa na Serikali, hiyo ni bahati yake lakini kwamba wabaki palepale ni jambo ambalo linaweza

likafikiriwa, naomba nilichukue tuone kama kwa mujibu wa sheria linaweza likatekelezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata kama likishindikana pia siyo jambo bayo kwa sababu kuna maeneo mapya mengi ambayo yanaanzishwa na yanapandishwa hadhi kuwa Mapori ya Akiba na yako chini ya *TAWA* na watumishi watakaotoka katika eneo hili wanaweza kwenda kuanzisha hayo maeneo mapya. Pia sisi kama Serikali tunaona tunavyozidi kufanya maboresho ya taasisi hii mpya ya *TAWA* ndivyo ambavyo mapato yake yanakua na pengine katika hatua fulani na wao wataweza kufikia hatua hiyo ya kulipwa vizuri zaidi kama ambavyo leo wafanyakazi wa *TANAPA* wanalipwa.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ni shahidi wakati mnaanza kazi kwenye maeneo haya ya uhifadhi mlikuwa mnavaa '*chachacha*', vijana wadogo wadogo kama Mlinga pengine hawakuwahi kuziona, lakini enzi hizo kulikuwa hata viatu hakuna, sare za kuvaan kulikuwa hakuna na hata waliokuwa *TANAPA* walikuwa hawapati hayo mahitaji. Hata *TAWA* wakati inaanza hata sare pia walikuwa hawana lakini leo hii watumishi wote wa *TAWA* wana sare nzuri, wanavaa viatu vizuri, wanalipwa vizuri, wanapata stahiki zao vizuri, japokuwa katika kiwango cha chini. Kwa hivyo, kadri *TAWA* inavyoendelea kuimarika ndivyo ambavyo na wao watazidi kuboreshewa maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii na naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Hamisi Kigwangalla. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tumefika mahali pa kuiamua hoja ya Serikali kuhusiana na Azimio lilito mbele yetu

na ni Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi, wengine walikuwa wanatumia kupandisha hadhi ni ubadilishaji hadhi kama ilivyo kwenye *Order Paper* hapa, Sehemu ya Eneo la Pori la Akiba la Selou kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mapendekezo ya Ubadilishaji Hadhi  
sehemu ya eneo la Pori la Akiba la Selous kuwa Hifadhi  
ya Taifa ya Nyerere lilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote wameafiki jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote, kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuasiisi jambo hili ambalo leo na sisi Bunge tumeliwekea baraka zake rasmi sasa ambapo jambo hili linaenda kutendeka sasa. Ni jambo jema kama Wabunge walivyoshauri kwa sababu linaweka maeneo haya katika hali ambayo kiuhifadhi ni ya juu kabisa katika nchi yetu. Hakuna hadhi tena kiuhifadhi kwa maana ya maeneo ya *terrestrial*/ya Bara inayozidi *National Park*. Kwa hiyo, kwa maana ya kuifadhi viumbe na mimea ya aina mbalimbali, kwa kweli uamuvi huu ni wa maana sana. Kwa hiyo, tunawapongeza na tunawatachia kila la kheri Wizara katika kufanya jambo hili, hili jambo ni kubwa.

Tuendelee kuwaomba Wizara ya Fedha, wakati wa Bajeti kuititia Kamati yetu ya Bajeti, tulisukuma sana hoja ya kuiangalia *TANAPA*, ni ukweli usiopingika inazidi kulemewa, inafanya kazi kubwa iliyotukuka, tunaiongezea majukumu, majuzi ilikuwa Hifadhi zile tano tunaiongezea hii kubwa na ni kubwa kweli kweli na bado kuna nyingine zitaiongezeka, kwa kipato kile kile walichonacho kwa kweli watafika mahali wanaweza washindwe ku-*perform* kama tunavyotarajia. Kwa hiyo, ombi letu bado liko palepale na

hatuwaombei wahurumiwe chochote, kama tulivyosema wakati ule, tunachoomba ni kwamba wasichostahili kukatwa basi wasikatwe, hicho tu. (*Makofi*)

Amesema Mheshimiwa Susan maeneo ya Mlimba huko, maeneo haya ya Mapori ya Selou ni maporini haswa. Mara nyingi hata Halmashauri zilizoko huko kujenga zahanati kwenye vijiji vilivyoko pembedni ni ngumu, kwa hiyo, *TANAPA* analazimika kufanya ujirani mwema kwa kutoa baadhi ya *services* kama kuna kujenga zahanati, madarasa na kadhalika. *TANAPA* anapojenga hiyo zahanati au madarasa, analazimika kuilipa Serikali kodi kwa hilo alilolifanya ambalo ni jukumu la Serikali kufanya. Sasa anafanya kosa kujenga zahanati, kwa hiyo, ali pe kodi? (*Makofi*)

Ni vitu kama hivyo tu ambavyo vinafanyika hivi sasa, yaani viko waazi tu, hatuwaombei kitu kingine, tujaribu tuanze na hili kwanza la kutowalipisha kodi pale ambapo kwa kweli hawastahili kulipa, kwa vile wamefanya jambo jema. Wakileta greda la kuchonga barabara kodi, sasa barabara hizi zinazochongwa, nyingine ndiyo hizi hizi na wengine mnapita humo humo. Ikichongwa barabara kutoka Ngorongoro *gatekwenda* mpaka kule Fort Ikoma watu wote wa Mkoa wa Mara, Mwanza si mnapita barabara hiyo, ambayo ilitakiwa *TANROADS* watengeneze hiyo barabara lakini wanaitengeneza watu wa Hifadhi na kadhalika. (*Makofi*)

Wakiagiza vifaa toka nje, kwa mfano sasa hivi wao ni *paramilitary*, vifaa vyote vya kijeshi wanalipa kodi jamani? Si wanaingiza tu bandarini pale. *TANAPA* nao siku hizi wanafanya kazi hizo lakini wakileta vifaa vyao wanatakiwa walipe kodi, yaani kila wakati wanakuwa *treated different*, hizo *difference* ndiyo tunazosema ziondoke, wapate tu haki yao, kwa kuanzia watazamwe kwa jicho hilo. Kwa kufanya hivyo itawasaidia sana kwa sababu tuna eneo ambalo tunaweza kupata mapato makubwa sana siku za mbele tukizihifadhi hizi hifadhi zetu ambazo ni *competitive* kwa sasa na hata mbele tunakoenda.

Kwa kweli kwa wale mliosikia palikuwa na kamvutano kidogo hakikuwa cha nia ya kufanya chochote. Ni kama Bunge leo tulivyomaliza yaani Wabunge walitaka kwenda hata zaidi ya Waziri alichokuwa anapendekeza ndicho kilichokuwepo hapa katikati, kwamba na eneo hili nalo liingie na hili liingie lakini Waziri akasema tuanze hapa kwanza kwa wakati huu, jambo ambalo ni jema. Kwa hiyo, kwa kweli Wabunge wala hawakuwa wanapinga jambo hili wala nini ila walikuwa na malengo makubwa zaidi. Kwa ujumla wake ni hili ambalo amelieleza Mheshimiwa Waziri kwamba ni wito wa kupanga upya aina na namna za uhifadhi wetu kama walivyokuwa wanapendekeza labda *TAWA* na Ngorongoro wawe pamoja, hivyo, ifike mahali tuyapange upya maeneo yote yakae sawasawa.

Mbunge wa Liwale hayupo hapa lakini angekuwepo nadhani kuna jambo moja angeliongelea, inapokuwa Park sasa, watu wa Liwale ni Wangindo, *actually* wanaitwa Wamagingo. Wamagingo wale wana mila ya kutoka kule kwao Liwale wanakatiza Selou wanakwenda mpaka kwa Mlinga kule kunaitwa Mwaya wanaenda kuhiji, ni imani kweli kweli hiyo. Nikisema hivi msiofahamu haya mambo hamuwezi kuelewa lakini ni imani haswa kama watu wengine wanavyoenda kuhiji maeneo mbalimbali kutokana na imani zao. (*Makof/*)

Sasa inapokuwa *National Park* kukatiza hapo itakuwa *almost mission impossible*. Naomba *TANAPA* mnapochukua eneo hili mkumbuke yako mambo kama hayo ambayo ni *cultural/msiende* kuwa kikwazo cha moja kwa moja. Nendeni mkaone namna gani ya ku-*facilitate* jambo hilo, wenyewe wanaita kwenda Ngende. Kwa hiyo, hiyo njia ya kwenda Ngende iendelee pamoja na kwamba inakuwa ni Hifadhi. (*Makof/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kama usipoolewa jambo hilo utalionia ni jepesi lakini ni gumu kweli kweli. Nakumbuka enzi zile mimi niliitwa mbele ya Mheshimiwa Kawawa akiwa

Katibu Mkuu wa Chama, kwa nini unazuia watu wangu kwenda Ngende? Ilikuwa kesi kubwa sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri, kwa kweli tunawatakia kila la kheri katika jambo hili. Tunaamini kabisa tutafanikiwa na litakuwa ni jambo jema. *TANAPA* wana kazi kubwa kwelikweli ya kujenga miundombinu inayofanana na masuala ya utalii wa picha kwa huko Kusini, ni kazi ya gharama kubwa kweli, madaraja na kufungua barabara huko Kusini, viwanja vyta ndege, kujenga nyumba, magari, magreda na kadhalika na hiyo miradi hiyo misaada ya *REGROW*na mingine itasaidia kwa kiasi fulani. Naamini muda si mrefu tutarudi tena hapa kuiongezea *TANAPA* maeneo mengine.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nimalizie kwa kuwaomba kweli Wizara ya Fedha tuwatazame *TANAPA* kipekee vinginevyo watashindwa kubeba mzigo ambao tunawatarajia wafanye. *So far* wamekuwa ni watu ambao wanafanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kazi zilizopangwa leo zimekamilika kama zilivyopangwa lakini naomba niwaambieni tu kwamba Mheshimiwa Miraji Mtaturu kwa wale waliokuwa wana mashaka mashaka oooh sijui Mahakama, ni Mbunge halali wa Singida Mashariki. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, mambo haya mengine mtayasikia wenyewe huko nje mtakapotoka sitaki kuyasema, si ndiyo leo tarehe 9 bwana au leo tarehe ngapi, ndiyo maana tunasema hivyo. Ukiheshimu mamlaka, ukashirikiana na mamlaka huwezi kupata matatizo haya, haiwezekani. Bahati mbaya Spika hawezi kutokeza kila wakati kujibu kila mtu akienda kwenye mitandao huko na mimi niko najibu lakini ningekuwa najibu kila wakati, sijui wangeweka wapi nyuso zao kwa sababu majibu yapo.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge kama hili linaloendelea wewe uwe unaumwa lakini uko *conscious* iyo unaumwa uko mahtuti kiasi hicho, hivi kumjulisha Spika tu,

Mheshimiwa Spika mimi sitaweza kuhudhuria Bunge hili la Kumi na Sita kwa sababu kama unavyojuu niko hospitali bado naendelea kuumwa na kikaratasi cha daktari wako ukiweza unakibandika pale unanitumia, kuna ubaya gani? Si ndiyo taarifa umeshatoa? Hata ukipiga simu tu si ndiyo taarifa umetoa? Hata ukiandika meseji tu si ndiyo taarifa umetoa? Kwa hiyo, mengine yote unafanya isipokuwa kumwambia Spika, hapana, mwaka unapita, nakuona tu huko wapi. Mengine yote unawenza kufanya lakini kuwasiliana na huyu hufanyi. Haiwezekani itafika mahali watu wataruka na wewe tu na usipige kelele ooh, sijui imekuwa imekuwa, umeyataka mwenyewe, kwa sababu taratibu mnazijua.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tukifua taratibu wala hatuna ugomvi. Habari ya fomu zile za maadili ni lazima tujaze, ni takwa la Katiba. Hata Mheshimiwa Mbwe alipokuwa Magereza alinilandikia barua Desemba illyopita kwamba bwana niko mahali ambapo siwezi kujaza zile fomu Segerea lakini nikitoka nitajaza, kulikuwa na ugomvi? Alipotoka amejaza lakini husemi, huandiki, huwasiliani, hufanyi nini, wewe unapuyanga na yako tu, ukitoka una yako, unamtandika huyo huyo unayetakiwa uripoti kwake.

Waheshimiwa Wabunge, mambo hayaendi hivyo na Katiba inakwambia mpe nakala mbili Spika, tena wengi ninyi hampeleki nakala zenu kwa Spika, ingawaje huwa nazitafuta huko nazipata lakini mjue nakala zile mnapaswa mzilete kwa Spika, ndivyo Katiba inavyosema halafu na mimi napaleka sasa kule kunakotakiwa. Wala sijawahi kuchungulia fomu ya mtu, mimi sijui mtu ana mali ngapi, wala sihangaikagi na jambo hilo. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi kwamba ataona kwamba sina kitu au nina kitu, ni utaratibu tu umewekwa. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwa kweli kwa maoni yangu mimi kama hili ni la kujitakia tu, ni kama lile la yule wa Arumeru Mashariki mwanzoni, la kujitakia tu. Wewe unakaa karibu mwaka huwasiliani chochote basi hata chama chako kiniambie, bwana Mbunge wetu hayupo anaumwa, hicho chama waliwahi hata siku moja? Hata

Kiongozi wa Upinzani basi uniambie, bwana nina mgonjwa wangu hivi na hivi usimuone hajaja Bungeni hayupo kwa sababu hii, aliwahi? Hata *Chief Whip* wao basi, bwana eeeh katika Wabunge wangu kuna huyu yuko hivi ana udhuru fulani, mliwahi? Kwa hiyo, mimi nikichukua hatua mwisho ndiyo wa kulaumiwa kweli? Haiwezekani, haiendi hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ndiyo hivyo jamani, Mheshimiwa Mtaturu, hongera sana tuendelee kuchapa kazi. Wananchi wa Singida Mashariki mnaye mwakilishi. Mengine hayo ikibidi tutayajibu huko huko kwenye mitandao, ikibidi lakini mpaka sasa sioni umuhimu wa kufanya hivyo lakini tuelewane haonewi mtu kwa sababu yoyote ile, likikupata umelitaka mwenyewe, umelilea mwenyewe, ujeuri tu, kiburi ambacho hakina tija, hakina nini, sasa tunavuna tunachopanda. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, naomba nahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 10 Septemba, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*